# Hatari za Ukanamungu Na njia za Makabiliano

KIMEANDALIWA NA

Idara Kuu ya Sira na Sunnah

Baraza Kuu la Mambo ya Kiislamu - Cairo

Usimamizi na Uwasilishaji


**Profesa Muhammad Mukhtar Juma**

**Waziri wa Waqfu**

**Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Mambo ya Kiislamu**

**Mjumbe wa Chuo cha Utafiti wa Kiisilamu**

**Kimefasiriwa na**

**Prof. Dr. Ali Ali Shaban**

**Chuo Kikuu cha Al-Azhar**

**Cairo - Misri**

**Kimepitiwa na**

**Prof. Dr. Issa Ziddy**

**Chuo Kikuu cha SUZA**

**Zanzibar - Tanzania**

Kimepitiwa Tafasiri ya kiswahili na
Profesa/ Ayman Alasar



1443 AH / 2022

**WAZIRI WA MAMBO YA WAOFU**

MJUMBE BARAZA LA TAFITI ZA KIISLAMU

Shirika Kuu la Vitabu la Misri

Shirika Kuu la Vitabu la Misri

Mkurugenzi Mkuu.
Dr. Haitham Al-Haj Ally

# Hatari za Ukanamungu Na njia za Makabiliano

MAANDALIZI
**DR. MOHAMMAD MUKHTAR JUMA**
**WAZIRI WA WAQFU**

Chapa ya kwanza
Shirikika Kuu la Vitabu la Misri 2021. S.L.P235 Ramsis 1194 Kornesh Nail – Ramlatu Bolaq Cairo.
Namba ya Post: 11794.
Simu: 202257775109 ndani 149 Fax: 20225764276.
Uchapishaji na utekelezaji
Kituo cha uchapishaji Shirika kuu la Vitabu nchini Misri

Mitazamo iliyopo ndani ya kitabu si msimamo wa shirika bali ni msimamo wa mtunzi kwa hatua ya kwanza.

Haki ya uchapishaji inalindwa na Shirika Kuu la vitabu la Misri. Ni marufuku kuchapisha au kusambaza au kutoa kopi au kuiga kwa hali yeyote ile isipokuwa kwa ruhusa ya Shirika Kuu la Vitabu la Misri au kwa maelekezo ya pande husika.

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

**﴿Basi jua kuwa hapana mungu ila Mwenyezi Mungu tu, na uombe msamaha kwa dhambi yako na kwa waumini wanaume na wanawake, na Mwenyezi Mungu anajua mahali penu pa kwenda na kurudi, na mahali penu pa kukaa﴾** (Sura 47:19)

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu,*

*Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu*

# Utangulizi

Sifa njema na shukrani zote ni za Mola Mlezi wa walimwengu wote, na swala na amani ziwe juu ya mwisho wa Manabii na Mitume yake, bwana wetu Muhammad bin Abdillah, na juu ya familia na Masahaba zake, na kila anayeufuata uongozi wake hadi Siku ya Hukumu.

Ingawa tunajua kuwa Ukanamungu una sababu nyingi za kiakili, kisaikolojia, kifalsafa na kijamii, pamoja na ukali wa vikundi vyenye misimamo mikali, tunajua pia kwamba kuna makundi wanaochukia dini yetu, umma wetu, nan chi zetu, wanaojitahidi kusaidia makundi ya wakanamungu na kueneza wazo la Ukanamungu kwa nia ya kuharibu jamii zetu kindani, kwa kutumia ugaidi

unaoibuka wakati fulani, na kwa Ukanamungu wakati mwingine, au kwa kuchochea ugomvi wa kikabila, au wa kimadhehebu, au kwa kueneza uvumi na uwongo. Ukanamungu ukawa umefanyika kisiasa, na unasaidiwa kwa mali, kwa nia ya kuchangia kusababisha fujo na machafuko, maana mambo mengi katika jamii zetu hayakuwa tena ya kisilika wala ya kikawaida. Mipango ya maadui ikawa inalenga kuharibu pande zote na viungo vyote vya maisha yetu, kwa hivyo kila mtu anayefuata tabia ya ibada ya kidini wanajaribu kumsogeza kuelekea misimamo mikali na ugaidi, na yule anayechukia dini, wanajaribu kumvuta kuelekea Ukanamungu na kushikilia mawazo ya uharibifu, na yule wanaomkuta ana mwelekeo mkali wa kidini, kimadhehebu, kikabila, au wa kitaifa wanajitahidi kuuimarisha mwelekeo huo moyoni mwake. Mambo haya yanatuhimiza kuwafahamisha watu hatari za mizushi hiyo mibaya.

Mipango ya maadui inadhamiria kueneza Ukanamungu uliobuniwa kisiasa au uliosaidiwa

kwa mali ili kuondoa maadili mema kutoka kwa mkanamungu, na kuiondoa maadili ya kujiangalia na kumuangalia Muumba aliyeumba ulimwengu na maisha. Basi haitakuwepo mbele ya yule mkanamungu isipokuwa kuiepukia sharia kwa kadiri awezavyo.

Kuna tofauti na hitilafu kubwa kati ya uhuru wa imani na malengo ya kisiasa chini ya jina la uhuru wa kuchagua. Uhuru wa imani umedhaminiwa, lakini malengo yanayoelekezwa ili kuchochea machafuko na kuangusha madola au kuyadhoofisha na kuyabomoa kindani ni kitu ambacho hakuna mtu awezaye kukikubali….

Ingawa tunasisitiza kwamba Uisilamu umejengwa juu ya msingi wa uhuru wa kuchagua, kama asemavyo Mwenyezi Mungu:

﴿**Hakuna kulazimisha katika dini. Bila shaka uongofu umeshapambanuka na upotevu**﴾ (2:256), na anasema: ﴿**Na kama angelitaka Mola wako, bila shaka wangeliamini wote waliomo katika ar-**

**dhi. Basi je, wewe utawalazimisha watu kwa nguvu hata wawe waumini﴾** (10:99), na anasema: **﴿Na lau Mola wako angelitaka, bila shaka angeliwajaalia watu kuwa ni umma mmoja. Na wao wangali wenye kuhitilafiana, Isipokuwa wale ambao Mola wako amewarehemu; na kwa hiyo amewaumba﴾** (11:118-119).

Ujenzi wa nchi hautegemei dhamiri peke yake, maana lazima kuweko kwa sheria iliyopangwa kuisimamia na kuiimarisha. Tunaamini na tuna yakini kwamba Mungu (ametukuzwa na kutakaswa) Allah huzuia watu kufanya mambo ambayo yamekatazwa kwa nguvu ya utawala zaidi kuliko kwa Qurani. na kwamba haifai kuwaacha watu katika machafuko bila mfumo au sheria inayotawala.

Hakika tunasisitiza - pia - kwamba pamoja na heshima yetu kamili kwa utawala wa sharia, na msisitizo wetu juu ya kushikilia bendera yake, kukiimarisha cheo chake na utekelezaji wa hukumu za sheria na dola la sheria, tunasisitiza pia kwamba kujitahidi kuamsha dhamiri, kukuza hi-

sia za Imani, na kumcha Mungu (Ametukuzwa na kutakaswa) ni muhimu sana kwa faida ya mtu na jamii. Maana ni vigumu kumwekea kila mtu askari, au mlinzi wa kumlinda, lakini ni rahisi kulea katika kila mtu dhamiri hai ambayo humhimiza na kumsukuma kwa haki, ili ajue kuwa anaangaliwa na Asiyeshikwa na usingizi wala kulala, Mwenyezi Mungu mtukufu anasema: ﴿**Je! Hukuona kwamba Mwenyezi Mungu anajua vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini? Haupatikani mnong'ono wa watu watatu ila Yeye huwa ni wa nne wao, wala wa watano ila Yeye huwa ni wa sita wao, wala wa wachache kuliko hao wala zaidi ila Yeye huwa pamoja nao popote walipo. Kisha Siku ya Kiyama atawaambia yale waliyoyatenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kila kitu**﴾ (60:7), na Anasema: {**Na bila shaka tumemuumba mwanadamu, na Sisi tunayajua yanayopita katika nafsi yake, na Sisi tuko karibu zaidi na yeye kuliko mshipa wa shingo**﴾(50:16), na Anasema: ﴿**Na kila mwanadamu tumemfungia matendo yake shingoni mwake, na tutamtolea Siku ya Kiyama Daftari atakalolikuta**

**limekunjuliwa, soma Daftari lako. Nafsi yako inakutosha leo kukuhesabu.﴾** (17:14), na Anasema: **﴿Na tunaweka mizani za uadilifu kwa Siku ya Kiyama, basi nafsi yoyote haitadhulumiwa chochote. Na hata ukiwa uko uzito wa chembe ya hardali, tutaileta. Na Sisi tunatosha kuwa Wenye hesabu﴾** (21:47), na Anasema: **﴿(Mwenyezi Mungu) anajua hiana ya macho na yanayoficha vifua﴾** (40:19). Nabii wetu (SAW) alisema wakati bwana wetu Jibril (amani iwe juu yake) alipomuuliza juu ya ihisani, na yeye (SAW) akasema: (Ihsani ni kumwabudu Mungu kana kwamba unamuona, lakini ikiwa humuoni, hakika Yeye anakuona).

Hakuna shaka kuwa Ukanamungu na kupotoka kutoka njia ya Mungu na silika yake Aliyoiweka ndani ya watu una maovu na madhara yasiyoweza kuhesabika juu ya mtu binafsi, jamii, mataifa na watu. Miongoni mwake: Upotevu wa maadili, kuenea kwa uhalifu, kutenganisha kwa familia na jamii, utupu wa kiroho, usumbufu wa kisaikolojia, na kuenea kwa mizushi ya hatari kama vile, kujiua makusudi, ushoga, na unyogovu wa kisaikolojia.

Kufuata njia ya Ukanamungu na upotevu ni kujidhuru mwenyewe, na kujiharibu katika dunia na Akhera. Hali ya wakanamungu ni chungu, imejaa magonjwa na tata za kisaikolojia, Mwenyezi Mungu anasema: ﴿**Na atakayejiepusha na mawaidha yangu, basi hakika yeye atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua na hali ni kipofu, Atasema: Mola wangu! Mbona umenifufua kipofu, na hali nilikuwa (duniani) ni mwenye kuona? (Mwenyezi Mungu) atasema: Ndivyo vivyo hivyo. Aya zetu zilikufikia, ukazisahau. Na hivi ndivyo leo, utasahauliwa, Na hivi ndivyo tutakavyomlipa kila apitaye kiasi, na hakuamini Aya za Mola wake. Na bila shaka adhabu ya Akhera ni kali zaidi na yenye kudumu Zaidi**﴾ (20:124-127), na anasema: ﴿**Na waliokufuru waangamizwe, na atavipoteza vitendo vyao!**﴾ (47:8).

Adhabu za kidunia na mila na desturi peke yake - haijalishi ni sahihi jinsi gani - haziwezi kudhibiti harakati za mtu ulimwenguni, isipokuwa mtu huyu awe na uhusiano wa karibu na Muumba

wake. Udini wa kweli, humlinda mtu na upotovu, maana anajua kuwa matendo yake yatahesabiwa kwake, na kwamba atasimama mbele ya Mwenyezi Mungu ambaye hakuna siri hapa duniani au angani inayofichika kwake, Mwenyezi Mungu anasema: ﴿**Na wasimamisheni; hakika wao wataulizwa**﴾ (37:24).

Lakini, udini tunaoutafuta na tunaojitahidi kuufikia ni udini wa kweli tu unaosafika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, sio wa kirasmi, wa kimatumizi wala wa kisiasa.

Hakuna shaka kuwa hali za udini rasmi na udini wa kisiasa ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazowakabili jamii za Kiarabu na Kiislamu, hasa wale ambao wanashughulikia muonekano na umbo, hata ikiwa ni kwa gharama ya maadili na ukweli, hata ikiwa mwenye lile umbo hana madaraka ya kibinadamu wala ya kimaadili ambayo humfanya awe mfano. Hiyo ni kwa sababu mwenye umbo la kirasmi ambaye mienendo yake

inapingana na mafundisho ya Uislamu, anahesabiwa kama ni kifaa cha ubomoaji, kinachowatenga watu mbali na dini. Basi, ikiwa umbo ni umbo la mwenye dini, lakini vitendo ni vitendo viovu, vya uwongo na usaliti, uhaini, kutotekeleza ahadi, au kula mali ya watu kwa dhuluma, basi hali hapa ni hatari sana katika kuwaondoa watu wasifuate dini ya Mwenyezi Mungu, na kuwaweka mbali nayo. Zaidi ya hayo, anayefanya hivyo anaingia katika unafiki., Mtume wetu (SAW) amesema: (Alama za mnafiki ni tatu, anapozungumza husema uongo, na anapoahidi huvunja ahadi, na anapoaminiwa hufanya hiana.), na anasema (SAW): Mtu aliye na sifa hizi nne ni Mnafiki Mtupu. Na aliye na moja katika hizo basi atakuwa na sehemu ya unafiki mpaka aiache: (Anapoaminiwa hufanya hiana, na anapozungumza husema uongo, na anapoahidi huvunja ahadi yake, na anapogombana na mtu hupita kiasi katika uovu).

Vivyo hivyo, wale ambao huingiza udini katika ibada na kufanya bidii lhali hawaelewi dini, kwa

kuwakufirisha watu, kubeba silaha na kuwavamia watu, kama walivyofanya khawaarij ambao walikuwa ni miongoni mwa watu wanaoswali na kufunga sana, na kulala kidogo, lakini hawakujifunza elimu ya kutosha ya dini inayowazuia kumwaga damu, ndiyo mana waliwavamia watu na panga zao. Ingekuwa bora kama wangelitafuta maarifa kwanza, kama Imam Al-Shafi'i (Mungu amrehemu) alivyosema, ingewazuia na kufanya hivyo.

Uislamu ni dini ya huruma kwa wote, na kila kitu kinachokutenganisha na huruma kinakuweka mbali na Uisilamu. Jambo la muhimu ni tabia sahihi na sio kusema tu. Watu wa kale walisema: Matokeo ya kitendo cha mtu kwa watu elfu ni bora kuliko matokeo ya maneno ya watu elfu kwa mtu mmoja.

Lakini, vitendo vyote vya ibada havizai matunda visiposafisha tabia na maadili ya mtu, kwa hivyo ikiwa Swala za mtu hazimzuilii na machafu na ubaya, basi hakuna malipo kwa Swala zake, na

mtu yeyote ambaye Saumu yake haikumkataza asiseme uwongo, basi hakuna malipo kwa Saumu yake. Nabii wetu (SAW) anasema: “Asiyeacha kusema uongo na kufanya uongo, Mungu hamhitajii kuacha chakula na kinywaji chake”. Na Mwenyezi Mungu hakubali Zaka wala Sadaka isipokuwa zimetoka kwa pesa halali. Nabii wetu (SAW) anasema: (Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwema, hakubali ila vyema) na anasema: (Mungu hakubali Swala bila ya kujitakasa, wala Sadaka kutoka mali haramu).

Udini wa kisiasa ni hatari zaidi kuliko udini huu wa kirasmi. Kauli hiyo inamaanisha kwamba wale watu ambao huchukua dini kama njia ya kufikia madaraka kwa kutumia hisia za kidini na mapenzi ya watu kwa dini yao - hasa watu wa kawaida - na kuwadanganya kwa kusema kuwa lengo lao la kufikia madaraka ni kutumikia dini ya Mungu tu, na kujitahidi kuinusuru na kuitilia nguvu, ingawa ukweli wao ni kinyume cha hayo. Hakika hao huchangia kuwazuia watu wasifuate

dini ya Mungu, na kukuza msimsmo mkali wa upinzani. Kwa hivyo, ni wajibu wa kila mwenye ikhlasi kwa dini yake awe mfano wa kuigwa kwa vitendo vyake kabla ya maneno yake, na kuifunga upya nia yake kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo lazima tuufanye Uislamu uwe ukweli ambao tunaishi ndani yake na unaishi ndani yetu, na kushikilia sababu zote za maendeleo na utamaduni ili tuhakikishe mfano ambao unapaswa kushikiliwa na kila Muislamu anayeelewa dini yake, ambaye ana hamu ya kumpendeza Mola wake, anayeweza kukabili hoja kwa hoja na mantiki, na kukumbuka aliyoyasema Mwenyezi Mungu: ﴿**Hakika wewe huwezi kumuongoa umpendaye, lakini Mwenyezi Mungu humuongoa amtakaye. Na Yeye ni Mwenye kuwajua vyema wenye kuongoka**﴾ (28:56).

Hakika, wajibu wetu ni kufikisha ujumbe ulio wazi ili Mwenyezi Mungu atuwie radhi katika kumlingania Yeye, (Utukufu uwe wake) kwa hekima na mawaidha mema, Mwenyezi Mungu anasema: ﴿**Ulinganie katika njia ya Mola wako kwa**

hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako Yeye ndiye Mwenye kuwajua vyema waliopotea njia yake, na Yeye ndiye Mwenye kuwajua vyema wenye kuongoka﴾ (16:125)

Mungu ndiye Mwenye kuelekeza na kuongoza kwenye njia sahihi, na Yeye ndiye anatutoshea na Mwenye kutegemewa.

***Profesa Mohamed Mokhtar Gomaa Mabrouk***

*Waziri wa Waqfu*

*Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Mambo ya Kiislamu*

*Na Mjumbe wa Chuo cha Utafiti wa Kiisilamu*

*Al-Azhar Al-Sharif*

## Maana ya Ukanamungu

Ukanamungu ni hatari kubwa zaidi inayogeukia silika halisi, na imani safi, pia ni kurudishwa nyuma kiakili na kiroho. Matumizi ya neno hilo yameendelea wakati wote na zama zote. Kilugha, neno hilo linaelezwa kwa maana mbalimbali, lakini tafiti za kisasa zinalihusisha na maana moja tu kati ya hizi, na kuliweka katika mfumo maalumu.

**Ukanamungu kilugha:**

Ukanamungu kwa Kiarabu ni Il***ḥ***ad, neno hili lina maana kadha za kilugha:

Il***ḥ***ad ina maana ya kimsingi ambayo ni "kugeuka na kubadilika", na maana hii kuu ina matawi kwa maana mbalimbali kulingana na maana hii ya asili, na tutaeleza maana hizi kama ifuatavyo:

A - Asili ya maana za Il***ḥ***ad ni: kugeuka na kubadilika kwa jambo; imesemwa: maana ya

Ilḥad kilugha ni kugeuka mbali na uadilifu, na amegeukia kitu, yamaanisha amekielekea.

B - Kaburi: shimo lililo upande wa kaburi, kwa sababu iligeuka kutoka katikati kwenda upande, au shimo ambalo liko upande wa kaburi panapowekwa wafu.

C - Kisima kisicho sawa: kisima chenye Ilḥad.

D- Mojawapo ya maana za Ilḥad ni makimbilio, kwa sababu mkimbizi anaelekezwa kwake, na kutoka kwa maana hiyo ni msemo wa Mwenyezi Mungu: {**Wala sitapata makimbilio ila kwake Yeye tu**} (72:22), na maana yake: hakuna makazi, ambapo mnaweza kuyageukia.

E- Mojawapo ya maana za Ilḥad pia ni kujadiliana na kuhojiana.

F- Vilevile mojawapo ya maana za Ilḥad ni Ukanamungu, kwa sababu inaelekea mbali na haki kwa udhalimu na aina mbalimbali za makosa na maovu.

G- Vilevile inamaanisha dhuluma kwa jumla, maana inayotokana na msemo wa Mwenyezi Mungu: ﴿**Na yeyote atakayetaka kufanya upotofu humo kwa dhuluma, basi tutamwonjesha adhabu yenye kuumiza**﴾ (22:25), maana yake: Amegeuka kwa kufanya dhuluma.

**Ukanamungu katika Qurani Tukufu:**

Mzizi wa neno Il**ḥ**ad (lahada) umetajwa katika Qur'ani tukufu mara sita, mara moja katika mfumo wa: "Il**ḥ**ad", mara tatu katika mfumo wa kitenzi cha wakati uliopo: "yulhiduna", na mara mbili katika mfumo wa nomino: "multa**ḥ**ada" (makimbilio).

Kwanza: Neno "Il**ḥ**ad" (upotofu) limetajwa katika maneno ya Mwenyezi Mungu: ﴿**Hakika wale waliokufuru na kuzuilia (watu wasifuate) njia ya Mwenyezi Mungu na Msikiti Mtukufu ambao tumeujaalia kwa ajili ya watu wote; wakaao humo na wageni sawasawa. Na yeyote atakayetaka kufanya upotofu humo kwa dhuluma, basi tutamuonjesha**

**adhabu yenye kuumiza**﴾ (22:25). Katika tafsiri yake, Al-Tabari ametaja maoni yote yaliyotajwa katika maana ya "Il***ḥ***ad" kugeuka kwa dhuluma kwenye Msikiti Mtukufu, na alifupisha maoni hayo kama ifuatavyo:

1- Ni ushirikina kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuwaabudu wengine pamoja naye, i.e Msikitini

2- Ni kuhalalisha iliyo haramu ndani ya Msikiti Mtukufu au kuifanya humo.

3- Ni dhuluma, kwa kuhalalisha makusudi maovu Msikitini.

4- Ni ukiritimba wa chakula huko Makkah.

5- Vitendo vyote ambavyo vilikuwa vimekatazwa.

Yote hayo ni maoni kulingana na kuhalisisha maana ya Il***ḥ***ad kuwa ni “dhuluma. Kwa hivyo yalielekea kueleza maana ya dhuluma, kisha Al-Tabari alipendekeza kuwa yanayokusudiwa kwa “dhuluma” ni kutomtii Mwenyezi Mungu kwa

jumla kulingana na maana ya Aya, alisema: Wazo lililo muhimu kabisa katika mawazo tuliyoyataja hapo juu ni lile la Ibn Mas'ud na Ibn Abbas (Mungu awe radhi nao), ya kuwa dhuluma hapa maana yake ni kila tendo asilolipenda Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa maaana ya Aya.

Pili: Neno "Il**ḥ**ad" limetajwa katika sehemu tatu katika mfumo wa kitenzi cha wakati uliopo: "yulhiduna":

1- Kauli ya Mwenyezi Mungu: ﴿**Na ni ya Mwenyezi Mungu tu majina yaliyo mazuri kabisa, basi muombeni kwayo. Na waacheni wale wanaoharibu utakatifu wa majina yake, hao watalipwa waliyokuwa wakiyatenda**﴾ (7:180).

Maana ya "wanaoharibu utakatifu wa" majina ya Mungu ni yale waliyoyafanya washirikina kwa kuyakana, kuyaongezea, na kuchukua kutoka kwayo majina ya miungu yao.

Al-Tabari amesema: Washirikina walikosea majina ya Mwenyezi Mungu kwa kuzibadilisha

maana zake, na kutumia baadhi yake kama majina kwa miungu yao, kama walivyofanya kwenye jina la "Uzza" lililotokana na jina la Mwenyezi Mungu "Aziz" (Mwenye nguvu). Ibn Katheer, na Mujahid walisema hivyo hivyo.

2- Msemo wa Mwenyezi Mungu: ﴿**Na kwa yakini tunajua kwamba wao wanasema: Hakika yuko binadamu mmoja anayemfundisha. Lugha ya huyo wanayemuelekea ni ya kigeni, na hii ni lugha ya Kiarabu bayana**﴾ (16:103) Washirikina wa Makkah walidai kuwa mtumwa wa kirumi alikuwa anamfundisha Mtume (SAW) Qur'ani, basi Mwenyezi Mungu akasema: Mnayemrejelea ni A'jami. Al-Tabari alisema: "Ulimi wa mtu mnaomrejelea na mnaodai kuwa anamfundisha Muhammad ni A'jami, sio mwarabu. Kwa sababu ilisemekana kuwa walidai kuwa mtumwa wa kirumi alikuwa anamfundisha Mtume (SAW) Qur'ani, Mwenyezi Mungu akasema: ﴿**Na kwa yakini tunajua kwamba wao wanasema: Hakika yuko binadamu mmoja anay-**

**emfundisha. Lugha ya huyo wanayemuelekea ni ya kigeni, na hii ni lugha ya Kiarabu bayana﴾** (16:103).

3- Maneno ya Mwenyezi Mungu kuwa: **﴿Hakika wale wanaoupotoa ukweli uliomo katika ishara zetu hawafichiki kwetu﴾** (41:40). Wafasiri wa Qur'ani walitofautiana juu ya maana ya Il***ḥ***ad katika Aya za Mwenyezi Mungu kwenye maoni kadhaa, miongoni mwa maoni hayo ni:

1- Upinzani wa washirikina kwa Qur'ani kwa kejeli na kuidhihaki.

2- Mradi ni: kuonyesha uwongo waliousema kuhusu Aya za Mwenyezi Mungu.

3- Mradi ni: wanaikaidi.

4- Mradi ni: kufuru na ushirikina.

5- Mradi ni kuonesha kuwa wameibadilisha maana ya Kitabu cha Mungu.

Al-Tabari ameonesha kuwa hakuna oni lolote miongoni mwa hayo linaloweza kutawala men-

gine, kwa sababu ya ukaribu wao katika maana ya kilugha. Kwa hivyo, Aya zinagusa maana zote hizi na kuzikumbata. Anasema: “Maneno haya yote tuliyoyataja katika tafsiri ya neno hilo yanafanana kimaana, kwa sababu Il***ḥ***ad na La***ḥ***d yanamaanisha kugeukia Aya za Mwenyezi Mungu, kuziepukia kwa kuzikana, kuzidhihaki, mabishano, kujitenga nazo, ukaidi, kwa kuziapotosha na kuzibadilisha maana yao. Na hakuna msemo unaostahiki kutawala kuliko ule tuliosema, na kuonesha kwamba wao ndio waliharibu maana za aya za Mungu, kama Mola wetu, alivyoonesha.

Tatu: Neno "makimbilio" (multa***ḥ***ad kwa Kiarabu) limetajwa mara mbili: katika Aya ya Mwenyezi Mungu: ﴿**Na soma Wahyi uliopewa katika Kitabu cha Mola wako, hapana wa kubadilisha maneno yake, wala wewe hutapata makimbilio isipokuwa kwake.**﴾ (41:27), na kauli yake: ﴿**Sema: Hakika hakuna yeyote awezaye kunilinda na Mwenyezi Mungu, wala sitapata makimbilio ila kwake Yeye tu**﴾ (72:22), nalo lenye maana moja katika Aya hizi mbili: "makimbilio"

Kwa msingi huu, maana ya Qur'ani inalingana na maana ya kilugha inayomaanisha "mwelekeo", ikiwa mwelekeo huu unatoka mbali na haki na uadilifu kwa ushirikina, ukosefu wa haki, kutotii, au "mwelekeo" kwa jumla.

**Ilḥad (Ukanamungu) Katika Sunnah ya Mtume (SAW):**

Katika Sunnah ya Mtume (SAW), mzizi wa neno Laḥada ulitokea katika Kauli ya Nabii (SAW): "Watu waliochukiwa sana na Mwenyezi Mungu ni watatu: Mtu mwenye kufanya machafu katika Msikiti mtakatifu, anayetafuta ada za Jahiliya (zama zilizotangulia Uisilamu) katika Uislamu, na anayetafuta kumwaga damu ya mtu bila ya haki " Omar (RA) alisema: "Ukiritimba wa chakula katika Makkah ni Ilḥad (mgeuko mbali na haki " Hiyo ni: dhambi, udhalimu na mwelekeo ulio mbali na ukweli.

Kwa msingi huu, Qur'ani au Sunnah hazikuweka maana moja maalumu ya kilugha kwa neno

Ilḥad. Bali Aya zote, zilimaanisha “mwelekeo” kwa jumla, na kuachana na uadilifu, na unyoofu. Vilevile maana yake ilikumbatia kila aina ya dhambi na udhalimu, hata ukiritimba wa chakula katika Makkah.

**Ilḥad katika maana ya kiistilahi:**

Ikiwa maana ya kilugha ya Ukanamungu (Ilḥad) katika Qur’ani tukufu, na katika Sunnah ya Mtume Mtukufu, inazunguka maana ya kuugeukia uadilifu, na hutumiwa kwa mgeuko kwa jumla, Waislamu walihusisha maana moja kwa lile neno, nayo: mtu aliyeharibika kidini, kama vile Dahriya, na wengineo, kwa hivyo Al-Razi anasema: "Na miongoni mwao mkanamungu, kwa sababu alielekeza madhehebu yake mbali na dini zote, hakuielekeza kutoka dini moja kwenda dini nyingine", na Al-Zamakhshari karibu akafafanua maana ya lile neno kwa maana hiyo hiyo na maneno yale yale kwa kusema: “Mtu fulani ameugeuka uadilifu katika msemo wake, na ameugeuka uadilifu katika dini yake, kwa sababu

aligeuza madhehebu yake mbali na dini zote, hakuigeuza kutoka dini moja kwenda dini nyingine".

Hii ilielezwa na Ibn Hajar kwa kusema: "Maana ya asili ya neno “Mkanamungu” ni yule aliyeugeukia ukweli, na “Ukanamungu” ni kinyume cha haki. Lakini ikajibiwa kwamba mfanya dhambi dogo ni mgeuka wa haki, akasema jawabu ni: Mfumo wa neno hili unatumika kwa kawaida kwa mtu asiye na dini, basi likitumika kwa matu anayefanya madhambi madogo, maana yake inaashiria ukuu wa dhambi".

Na akasema katika ufafanuzi wa mpotofu (Zindiq): “Zindiq ni neno la Kifarsi, kisha likatumika katika Lugha ya Kiarabu, na kumaanisha “Mtu ambaye anaangalia mambo kwa uangalifu”, na Tha’lab alisema: Hakuna katika Lugha ya Waarabu neno “Zindiq”, lakini walisema: “Mwenye uzindiqi” (mpotofu) ni yule aliye mdanganyifu sana, na ikiwa wanakusudia maana inayotumika na watu wa kawaida wakisema: Mkanamungu

na “Dahriy” humaanisha mtu anayeamini kuwa wakati unaendelea milele.

Hili ni jaribio la Ibn Hajar kuchanganya maoni haya mawili, yaani, neno hili linatumiwa na Waislamu kumwashiria mtu asiye na dini, na hutumika kwa mtenda dhambi kwa kumaanisha ukubwa wa uhalifu bila ya kukusudia maana ya kawaida, na hii inakaribiana na maana ya kiistilahi ya watu wa kisasa.

Kwa kuzingatia hali hii, tunasema kwamba: Baadhi ya wataalamu wa Lugha ya Kiarabu wanasema kwamba ‘Ukanamungu’ kwa maana yake ya kijumla unamaanisha “kila mwelekeo ulio mbali na ukweli”, na baadhi yao huujulisha kwa maana maalumu, ambayo ni “kuondoka kwa dini zote”.

Lakini tafiti za kisasa, zinalihusisha neno la ‘Ukanamungu’ na maana ya kukana uwepo wa Mungu tu, basi husemwa: Ukanamungu katika istilahi ni itikadi ya kukana uwepo wa Mungu.

Saiklopidia ya falsafa ya “Laland” imerekodi

mjadala unaoendelea kuhusu suala la Ukanamungu, ambapo watafiti wengine wanaamini kwamba neno hili haliwezi kufafanuliwa kifalsafa, lakini ni bora libakie katika upeo wa ufafanuzi wa maneno ya kawaida, kwa sababu "hakuna tuhuma iliyokuwa ikienea zaidi kuliko tuhuma ya Ukanamungu. Katika zama za kale, ilitosha kwa mtu kutuhumiwa kwa tuhuma hii na kunyimwa kushiriki katika maoni yaliyopo au imani rasmi katika enzi, hata zikiwa chafu au pungufu kupita kiasi". Neno 'Ukanamungu' kwa wanaotetea mwenendo huu halina madhumuni halisi, lakini lina thamani ya kihistoria iliyoamuliwa pekee katika kila kesi; basi jambo ambalo wanaliona baadhi ya watu ni uthibitisho wa uungu, wengine wanaweza kulihesabu ni Ukanamungu, maana lile neno linalingana na mijadala ya kidini kuliko ukweli wa kifalsafa.

Kweli mwenendo huu ni jaribio la kuutetea mwelekeo wa madhehebu ya uyakinifu (materialism) na ya kikanamungu, kwani unajaribu kuondoa maana ya neno na kuliacha tupu bila

ya maana wala ukweli, na kulifanya kuwa neno linalotumika kuwaashiria wanaokanamungu na wanaomuamini wakati ule ule. Basi Renovier anaona kuwa itikadi ya uungu labda itatoweka chini ya uchambuzi, basi hapo ile itikadi itakayotoweka ni ile inayostahili kuitwa Ukanamungu, na kwa upande huu neno hilo halihusiani na itikadi fulani pasina nyingine.

Hata hivyo, kuna wengine wanaoamini kwamba ufafanuzi wa neno hili hauwezi kufungwa katika ufafanuzi wa kilugha tu, na kufuta maana yake na uhalisia wake wa kifalsafa kwa kudai kuwa iko tofauti katika matumizi yake, kwa sababu tofauti hiyo sio kwenye madhumuni yake ya kifalsafa, lakini iko katika matumizi yake yaliyopotoshwa na kuelekezwa dhidi ya itikadi fulani au mtu fulani. Kwa hivyo, watetezi wa madhehebu hii wamehusisha maana ya neno la 'Ukanamungu' katika maana mbili zifuatazo:

Ya kwanza: Ni maana ya kinadharia; nayo ni Ukanamungu unaotegemea ukanaji wa sababu, au kuzitumia kwa kiasi.

Ya pili: Ni maana ya vitendo; ambayo ni Ukanamungu unaotegemea ukanaji wa thamani ya matendo ya kimungu katika ulimwengu.

Maana ya kwanza inategemea kukana uwepo wa mungu, na kujaribu kurudisha asili ya ulimwengu kwa nadharia zinazopingana na uumbaji, wakati maana ya pili mtetezi wake anajishughulisha sana na kuelekeza tuhuma kwenye tendo la kimungu, uhusiano wake na wema na ubaya, na suala la uadilifu wa kimungu.

Kwa hivyo, walihusisha matumizi ya neno hilo kwenye madhehebu inayokana uwepo wa mungu, sio kwa ile inayokana sifa fulani za mungu, au inayapingana na imani fulani ya kidini, au maoni ya kijamii yaliyostawi. Kwa maana hiyo, wanafalsafa wa uyakinifu (materialist) ni wakanamungu kwa sababu walisema: Vitu vya uyakinifu (mate-

rial beings) vinakuwepo kabisa, na ndio sababu ya harakati, maisha na mawazo. Vilevile ma-dahriya ni wakanamungu, kwa sababu wanadai kwamba ulimwengu hauhitaji mtengenezaji, na kwamba ulimwengu pamoja na yote yaliyomo ndani yake yalitokea kwa bahati.

**Umuhimu wa Ufafanuzi wa Kiistilahi:**

Umuhimu wa kuhusisha matumizi ya Ukanamungu kwa maana ya kiistilahi inayolingana na kukana uwepo wa mungu na kusema kuwa uumbaji wa ulimwengu ulikuwa kwa bahati bila maana nyingine za kilugha, unalenga kuimarisha juhudi ili ziungane katika kuukabili, na kutufanya tusitawanyike juu ya maana za kilugha tulizozitaja hapo juu, haswa baada ya kuenea kwa uzushi huu hivi sasa kuliko nyakati zilizopita, na kufikia jamii za Kiarabu na Kiislamu, na jaribio la kushawishi nayo baadhi ya wajinga katika vikundi tofauti hasa vijana.

**Kutojua na Ukanamungu:**

Kutojua: ni msimamo wa kimaarifa katika asili yake usiohusiana na uwepo wa Mungu, nao ni msimamo wa zamani ambao Wasofisti waliukumbatia, maana waliona kuacha kuamua uwepo wa chochote au kukijua. Na wameendelea kusema kuwa shaka huhusika na vitu vya kihisia, vya ufahamivu, na vya kinadharia, maana haiwezekani kuthibitisha chochote moja kwa moja. Basi ikisemwa: Msisitizo wenu ule unapingana na shaka yenu, wakasema: kutothibitisha hakumaanishi msisitizo bali kunamaanisha shaka. Sisi tunatilia shaka, na tuna shaka kuwa tunatilia shaka. Na kwa kweli huu ni msimamo usiomaanisha kuacha kuthibitisha chochote, bali unamaanisha kukana kwa uwepo wa chochote, kwa sababu shaka yao haizingatii mambo yasiyoonekana wala yale yasiyojulikana kwa akili na hisia, zaidi ya hayo, walitilia shaka vyote visivyoweza kutambuliwa.

Miongoni mwa wanachuoni wa kisasa wanadai kwamba:, kutojua kunamaanisha mambo mbalim-

bali, miongoni mwake ni kukana thamani ya akili na uwezo wake wa kutambua, au kukataa kujua ukweli halisi, kama alivyoona "Huxley", ambaye ni mwanamadhehebu ya kikweli inayoona kuwa madhehebu ya uyakinifu (materialism) na ya kiroho ni kosa, kwa sababu zinadhani kuwa tunajua ukweli wa vitu wakati hatuvijui, na yeye ndiye aliyeupa msimamo wake huu jina la: Kutojua. Madhehebu hii pia inakana kujua kwa yaliyomo metefizikia; yaani: "Kila mwanafalsafa anayekana maarifa, au kukiri uwepo wa kweli wa mambo ambayo hayawezi kujulikana, yeye ni miongoni mwa watetezi wa madhehebu ya "Kutojua".

Kutojua kama msimamo wa utambuzi kunaweza kusababisha Ukanamungu, kwa sababu mtetezi wake anaweza kukana ukweli kwa ujumla, kama ilivyo katika msimamo wa wazee kwa Sofisti, lakini kwa kweli kutojua hakuhusiani na Ukanamungu kwa sababu hakukani uwepo wa ukweli halisi, lakini inakana ufahamu na umbile lake, kwani inakanusha uwezekano wa kujua, kama

alivyosema "Herbert Cpencer":"Tunapozingatia vitu vinavyoisha, tunazingatia vitu vyenyewe na mwisho wake, lakini tunapozingatia vitu visivyoisha, tunakana mwisho, lakini hatukani vitu vyenyewe". Na anasema:" Sheria za fikira zinazotukataza kuunda maoni ya kuwa uwepo halisi upo, pia zinatukataza tusiepuke na kuzingatia maumbile yake".

Kwa hivyo, licha ya kuwa ameikiri nadharia ya mageuzi, alitoa nafasi kwa kukiri dini na kukiri kuwa ina uwanja wake mwenyewe, kama ilivyo sayansi ina uwanja wake mwenyewe na maswala yake ambayo hayatatuki isipokuwa kupitia sayansi. Katika hilo anasema: "Tukikiri hayo, dini lazima iwe na nafasi yake kando ya sayansi, lakini hitilafu baina yake ni kuwa dini mbalimali zinadai kuainisha umbo la ukweli halisi, na sayansi pia inataka kuelekea uwanja ulio ni uwanja wa dini hasa. Kwa mantiki hiyo, mipaka ya maarifa ikiainishwa barabara kati ya dini na sayansi zitaafikiana kuwa kiini cha uewepo hakijulikani wala hakihisiki, na

hivyo, kila moja kati yake itajifunga katika upeo wake, na mgongano baina yake utamalizika".

Kwa hivyo, yeyote miongoni mwa watetezi wa madhehebu hizi anayeweza kutofautisha kati ya uwepo na maarifa, kutojua kwake hakutakuwa kisawe na Ukanamungu, lakini asiyeweza kafanya hivyo, kutojua kwake kutakuwa kisawe cha Ukanamungu.

## Historia Fupi ya Ukanamungu

Kadhia ya Ukanamungu imeibua maswali mengi, kati yao ni: Je! Kuna uhusiano kati ya Ukanamungu na maendeleo ya wakati huu ya kiufundi, uwazi wa elimu na maendeleo ya kiteknolojia? Kwa maneno mengine, je! Ukanamungu ni moja ya uzushi wa zama za kisasa, na sifa zake za mawasiliano ya kimataifa ambazo hazikuwahi kutanguliwa kabla, mpaka ulimwengu umekuwa kama kijiji kidogo, na imekuwa rahisi kuhamisha maoni na mafundisho ambayo hutangatanga kati ya nchi za ulimwengu, na ikawa rahisi kutoka wazo katika nchi fulani, likapata watetezi wake katika nchi mbali mbali na kuwa ni jambo la kuathiri au kuathiriwa? Au ni jambo ambalo mizizi yake inaweza kupatikana katika taya za zamani, na katika vipindi vya nyuma vya kihistoria?

Na ikiwa uzushi wa Ukanamungu ni wa zamani au wa kisasa, ni zama gani ulikuwepo muonekano

wake wa kwanza? Ulikuwa umejulikana kwa jina la Ukanamungu au madhumuni yake ya kifikira yalikuwa yamepewa istilahi nyingine?

Tukijaribu kupata jibu la maswali haya katika fasihi ya watetezi wa Ukanamungu, tutakuta kwamba wanadhihirisha madhehebu yao kama matunda ya enzi za kisasa, uwazi wake wa utambuzi, na maendeleo yake ya kisayansi.

Maana wanajaribu kimoyomoyo, kudai upya wa madhehebu yao kwa kuiunganisha na enzi ya maarifa na maendeleo, kana kwamba dini na udini zinawakilisha umbo tofauti wa zama zilizotangulia maendeleo ya sasa, hivyo walijaribu kuunganisha dini na ushenzi wa kiutamaduni kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine, kuonesha madhehebu yao kama matunda ya ukombozi wa kiakili na kizazi cha ukomavu wa kisayansi ambao umeshuhudiwa na ubinadamu wa hivi karibuni

Wakanamungu wanajitahidi kutoa maelezo yanayofaa kwa uzushi wa dini, na kuonesha kuwa

ilikuwa jambo la lazima ambalo limetakiwa na sababu mbali mbali za jumla zinazotokana na mwanzo wa maisha ya wanadamu na tabia yao. Miongoni mwa waliyoyasema juu ya dini ni: "Kitu kisicho na ukweli, na ni dhihirisho la tabia ya wanadamu wanaotafuta ukweli wa ulimwengu, ambayo inajaribu kuuelezea. Hakika tabia hii ya kibinadamu yenyewe ni jambo zuri, lakini hmaarifa na mbinu adimu zimewaelekeza mababu zetu kwa majibu yasiyo sahihi, ambayo sasa yamo katika maoni yao juu ya mungu na dini. Lakini leo, baada ya kupata mbinu za kisayansi, na maarifa ya kisasa imejaa katika itikadi zetu za kijamii na kiutamaduni. Wakati umewadia wa kufikiria upya mawazo yote ya babu zetu".

Miongoni mwake misemo yao ni: Dini ni matokeo ya ufahamu wa ndani wa binadamu, sio udhihirisho wa ukweli wa nje, na usemi wao: Mungu sio chochote ila ni kielelezo cha utu wa binadamu kwenye skrini ya ulimwengu, na itikadi ya dunia na Akhera siyo ila picha kamili ya matamanio ya

wanadamu, na Wahyi na ufunuo siyo ila onyesho lisilo la kawaida la hadithi za watoto zalizofichika ndani yao.

Julian Huxley anasema: Dini ni matokeo ya uhusiano maalumu kati ya mtu na mazingira yake, pia anasema: Imani ya kimungu imefika hadi mwisho wa faida yake kwetu, na haiwezi kukubali maendeleo yoyote sasa, maana mwanadamu alivumbua nguvu ya metafizikia ili ibebe mzigo wa ulimwengu. Akavumbua uchawi, kisha michakato ya kiroho, kisha imani ya kiungu, baadaye aligundua wazo la "Mungu mmoja", na kwa maendeleo haya, dini limefikia mwisho wa maisha yake. Na bila shaka imani hizi wakati mmoja zilikuwa sehemu nzuri ya maendeleo yetu, lakini sehemu hizi zimekosa umuhimu wake, na faida yake kwa jamii ya kisasa iliyoendelea.

Auguste Comte anasema "Dini inachukuliwa kuwa hali ya zamani inayopaswa kuisha ili ubinadamu ufikie hatua ambapo sayansi inachukua ma-

hali pa dini na fikira za kimetafizikia, na kuunga haya yote kwa sayansi kwa jumla ambazo baadhi yake zinafanya kazi uwanjani mwa ulimwengu wa kitabia, na nyingine uwanjani mwa maisha ya binadamu, hivyo, dini haitakuwa na chochote kilichobaki katika uwanja wa tafsiri wala katika uwanja wa mwongozo, na baadaye haitakuwa na faida, wala hatutaihitaji tena ... ".

Kwa jumla, watetezi wa madhehebu ya Ukanamungu huona dini kama kipengele tofauti cha ukuaji wa akili na ufahamu wa kihemko kabla ya zama ya ukomavu wa kisasa, kwani mwanadamu katika zama zake za mapema amepitia hatua za maendeleo, na alipata misiba na migogoro ambayo hakuweza kupata maelezo ya kushawishi, vilevile, hakuweza kuikabili wala kugongana nayo, jambo lililomfanya azindue wazo la dini, na itikadi ya Mungu mwenye nguvu na utawala, kwa sababu moja kati ya zifuatazo:

1- Kutafuta majibu ya kuridhisha na yenye kushawishi juu ya siri ya uwepo wake katika

ulimwengu huu, mwisho wake, na uhusiano wake na ulimwengu uliomzunguka.

2- Kwa kuchochewa na hofu, alitafuta nguvu kubwa iwezayo kumpa usalama na matumaini katika mapambano yake na misiba ya tabia na siri zake zalizofichika. Basi, akavumbua wazo la Mungu mwenye nguvu anayemuwezesha kukabiliana na hofu, na anayempa amani na salama inayotakiwa.

3- Kutafuta Pepo iliyopotea, ambapo mtu hupata ukombozi wa shida ya hali halisi aliyoishi, na shida ya maisha yake ambayo alipatwa nayo. Kwa sababu angepoteza furaha na neema katika siku yake hii, angepata neema ambazo alitamani kuzipata kesho katika ulimwengu tofauti.

(Wakanamungu wanarejesha ukuaji wa uzushi wa dini miongoni mwa jamii kwa mambo ya mazingira, kisiasa, kiuchumi), kijamii, na hata kisaikolojia pia. Sababu zote hizi zilisaidia kuenea

kwa dini kama uzushi uiliojulikana katika mataifa na maendeleo zamani.

Basi Dini, kwa mtazamo wao ni uzushi uliotakiwa kwa mujibu wa haja za mwanadamu katika zama za mapema, na mwanadamu amekuwa hana haja nao baada ya kuweza, kwa kuzingatia maendeleo ya kisayansi ya kisasa, kugundua siri za ulimwengu, na akaweza kukabiliana na shida zake, na labda akazitawala kwa ile silaha ya sayansi aliyo nayo.

Na bila kujali majadiliano ya maoni haya, au uchambuzi wa madhumuni yake ya kiakili na kisaikolojia inayoonesha hali ya utupu wa kisaikolojia, usumbufu wa kihemko, ujinga wa kweli, na kiburi kibaya, matokeo ya sayansi ya kisasa kwa kweli ni ushahidi wa uwepo wa Muumbaji mwenye busara, au bahati inawezaje kutuelezea uamuzi huu, na mfumo huu, na hata ikiweza kuieleza, inaelezeaje kupona kwake na mwendelezo wake? Je! Ni bahati, au utunzaji na hekima

ya Muumbaji mkubwa zaidi, aliyeumba, na aliye mbunifu na mwenye busara zaidi, na aliye muweza kushinda wote?!

Katika masomo ya elimu ya "historia ya dini," wanathiolojia kwa jumla, na wasomi wa historia ya dini hasusana, walipendezwa kutafuta kuibuka kwa "dini" kama uzushi wa kibinadamu uilioshirikishwa na mataifa yote, na uinaojulikana na watu wote, bila kujali kiwango chao cha kielimu, kiutamaduni, na kiustaarabu. Historia imerikodi kwetu, tangu ukurasa wake wa kwanza, sifa za mawazo ya kidini kati ya mataifa na makabila ya kale zaidi juu ya utofauti wa maeneo ya kijiografia, na utofauti wa kiwango cha kielimu na kiutamaduni "makabila yasiyostaarabika mataifa yaliyostaarabika".

Ikumbukwe kwanza kuwa "dini" kama uzushi uliokataliwa na wakanamungu, na wasomi wa dini wameufanyia utafiti kuhusu chimbuko lake ni wazo la kidini kwa jumla. Basi, hawa hawakuweza

kutofautisha kati ya zile zilizobuniwa na mataifa na watu, na kwa hivyo inawekwa chini ya jina la dini za kibinadamu, na kile kinachohusisshwa na ufunuo wa kimungu, chini ya jina la dini za mbinguni.

Kwa kuchunguza maoni ya wataalamu wa dini, tunaona kwamba walitoa nadharia tatu ambazo ni nadharia zinazoeleza asili ya dini, zile nadharia ambazo zilijengwa kwa mujibu wa mitindo ya kielimu, na mada yake ilyochunguzwa ilichukuliwa kutoka kwa uistaarabu wa umma za kale kabisa, na ilichunguza itikadi zake za kidini ambazo hazikujua utamaduni wa kisasaa, ikawa mabali na maendeleo yoyote ya kiustaarabu, zikajaribu kuhifadhi vyombo vyao wenyewe, na urithi wao wa kidini, kiakili na kijamii mbali na mkono wa mabadiliko. Matokeo ya tafiti hizi yalikuwa ni kuwepo kwa nadharia tatu, ambazo ni:  innateness

## Kwanza: Nadharia ya Maendeleo ya Mbele au ya Upandisho[1]:

Watetezi wa nadharia hii wanaona kwamba "Dini ilianza katika mfumo wa ushirikina na upagani, na mtu alianza kuongezeka katika dini kizazi na kizazi hadi akafikia ukamilifu kwa Umoja, na aliendelea hatua kwa hatua kwendea ukamilifu katika sayansi na tasnia yake, hadi baadhi yao wakadai kwamba itikadi ya" Mungu mmoja "ni imani ya kisasa sana.

Nadharia hii iliungwa mkono na watetezi wa madhehebu ya mbele au ya upandisho iliyoenea Ulaya katika karne ya kumi na tisa katika tawi zaidi ya moja la sayansi, na wasomi kadhaa walijaribu kuihusisha na historia ya dini, miongoni mwao: "Spencer", na " Tylor, Frazer, Durkheim, na wengineo"

(1) - The theory of Evolution.

**Pili: Nadharia ya Usilika wa Umoja na Uhalisi wake:**

Kundi jingine lilikumbatia nadharia hii, pale walipoamua kwa njia za kisayansi "kwamba itikadi ya Muumba mkubwa ndiyo dini ya zamani kabisa iliyoibuka na wanadamu, walitoa dalili ya kuwa hakuna taifa kutoka kwa mataifa walioiacha itikadi hiyo tangu zama za kale mpaka za leo, kwa hivyo upagani si chochote ila ni dalili za dharura, au magonjwa ya vimelea kulingana na itikadi hiyo ya kimataifa na ya kimelele. Nadharia hii ilishinda hadhira ya wanasayansi wa kijinsia, wanathiolojia, na wanasaikolojia. Kati ya wanaojulikana zaidi ni Lang aliyethibitisha uwepo wa itikadi ya "Mungu mkuu" kati ya makabila ya washenzi huko Australia, Afrika, na Amerika, pamoja na Seheroeder aliyeuthibitisha uwepo wake katika jamii za kale za Aryan, na Brockelman ambaye aliipata kati ya Wasemiti kabla ya Uislam, na LaRoY, Quatrefages na Wambilikimo wa Afrika ya Kati, na Schmidt kwenye wambilikimo na wenyeji wa Australia

Kusini Mashariki. Utafiti wa Schmidt ulihitimisha kuwa wazo la Mmungu mkubwa" hupatikana miongoni mwa watu wote ambao ni kati ya jamii zote za wanadamu wa kale kabisa".

**Tatu: Nadharia ya Kutokea Wakati Mmoja:**

Na maana yake ni "kuwa uwongofu na upotofu katika wazo la kidini si mizushi mifululizo mmoja baada ya mwingine, lakini ni wa wakati mmoja, ulizosambazwa katika kila taifa na kizazi, kulingana na tofauti ya watu kwa daraja ya unyoofu wa uvumbuzi wa kiakili na heshima ya hisia ya akili ya ndani, kwani hakuna kizazi kisicho na roho safi inayotambua ukweli uliosafishwa kutoka kwa makosa ya ushirikina, na nyingine bila hiyo ... ".

Mbali na kujadili nadharia hizi, kwa kuzitetea au kuzipinga - hii sio maana ya muktadha wa hadithi hiyo - wala kwa kusudi hilo ulikuwa uwasilishaji wake, lakini tunayoyajali ni yale maelezo yanayotolewa kutoka nadhariya hizo kwa jumla, na yafuatayo yanaeleza jambo hili:

1- Kulingana na nadharia ya kwanza - Nadhariya ya Maendeleo ya Mbele au ya Upandisho – itikadi ya 'Mungu muumba mmoja' huwakilisha kilele cha piramidi katika tafsiri yake ya hatua za maendeleo yake ya kiitikadi, kwani ni nini baada ya ukamilifu ila kinyume chake?

2- Tukiangalia nadharia ya pili inayopambanua chanzo cha "dini" - ambayo inapingana na nadharia ya kwanza - tunakuta kwamba kuenea kwa fikra ya Mungu muumbaji mkuu kati ya jamii na makabila mbalimbali, na hata mataifa yaliyostaarabika, ni ushahidi kwamba hazikuwa hadithi safi zilizozuliwa na mwanadamu, kwa sababu madai kwamba mataifa haya na ustaarabu yalikuwa kwenye mawasiliano ambayo yanaruhusu kupeleka maoni kati yao ni jambo lisilo la yakini, na hata ikifafanua uwepo wake, haitafafanua kuenea na mwendelezo wake. Kwa upande mwingine, tungezingatia kwamba mataifa yalitofautiana kimsingi, kwa upande wa kielimu, kiutamadu-

ni, na kiustaarabu, na baadhi yake yakijulikana kwa maendeleo na ufanisi, ambapo mengine yalijulikana kwa ubedui, basi kwa yakini jambo hili linapelekea kujitokeza swali juu ya siri ya makubaliano yao kwa wazo la Mungu Muumbaji, kwa sababu tofauti kati yao katika kiwango cha maendeleo na ustaarabu inatosha kuwa sababu ya kutokukubaliana baina yao na jambo hilo. Kilichokubaliwa na taifa moja sio lazima kikubaliwe na mataifa mengine.

3- Madai ya kwamba dini ni hali ya zamani, na kwamba ukombozi kutoka imani ya kidini kwa jumla ni lazima, na kutoka imani kwamba kuna Muumbaji Mungu si jambo jipya, kwani maoni haya yalitokea na yalitetewa zamani, yaani madhehebu hiyo imeishi wakati mmoja na mahali pamoja na maoni yanayotetea mawazo ya kidini na imani kwamba kuna Muumba, na hiyo ndiyo inafaidika kutoka kwa nadharia ya tatu. Kwa hivyo inaweza kusemwa kwamba madhehebu ya Ukanamungu ina mizizi ya

kihistoria, kama inavyowezekana kusemwa kwamba madai ya Ukanamungu yanawakilisha hatua ya ukomavu wa kiakili na kihemko sio sahihi.

4- Imani ya kuwa Muumba yupo si matokeo ya dini kama silika ya kibinadamu iliyoibuka kwa sababu mbali mbali kama wanavyodai, kwa sababu watu hutofautiana katika jinsi wanavyotimiza matamanio yao, kwa hivyo ikiwa watu fulani huunda hiari yao imani ya kuwapo kwa Muumba, basi kwa nini wengine huenda kwenye mwelekeo ule ule?

Ukweli wa msemo kwamba kumuamini Muumba ni silika ya kibinadamu ambayo Mungu aliwatilia watu, kulingana na msemo wa Mwenyezi Mungu unabainika kama ifuatavyo ambayo maana yake nzuri iliyomo katika hadith isemayo: (Kila mzaliwa huzaliwa kwa silika ya kawaida ...).

Kwa ajili hiyo, kuamini uwepo wa Muumba, (Utukufu uwe kwake), ni silika, hata ikiwa watu

hutofautiana juu ya maana hiyo. Inaambiwa kuwa Al-Shahristani alisema: "Jambo ambalo watu waliafikiana juu yake ni kuwa ulimwengu una nguvu ya kimungu iliyoupanga, lakini ina majina mbali mbali", na tofauti zilizoko katika imani zao kwa Muumba (Utukufu ni kwake) hazikuwa ila kwa tofauti baina yao katika kujiongoza kwa nuru ya ufunuo wa Kimungu, umbali wao kutoka kwa chanzo sahihi, na ukosefu wao wa kuelewa dhamira yake kuu.

Baada ya maelezo haya, huenda ikawa rahisi kwa mtu kujibu swali lifuatalo: Je! Imani juu ya uwepo wa Mungu muumba ni ngano, au kukana kwa uwepo wake ndio ngano na kiini cha kosa?!

Swali linalojitokeza sasa katika muktadha wa utafiti huu ni: Ikiwa imani ya uwepo wa "Mungu" ni silika ya kibinadamu na dini ni silika ya kibinadamu, lini kulitokea kupotoka kwa silika mara ya kwanza ikakana uwepo wa mungu, na katika umbo gani ilionekana?

Kabla ya kujibu swali hili, inapaswa kuzingatia kwanza kwamba sio kila upotofu wa imani huzingatiwa kama Ukanamungu kwa maana ya kiistilahi ambayo utafiti huu umeshughulika nayo, na inayomaanisha "kukataa uwepo wa Mwenyezi Mungu ".

Neno "Ukanamungu" lina maana nyingi, yote yanaelezea upotofu wa kiitikadi na wa kiakili. Watu wakati mwingine "hutumia neno hili kumaanisha kukana uwepo wa Mungu, na wakati mwingine kukana ujuzi wake, utunzaji wake, uwezo wake, mapenzi yake, na inatosha kwa mtu kukana msingi mmoja wa misingi ya dini, au itikadi moja ya itikadi zinazojulikana, au moja ya maoni maarufu ili atuhumiwe kwa Ukanamungu....". Hii inachukuliwa kama Ukanamungu kwa maana yake ya jumla na maana yake ya kilugha, ambayo inamaanisha kuachana na Imani, mazoea na maoni maarufu ya kidini, ikiwa ni yenye asili ya kimungu au ya kibinadamu.

Na kwa kuwa utafiti huu unahusika na kuchunguza Ukanamungu kama uzushi unaochochewa hivi karibuni, na ambayo madhumuni yake ya kiakili yanaonesha uharibifu wa itikadi ya uungu kwa kukana uwepo wa Muumbaji, (Utukufu ni wake), utafiti huu utajifunga kufuata mwenendo wa wazo hili kihistoria, na ili tufanye jambo hili liwe rahisi, tunaweza kutofautisha kati ya vipindi vitatu vikuu ambavyo Ukanamungu ulivipitia kama uzushi:

Cha kwanza: Kipindi cha muonekano wa kwanza, "vyanzo vya mawazo ya Ukanamungu".

**Cha pili:** Kipindi cha kati.

**Cha tatu:** Kipindi cha kuonekana kisasa.

Yafuatayo hapo chini ni maelezo mafupi ya kila kipindi peke yake.

**Kwanza: Kipindi cha Muonekano wa Kwanza:**

Kipindi hiki kinahusika na kuainisha mkoa wa kwanza wa kijiografia, mazingira ya kiakili, na

zama zilizokumbatia mbegu za wazo la Ukanamungu. Maoni matatu yalisemwa juu ya kipindi hiki:

1- Maoni yanayorudisha chanzo cha wazo la Ukanamungu kwa falsafa ya Uigiriki, haswa katika karne ya nne na ya tatu KK (Kabla ya Kristo), wakati wazo la Ukanamungu lilipounganika na mawazo ya uyakinifu (materialism) katika tafsiri yao ya uanzishaji wa ulimwengu na vitu vilivyomo humo, basi, "Wanafalsafa wa uyakinifu (material philosophers) ni wakanamungu kwa sababu walisema: Vitu vina uwepo halisi, na ndivyo sababu ya taharuki na maisha na mawazo...", na inasemekana kwamba marejeleo ya kwanza ya wazo hili yanapatikana kwenye "Demokratisi"; mmoja wa wanafalsafa wa kale wa Ugiriki, na baada yake "Epicurus" aliyakumbatia.

Wenye hekima wa Ugiriki waligawanyika katika makundi mawili: "Kundi moja lilikubali uwepo

wa dhati iliyo bila ya mwili wala muda, inayotofuatiana na vitu vya kihisia katika sifa zake, bila ya viungo vya mwili na alama zake, na lilithibitisha kwamba mfululizo wa viumbe ukiwa wa kimwili au wa kidhahania unaishi na dhati moja ya kidhahania isiyoundwa wala kurekebishwa, na ni muhali kwa akili  kuzingatia uwepo wa marekebisho ndani yake; uwepo wake ni ukweli wake hasa, na ukweli wake ni uwepo wake, na ndio chanzo cha kwanza, na Mvumbuzi wa kweli, na Muumbaji wa viumbe vyote, vikiwa vya dhahania au vya kimwili. Na kikundi hiki kilijulikana kwa jina la "Wenyenyekevu wa Mungu", na miongoni mwao ni Pythagoras, Socarates, Plato, Aristotle, na wafuasi wa madhehebu yao ni wengi.

Kundi la pili lilikana uwepo wa chochote ila mwili na vitu tu, na kwamba kutoa sifa ya yaliyopo kumehusika na kile kinachotambuliwa na hisia tano na hakushughuliki na chochote nyuma yake. Wafuasi wa Kundi hili walijulikana kwa jina la “waumini wa miili”, na walipoulizwa juu ya asili

ya tofauti baina ya aina za miili na sifa zake, na tofauti iliyoko katika athari zake, wale wazee wao walizihusisha na maumbile yake…. Ndio maana kundi hili lilijulikana miongoni mwa Waarabu kwa "waumini wa tabia". Na mkuu wa wale wanaosema hivyo ni "Demokratisi".

Dk. Abdel Halim Mahmoud anaunga mkono maoni haya; kwa kusema: Ukanamungu ulianzishwa na ustaarabu wa Uigiriki wa zamani kugeukia silika na dini. Na iliibuka kando ya ushirikina na kando ya Umoja wa Mungu

Maana inayokusudiwa ya 'Umoja wa Mungu' katika matini iliyotangulia ni umoja kwa maana iliyokumbatiwa na baadhi ya wanafalsafa wakati ule. Nayo ni matokeo ya kutafakari kiakili wala sio matokeo ya ufunuo wa kimungu.

Dk. Abdel-Halim Mahmoud anaonesha kuwa tunaweza kugundua mbegu za kwanza za Ukanamungu kati ya wasofisti, Epicurus, na Stoiki.

Watetezi wa maoni haya wanategemea maandishi ya falsafa ya Uigiriki na historia ya kale ya Uigiriki, kwa hiyo ni mazingatio ya kielimu yanayotegemea hati na matini za kifalsafa na za kihistoria zinazoaminika.

Licha ya hii, ni muhimu sana kuzingatia maoni haya kama nadharia ambazo zina mstari wa mbele katika historia ya wazo la uyakinifu (materialism) na la Ukanamungu. Lakini kusisitiza kwamba "ubinadamu haukupotoka kutoka kwa Umoja kwenda Ukanamungu, na Ukanamungu haukujulikana kabla ya ustaarabu wa Uigiriki wa kale", ni jambo linalonahitaji kuchunguzwa zaidi na kuitafuta mizizi yake.

Wakati tukizingatia upanuzi wa mstari wa historia kabla ya ustaarabu wa Uigiriki kwenye vipindi vya kikale sana vya historia, na pia tukiangalia upanuzi wa uwepo wa mwanadamu katika mazingira ya kijamii yaliyokuweko wakati wa ustaarabu wa Ugiriki, tungedhani kuwa Ukanamungu uli-

kumbatiwa katika mahali fulani kabla ya Ugiriki, au labda katika jengo la kifalsafa lililotangulia kwa zamani katika ukuaji na uzushi wa mawazo ya Ukanamungu.

2- Maoni yanayoona kuwa mwanzo wa madhehebu ya Ukanamungu hurejelea dini ya Wajaini (Jainism) na ya Wabudhi; dini za India za zamani, ambazo zilianzishwa kabla ya (KK), na inasemekana kwamba uzushi wao ulianza karne ya sita KK, kama majibu ya nguvu ya Wabrahmins, na mpango wa tabaka waliouzua na ambao Wahindi waliteseka nao.

Inasemekana kwamba sababu iliyomsukuma Mahavira kukana Muumba - wakati ambapo madhehebu ya Ujaini yalihusishwa naye - ni kwamba dini yake "ilikuwa sura ya kupinga Uhindu na mapinduzi dhidi ya mamlaka ya Wabrahmins. Kwa hivyo Mahavira hakukubali kukiri miungu, kwa kuwa kukiri miungu inaweza kuleta upya Wabrahmins au watawa watakuwa kiungo baina

a watu na miungu, na akaamua kwamba hakuna roho mkubwa zaidi au muumba mkubwa wa ulimwengu huu, kwa hivyo dini hii inaitwa dini ya Ukanamungu".

Ama kwa Buddha, falsafa yake ilikuwa pia dhidi ya Uhindu na maovu ya kitabaka yake, hata hivyo, haikuonekana dhahiri katika mawazo yake kuwa alikanusha Muumba, kwa sababu alijali hali ya vitendo na maadili katika wito wake, na ndipo mabishano yaliibuka juu ya msimamo wa Buddha juu ya "wazo la Mungu", je, ni yeye kati ya wale wanaokana uwepo wa Mungu, na hapo madhehebu yake itakuwa ya mawazo ya Ukanamungu, au alithibitisha uwepo wa Mungu!

Mmoja wa watafiti anapendekeza kwamba Buddha "wakati mwengine alikwenda upande wa kukana zaidi ya upande wa kuthibitisha, maana aliwadharau katika moja ya mahubiri yake wale wanaosema kwamba kuna mungu akasema: Wazee ambao wanazungumza juu ya Mungu pindi

hawakumwona uso kwa uso ni kama mpenzi anayejisumbua sana hali ya kuwa yeye hajui mpendwa wake ni nani, au kama yule anayejenga ngazi pindi hajui ikulu iko wapi ... ".

Vile vile, hali inayopendekeza zaidi kuwa amekana wazo la uungu ni misemo iliyonasibishwa kwake kama vile: "Desturi ya tabia hainyenyekeii Nguvu kuu inayomtawala kama itakavyo, bali desturi hii ni huru kabisa, yenye utawala wake, na haiathiriki kamwe na athari za kibanadamu wala kimungu ".

Inaonekana kuwa kusema kwamba wazo la Ukanamungu lilianza katika Jainism na Budhism – dini za kikale za India zilizoanza kihistoria katika karne ya sita (KK)- kunapingana na wazo la kwanza lililothibitisha kuwa vyanzo vya fikira ya Ukanamungu vilianza Uigiriki.

3- Wazo linalosema kuwa vyanzo vya fikira ya Ukanamungu vinarejelewa kutoka madhehebu ya Dahriya, nayo miongoni mwa madhehebu ya Uajemi zamani.

Basi, inasemwa kwamba Dahiya ni asili ya madhehebu ya uyakinifu (materialism) na ya kikanamungu yaliyojulikana kwa wanadamu. Nayo ndiyo madhehebu ya wote walioamini ukale wa wakati, miili, na ulimwengu, na kukana uungu, viumbe, uangalifu, ufufuo, na hesabu …., lakini wlinasibisha uumbaji, na upangaji wa ulimwengu kwa nyota.

Wazo hili linategemea aliyoyasema Mustashriki "Frank de Boer" kuwa chanzo cha Dahriya kina asili za kifarsi, na kuwa neno Dahriya "Zrwanismus" ni neno la kifarsi, lililonasibishwa kwa "Zruwan" au "Zruvan" na linalomaanisha wakati wa milele (usio na mwisho).

Madhehebu ya Dahriya yamekuwa, kama ilivyosemekana katika misemo ya zamani, ni dini iliyoenea na inayowaita watu kuikumbatia wakati wa Yezdgird wa Pili wa Dola la Kisasani (438 – 457 AC).

Watetezi wa madhehebu ya Dahriya wamepewa majina mengine yanayofafanua madhumuni

ya fikira yao, kama vile: Wayakinifu (materialists), wahisia, wakanao Muumba, na watetezi wa Uzalishaji upya wa roho (reincarnation).

Qur'ani tukufu imetaja madhehebu ya Dahriya katika kauli ya Mwenyezi Mungu:﴿Na walisema: Hapana ila maisha yetu haya ya dunia; tunakufa na tunaishi, na hakuna kinachotuangamiza ila dahari, na wao hawana elimu yoyote ya hayo. Hakika wao wanadhani tu (45:24), na miongoni mwa maoni yaliyotajwa kufasiri Aya hii ni aliyoyataja Al-Zamakhshariy kuwa "Wadahriya walidai kuwa kupita kwa wakati ndiko sababu ya hilaki ya watu, na wanakana Malaika wa kifo anayefisha watu kwa amri ya Mwenyezi Mungu, na walikuwa wanarejelea kila ajali kwa wakati". Imam Shihristani aliweka Udahriya wa Waarabu miongoni mwa Waarabu waliokuwa Uarabuni kabla ya majilio ya Uislamu, na waliotetea fikira ya kukana majina na sifa za Mwenyezi Mungu.

Wanathiolojia Waislamu walikuwa na hamu kubwa ya kujadiliana kifikira na wafuasi wa Dah-

riya walipoona kuwa wanakana uungu na kusema kuwa ulimwengu hauna mwanzo. Kwa hivyo, Kadhi Abdul-Jabbar anasema "Tumetoa dalili inayobatilisha kuwa miili haina mwanzo, na tumethibitisha kuwa lazima awepo Muumba mpangaji asiye na mwanzo, pia tumetoa dalili ya kuwa mwili hauwezi kuumba mwili, na hiyo inabatilisha madai ya wanaotetea Dahriya na wanaokana majina na sifa za Mwenyezi Mungu….".

Haya ni maoni yaliyo muhimu zaidi katika historia ya mawazo ya Ukanamungu katika vipindi vyake vya mwanzo, na inaangaliwa kuwa maoni haya kwa jumla yalihitaifiana katika kuainisha vyanzo vyake vya kwanza kabisa, na yalihitalifiana pia katika kuainisha eneo lake la kijiografia, na jambo hili limepelekea kujitokeza swali kuhusu ni ipi iliyo ya kwanza kujitokeza; ni falsafa ya Ugiriki, dini za kihindi, au madhehebu za kifarsi?

Kutegemea historia zilizoko kwenye kila wazo, dini za kihindi ni za kwanza kihistoria, baada yake inakuja falsafa ya Ugiriki, kisha madhehebu za kifarsi.

Hapa tunakutana na wazo la kuathiri na kuathiriwa, maana tukiwa na yakini ya kuwa mahali fulani ni pa kwanza kihistoria na kijiografia pa kukumbatia Ukanamungu, tungeweza kusema kuwa mahali hapo paliathiri pengine, na hivyo kuathiri na kuathirika kulipatikana, na je! Kwa mujibu wa haya madhehebu ya Ukanamungu yalihamia mazingira mbalimbali?

Hakika, si lazima kuweko ile iliyoathiri na ile iliyoathirika, kwani labda fikira hizi zilianza pekee katika mahali mbalimbali bila ya kukutana,wakati ambapo hayakuwa mawasiliano yanayosaidia kuathiri na kuathirika baina ya madhehebu zile. Kwa hivyo, kinachofafanua wingi wa mazingira ya kijiografia na tofauti za fikira ni upungufu wa mantiki ya kiakili, na uadimu wa fikira inapojaribu akili kupita mipaka yake ya kufahamu shughuli za kimetafizikia, hasa ikiwa imetengwa mbali na nuru ya ufunuo na uwongozo wake.

Ukijaribu kuweka sifa hasa zinazotambulisha kipindi hiki cha Ukanamungu na vipindi vilivyokuja baadaye, zingekuwa kama ifuatavyo:

1- Vyote vilianzishwa kwa fikira za kiakili zilizokua mbali na ufunuo wa kimungu, na zilizohimizwa kwa sababu mbalimbali, kama vile, taharuki inayopinga dini za kishirikina (pagan religions), au mifumo mibaya ya kijamii iliyotokea kwa itikadi batili, au ni matokeo ya mazingatio ya kifalsafa ya uyakinifu (materialist philosophy) yaliyojaribu kutambua uanzishaji wa ulimwengu na viumbe kwa njia ya utambuzi wa hisia tu, bila ya kupitia kwenye mambo yasiyotambuliwa kwa hisia na kwa kuyaangalia.

2- Vyote viliishi katika mazingira yake mbalimbali – India, Ugiriki, au Uajemi – kando ya dini mbalimblai zisizo za kimungu, vikawa kama batili inayosukumana na batili, na siyo batili inayosukumana na dini ya kimungu.

3- Havikugombana na itikadi za wakati wake ila kwa njia ya majadiliano na hoja za kiakilil. Hali hii iliendelea kwa mujibu wa ladha ya kihemko na makubaliano ya kiakili tu. Hali hii ni tofauti na Ukanamungu wa kisasa uliojikinga na silaha ya elimu kuipinga dini.

4- Havikuwa na tabia ya kijamii pasipo kuhusu urithi wa kifalsafa ya vitendo na maadili.

5- Vyote vilielekea katika falsafa yake ya kimaadili kukidhi matamanio na matashi yake, kwa hivyo, ilikuwa ya uyakinifu(material) katika tabia yake ya kimetafizikia na ya kimaadili, isipokuwa "Ubudha wa India" uliokuwa ni wenye tabia ya kimaadili halisi. Labda sababu ya hali hiyo ni kuwa – ingawa umeanzishwa kupinga dini ya Uhindu – umeshikilia maadili yake ya vitendo yanayohimiza unyenyekevu na ustadi. Kwa hiyo ulifahamika kama taharuki inayoelekea kutengeneza mfumo wa kitabaka ya Kihindu, na kutofuatiana nao katika itikadi yake

ya kidini iliyoumba mfumo huu wa kitabaka, lakini ulihifadhi mafundisho yake ya kimaadili.

Lakini falsafa ya Demokratisi ilikuwa ya kimaadili kamili, na labda sababu ya hiyo yaweza kurejelewa kwa maoni yake aliyoyatumia kueleza uanzishaji wa ulimwengu – na ijapokuwa ni ya uyakinifu (material) mtupu, na inaona kuwa uyakinifu ni sababu ya uwepo wa viumbe vyote; haikiri uwepo wa chochote kisichoweza kupimwa kwa kanuni za uyakinifu kwa upande wa kutambulisha au kuangalia – ni maoni ya kiakili tupu. Yaani maadili yake ya vitendo si lazima kulingana na yale ya uyakinifu (material), kwa sababu madhehebu yao ni ya kifalsaf tu, na hayakuelekea kupinga itikadi ya kidini au mfumo wa kimaadili.

**Pili: Kipindi cha kati:**

Hichi ni kipindi kilichofuata baada ya kipindi cha kwanza kilichoshuhudia itikadi za kubuni na falsafa za uyakinifu (materialism), na kilitangulia ukuaji mkubwa uliotokea hivi sasa; yaani zama

zilizojulikana Ulaya kwa jina la "Karne za kati". Wakati huu ulimwengu wa Kiislamu ulikuwa umesambaa sana katika viwanja vya ustaarabu na maendeleo. Na kipindi hiki labda kilitambuliwa zaidi kwa Ukanamungu ulioenea katika mazingira yaliyojua dini za kimungu, basi Ukanamungu ukawa upinzani kwa itikadi zilizothibitishwa kwa ufunuo sahihi.

Tunaweza kutambulisha katika kipindi hiki baina ya daraja mbili za madhehebu za Ukanamungu; ya kwanza iliibuka katika ulimwengu wa Kiislamu, na ya pili ilikumbatiwa na Ulaya. Utambulishi huu baina ya daraja hizi mbili ulisababishwa na sababu mbili:

1- Ulimwengu wa Kiislamu wakati ule ulishuhudia ukuaji wa ustaarabu na maendeleo ya kimaarifa, kwa hivyo uliendelea mbele zaidi katika ustaarabu, wakati Ulaya ilikuwa inasumbuliwa na kurudi nyuma kiustaarabu na ugumu wa kisayansi. Kwa hiyo kipindi hiki kimeju-

likana na ‘Zama za giza’, jambo linalobainisha tofauti baina ya mazingira haya mawili kiutamaduni na kiustaarabu.

2- Ukanamungu katika mazingira ya Ulaya ulielekea moja kwa moja kukana uungu, kisha kukana dini kwa jumla, wakati katika mazingira ya Kiislamu, Ukanamungu ulielekea kukana unabii, na wakati ule, ulichukua umbo linalolingana na mazingira yake.

Dr. Badawy aliashiria haya akisema: "…. udini unaknushwa kwa kukana Mungu asiye na ukomo katika mtazamo wa mtu wa Ulaya, na dini zinanaknushwa kwa kukana unabii na manabii katika mtazamo wa Waarabu, na anasema: " ….lazima tutambue maana iliyofichika nyuma ya kukana unabii, maana kukana huko lazima kufahamike kama ni kukana uungu wenyewe, kwa sababu unabii ni njia ya pekee inayomjulisha mtu uungu, na ukikataliwa, njia yoyote kwa uungu itakuwa imekataliwa vilevile….".

Tangu wakati ule, falsafa ya uyakinifu ilichukuliwa kuwa ni chanzo cha nadharia za madhehebu ya Ukanamungu, baada ya hayo, uchunguzi katika historia ya falsafa ya uyakinifu (materialism) ukawa uchunguzi katika historia ya Ukanamungu.

Falsafa ya uyakinifu ilidumaa zama za 'Karne za kati', na tunaweza kauona hayo katika msemo wa Prof. Mahmoud Zaqzouq kuwa: "Wapo wanafalsafa wengi wa uyakinifu (materialism) katika zama za kale na zama za kisasa, lakini hatukutani na mfano wao katika zama za kati katika Ulaya, kwa kuwa falsafa wakati huo ilikuwa inatumikia thioolojia, na hapakuwapo nafasi kwa madhehebu za uyakinifu ambazo aghlabu ni madhehebu za Ukanamungu".

Lakini kupotea kwa madhehebu ya Ukanamungu katika Ulaya katika Karne za kati kulikuwa katika uwanja wa kinadharia tu, lakini kwa upande wa vitendo kulikuwa kupo, lakini kumefichika nyuma ya harakati zilizodai utengenezaji.

Na tukijongea kwenye ulimwengu wa Kiisilamu tutagundua kuwa jitihada katika tafsiri - haswa tafsiri ya urithi wa maarifa wa Ugiriki na Waajemi – ya mawazo yanayopinga imani za Kiisilamu, yalihamia utamaduni wa Kiislaamu, ambayo wasomi Waislamu waliyatambua na kuyakanusha na kuyapinga katika muktadha wa kithiolojia na kifalsafa za Kiislamu.

Hatari za baadhi ya maoni haya ni kwamba katika madhumuni yao huharibu itikadi za Kiislam, kama vile msemo wao wa kukana unabii, au ukale wa ulimwengu, au nadharia ya chembe katika tafsiri ya kuibuka kwa ulimwengu, nayo ni maoni ambayo yanaathiri fundisho la uungu na ukweli wa Umoja (wa Mungu).

Historia ya wazo la Ukanamungu katika Ustaarabu wa Kiarabu na Kiislamu ilianza na kuzuka kwa mwito wa wale wanaokataa unabii, ambao katika madhumuni yake ni uharibifu wa fundisho la uungu. Na kati ya hao waliohusishwa na wazo hili: Ibn Al-Rawandi, na Abu-Zakaria Al-Razi.

Wanafalsafa wa Kiislamu walichungua fikira hizo, wakabainisha makosa yake, na walifichua mawazo yanayoharibu itikadi ya uungu yaliyomo ndani yake, ambayo wakati huo huo ni tarehe ya mwanzo wa madhehebu ya Ukanamungu katika ustaarabu wa Kiislamu, maana, kwa kuibuka kwa maoni kama haya, tunaweza kuweka tarehe ya mwanzo wa kuibuka kwa madhehebu ya Ukanamungu katika Ustaarabu wa Kiislamu kwa upande wa kinadharia.

Lakini kwa upande wa vitendo, watafiti wengine wangeweza kuona kuibuka kwa harakati ya kiwatu (Populist movements) kama moja ya alama za kuibuka kwa madhehebu ya Ukanamugu.

Kwa hali yoyote iwayo, Ukanamungu katika viwango vyake viwili vya vitendo au vya nadharia - ijapokuwa ulionekana katika ustaarabu wa Kiisilamu katika kipindi hicho - lakini haukushikiliwa na watu wengi, kwa kuwa kwa kiwango cha falsafa ya nadharia ulikuwa umefungwa sana kwa utafiti

na mabaraza ya kusomeana, lakini kwa kiwango chake cha vitendo haukuenea katika mazingira ya Kiislamu.

Labda maoni muhimu zaidi ambayo tunaweza kurikodi juu ya uzushi wa Ukanamungu katika kipindi hicho ni:

1- Ukanamungu ulianza katika Ulaya kwa sura ya taharuki za utengenezaji zinazopinga kurudi nyuma kifikira, kiustaarabu, na kijamii. Yaani taharuki hizi zilichukua mabaya ya maisha ya Karne za kati sababu kuulingania Ukanamungu, ijapokuwa zilikuwa kwa siri.

2- Ukanamungu ulianza katika mazingira ya Kiarabu na ya Kislamu, lakini kwa mfumo ulio tofauti na mifano yake katka mazingira ya Ulaya, yaani ulikuwa mojawapo ya uzushi wa uwazi wa kifikira, wa kiutamaduni, na wa kiustaarabu uliyoshuhudiwa na ustaarabu wa Kiislamu baada ya upanuzi wa harakati za ufasiri wa fasihi ya umma na ustaarabu uliotangulia

kabla, yaani ulikuwa mojawapo ya dosari za harakati za kuangazia kiutamaduni na kifikira wakati huo.

3- Uanzishaji wa harakati za Ukanamungu katika mazingira ya Kiarabu na ya Kiislamu haukuwa mchakato wa kijamii; hapakuwepo sababu kwa hiyo, lakini ulikuwa umefungwa sana kwa utafiti ndani ya mabaraza ya wataalamu, na maandishi yao yanayouthibitisha au yanayoukanusha, lakini hakuna dalili ya kuwa umeenea kijamii.

4- Uzushi wa Ukanamungu katika mazingira ya Ulaya au ya Kiislamu uliegemea majadiliano ya kiakili na mahojiano ya kifikira tu.

5- Alama iliyo wazi sana iliyotambulisha Ukanamungu wa wakati huo ulikuwa fikira zake zinazopinga itikadi za dini za mbinguni, na zilizoleta maendeleo makubwa katika nyanja za majadiliano na maswala yake, hivyo maswala mapya kama vile unabii na mengineyo

yaliibuka, na yasingeibuka kama Ukanamungu usingeelekea kupinga dini za mbinguni.

6- Fasihi ya fikira ya Ukanamungu katika kipindi hiki inaweza kuzingatiwa, kwa sababu kuna hati na maandishi yaliyokusanya maoni yao ambayo yapo lakini hayakupitiwa.

7- Wazo la Ukanamungu katika hatua zake za mapema - ijapokuwa lilifungamana – wakati mmoja - na falsafa za maadili zinazopinga ubora (udhanifu)? (idealism), kanuni (principles) na maadili katika baadhi ya pande zake, kama ilivyokuwa katika falsafa ya Epicurus, na wakati mwingine lilifuatia ubora (idealism) wa maadili katika falsafa yake ya vitendo, kama ilivyo katika falsafa ya Budha, na Demokratisi - lilianza kujiunganisha kwa karibu na falsafa za maadili za uyakiifu (materialism) zilizokuwa hazina hamu ila kukidhi matamanio na matashi katika kipindi hiki, na uhusiano huu ulikazwa mpaka ukawa sifa iliyo dhahiri sana ya maadili ya Ukanamungu katika enzi ya kisasa.

8- Ukanamungu sio matokeo ya ukombozi wa akili wala maendeleo ya sayansi, kama wengine wanavyodai, maana kuibuka kwa Ukanamungu katika Ulaya na ulimwengu wa Kiislamu katika kipindi hiki cha kati - pamoja na tofauti ya kiutamaduni na kiustaarabu baina ya Ulaya na ulimwengu wa Kiislamu - ni ushahidi bora wa hali hiyo. Wakati huo, hazikuweko sababu za maendeleo huko Ulaya. Bali hali hapo ilikuwa ni kinyume chake, ulikuwa umesumbuliwa na ujinga ambao uliiweka nyuma ya mataifa yote, lakini hali ya ustaarabu wa Kiisilamu na ulimwengu wa Kiisilamu ilikuwa tofauti. Waislamu wakati huo walikuwa na funguo za ustaarabu na taa za Ufunuo, na licha ya hii, fikira za Ukanamungu hazikukubaliwa wala hazikuenea miongoni mwa watu wake, bali zilikuwa zimevizwa kiakili na kijamii, na dini na udini zilibaki kuwa alama ya jamii ya Kiislamu na sifa zake zilizo muhimu zaidi.

***

## Tatu: Kipindi cha muonekano wa kisasa:

Maoni ya wanahistoria yametofautiana kuhusu mwisho wa Karne za kati na mwanzo wa Karne za kisasa. Tukiangalia jumla ya maoni haya, tunaweza kufahamu kutoka kwa matukio ya kihistoria waliyoyataja kuwa matukio haya yalitokea baina ya karne ya kumi na tano hadi kumi na sita KK. Kwa sababu walichukua matukio hayo ya kihistoria kama alama muhimu katika historia ya Ulaya ambayo inaweza kuainisha mwisho wa Karne za kati na mwanzo wa enzi ya kisasa.

Ilikubalika kukiita kipindi hiki 'Renaissance', "na Renaissance ni ... utangulizi kwa enzi ya kisasa, na Renaissance ilifanyika katika enzi hiyo ambayo ilishughulikia pande zote za maisha ya kiroho, ya kiuyakinifu (material)na ya kiakili na ilionekana katika mfumo wa uamsho wa kifasihi, kisanii, kisayansi, na kidini. Hii ni pamoja na athari zake za kisiasa na kijamii ilizokuwa nazo ... ".

Kuibuka kwa udunia (secularism) kwa maana yake ya kiradikali, ambayo inajaribu kutenga dini, ni ishara dhahiri ya udhaifu wa mamlaka ya dini ndani ya roho, maana udunia umehama kutoka kipindi cha kujificha kuelekea kipindi cha kujitangaza.

Udunia (secularism) katika fikira ya Ulaya umepitia hatua mbili:

Hatua ya kwanza: Ni hatua ya udunia wa wastani katika karne ya kumi na saba na kumi na nane, ambayo dini zilizingatiwa kama jambo la kibinafsi na serikali haikuwa na uhusiano wowote nayo.

Hatua ya pili: Ni hatua ya udunia wa kiradikali katika karne ya kumi na tisa, na ilifika kilele cha uradikali wa fikira ya uyakinifu (materialism) wa kihistoria uliyotaka kufuta kila athari ya dini.

Maana yake, iliyotakiwa si kukomesha jukumu la dini litoweke kwa mambo ya maisha, na kuifun-

ga katika mipaka ya mtu binafsi tu, lakini badala yake iliendelea kujaribu kufuta kila athari ya dini, iwe kwa kiwango cha mtu au jamii. Maana yake, udunia hapa kwa maana hii ndio upande mwingine wa Ukanamungu, na kwa hivyo inatupasa kuzingatia hatari za fikira za kidunia na kubainisha ukweli wa taarifa zao, na nini inaweza kusababisha ukiendelea bila ya ubishani wa kiakili.

Udunia wa kiradkali na wa kikanamungu – tukiruhusiwa kuuita hivyo - haukuwa muonekano wa kwanza wa madhehebu ya Ukanamungu katika enzi ya kisasa, lakini kabla yake ilionekana katika maandishi ya Dideror (1713 - 1784), La metri (1709-1751), Hobach (1723-1789), na Auguste Comte (1798). - 1857), na wengineo katika falsafa za kisasa za uyakinifu (materialism) ambazo ni uamsho wa imani ya zamani ya Ukanamungu ya Demokratisi na Epicurus.

Madhehebu ya uyakinifu (materialism) ya enzi ya kisasa - ambayo kwa kweli ni madhehebu ya

uyakinifu (materialism) wa kwanza - yameendelea chini ya taathiri ya falsafa za Descartes, Gassende, na Hobbes ... Unaweza kukuta madhehebu hii ya uyakinifu (materialism) ya kisasa katika falsafa ya enzi ya kuangazia ( Filosophy of the Age of Enlightenment0-) huko Ufaransa, na miongoni mwa wawakilishi wake ni Dideror, La metri na Holbach wliotetea madhehebu ya uyakinifu (materialism), ya kikanamungu, na ya kiradikali.

Dideror alikuwa mhariri mkuu wa Encyclopedia ya Ufaransa, ambayo kitabu chake cha kwanza kilitokea mnamo 1751. Aliandika makala nyingi ndani yake, na Encyclopedia hiyo - ambayo ilikuwa yenye matoleo ya kumi na saba - ilikuwa chanzo cha uzushi wa uzandiki na Ukanamungu.

Maandishi ya Dideror yalikusanya maoni yake, ambayo yalianza kwa kuikumbatia madhehebu ya kitabia inayosema kuwa Mungu yupo, lakini inakana wakati ule ule uangalizi wa Mungu, kisha yaligeukia kukumbatia umoja wa uyakinifu (mate-

rialism) unaodai kuwa vitu ni hai binafsi, na kuwa vitu hai huibuka kutoka kwa seli ambayo imesababishwa na vitu hai.

Lakini Baron Von Holbach, alisema katika kitabu chake kinachoitwa "Mfumo wa Maumbile" - ambayo ni marejeo ya madhehebu ya uyakinifu (materialism) - kwamba hakuna chochote cha Kimungu au cha kiroho isipokuwa chembe za nyenzo "Mada" (material), na hakuna chochote ila ni nyenzo (material), lakini kile cha kiroho hakipo, hakuna ila nyenzo (material) tu na taharuki, na matokeo yote hufanyika kulingana na sheria za tabia, i.e. sheria za mitambo za juu. Sheria hizi pia zinatumika kwa serikali na jamii. Kwa hivyo kile kinachoitwa katika sayansi ya fizika, 'mvuto na msukumo' kinaitwa katika jamii kujipenda, kupenda na kuchukia.

Hivyo, mahusiano kati ya sayansi ya uyakinifu (materialism) na kuibuka kwa Ukanamungu na kutangaza mawazo yake katika zama za kisasa

huongezeka chini ya mwamvuli wa sayansi ya kifizikia na uvumbuzi wa kisayansi wa kisasa.

Karne ya kumi na tisa ilikuja kushuhudia uvumbuzi zaidi wa kisayansi, na nadharia za kifizikia zinazoeleza asili ya ulimwengu na asili ya uhai. Mojawapo ya nadharia muhimu zaidi ambayo iliibuka wakati huo ni "nadharia ya mageuzi ambayo mtaalamu wa biolojia wa Kiingereza Charles Darwin aliivumbua (1809-1882 BK), na mnamo mwaka wa 1859 BK Darwin alifafanua nadharia hii katika kitabu chake "Asili ya Spishi" (The Origin of Species)… " .

Darwin aliacha swali la asili ya mwanadamu bila ya majibu katika kitabu chake "Asili ya Spishi", lakini alilirudia katika kitabu kingine kilichotolewa mnamo 1871 BK, nacho ni kitabu "Mwanzo wa Mtu". Na katika kitabu hiki nadharia ya mageuzi iliongezeka kushughulikia mwanadamu vile vile. Na hivyo, katika Udarwini, mwanadamu alipotea nafasi yake mwenyewe katika ulimwengu wa

uhai. Na ilionekana kuwa Mungu hakumuumba moja kwa moja, bali alitokea kutoka kwa baadhi ya ukoo wa kibaolojia, na hivyo alikuwa aina ya mnyama pamoja na aina nyingine nyingi.

Darwin asingeshikilia mwenendo huu katika kufafanua uanzishwaji wa binadamu - sio uumbaji wake - asingelikana kuwepo kwa Muumbaji na imani yake katika nadharia ya mageuzi na upandisho. Msomaji anaweza kutafuta asili ya nadharia ya Darwin ya "mageuzi" katika nukuu zilizonasibishwa kwa Epicurus.

Inashangaza kwa akili kwamba maoni kama haya yanaendelea kuenea kati ya watetezi wa Ukanamungu, na kuwa wanayakariri na kuyatangaza kama ukweli, ambapo hawawezi kuthibitisha usahihi wake. Basi yalibaki maoni tu ambayo madhehebu yao ya kisayansi na ya kitabia, wanayoitegemea katika kuweka misingi ya madhehebu yao ya Ukanamungu, haikuweza kuthibitisha usahihi wake. Zaidi ya hayo, wasomi

wa kisayansi wamewasilisha ukosoaji wa kisayansi unaobomoa misingi ya hoja yao katika mageuzi.

Na tungeamua kuchunguza hali ya kisasa ya Ukanamungu iliyoshuhudiwa na jamii zetu za Kiarabu na Kiislamu, tungekuta kwamba madai ya kuwa sababu za kuibuka kwa Ukanamungu katika mazingira ya Kiisilamu zinafanana na ile hali ilivyokuwa huko Ulaya, zinarejelewa kwa kutojua ukweli wa Uislamu, au kupuuza ukweli wake, na sio chuki kati ya Uislamu na sayansi na wasomi, wala haikuwa kwa sababu ya dini – ya mbinguni au kubuni - ambayo iliwahimiza watu watafute maarifa na kufaidika nayo kama ulivyofanya Uislamu, je! haitoshi kuwa Qur'ani Tukufu haikuthibitisha viwango vya juu na vyeo vya juu kwa waumini tu, bali kwa wasomi pia? Mwenyezi Mungu amesema: ﴿**Mwenyezi Mungu anawapandisha walioamini kati yenu na waliopewa elimu vyeo vyema** ﴾ (85:11). Dalili juu ya hayo kutoka Qur'ani tukufu na Sunnah, na kutoka matumizi ya mababu wema ni zaidi ya kuhesabiwa.

Katika miongo kadhaa iliyopita, wazo la Ukanamungu lilisitasita kujitokeza na kujificha katika nyanja za mawazo na fasihi, hadi ukatutokea kwa maoni yake, na kuyatangaza, ukipinga jamii waziwazi na kwa kiburi. Mawasiliano ya kiteknolojia ya kisasa yalikuwa na jukumu kubwa katika maenezi ya wazo hili haraka miongoni mwa vijana wengine.

Labda ni wazi katika yaliyotangulia kwamba wazo la Ukanamungu halikuwahi kamwe kuwa tokeo la utamaduni wa zama za kisasa, wala halikuwa lenya mizizi ya kweli katika jamii zetu za Kiarabu na Kiisilamu, lakini ni wazo la zamani ambalo lina mizizi katika historia ya wanadamu, vilevile ni moja ya upungufu wa tamaduni zinazokuja kupitia njia za mitandao ya kijamii.

Inawajibika kutaja kuwa kuibuka kwa saiti (tovuti) za waarabu wasio na dini kulikuwa na mahusiano makubwa na saiti za waarabu wakanamungu, na labda ni hatua ya kutayarishia kutanga-

za Ukanamungu waziwazi katika saiti zake katika mtandao wa habari wa kimataifa "Internet".

Hii inatupasa kuongea juu ya sura za Ukanamungu au majina yake, na sifa zake, kwani Ukanamungu ulionekana zamani na sasa chini ya majina mbalimbali yaliyotofautiana katika istilahi lakini yalikuwa na madhumuni moja, miongoni mwa majina haya yalikuwa: Niturism, Uyakinifu, Dahriya, Kutoamini dini, na Wanatabia.

Sifa zilizo muhumu zaidi za Ukanamungu katika zama hii ya kisasa ni:

1- Uliweka sayansi za kifizikia na mavumbuzi yake mahali pa dini katika tafsiri yake ya uhai, asili ya ulimwengu, na wenye uhai.

2- Haukutosheka na majadiliano ya kiakili, wala ladha ya kihemko tu ili watu kuikubali na kuipokea, lakini ulitegemea - katika kubishana na kugongana na dini, au ulichodai ni ukweli wa dini kutokana na ujinga au kashfa - juu ya baa-

dhi ya kweli fulani za sayansi na mavumbuzi yake na makosa mengi ya kisayansi, na hii ilikuwa ina athari yake dhahiri katika kuueneza haraka na kuutetea.

3- Ulihusika na harakati nyingi za kimapinduzi zilizobadilisha mifumo ya nchi fulani kisiasa, kiuchumi, kiakili na kijamii, kama vile: Ukomunisti na Umarkisisti.

4- Ulihusika sana na falsafa ya maadili ya uyakinifu (materialism) inayopendelea kukidhi matamanio na kutosheleza misisimuko badala ya kufuata sheria yoyote "ya kidini au ya kijamii", hata ikiwa imetokana na hali ya busara ya akili ya mwanadamu, yaani haikujali ila silika ya mwanadamu inayolingana na upande wa uyakinifu (materialism) katika hali yake ya kibinadamu.

Miongoni mwa sifa muhimu zaidi za wazo la Ukanamungu zinazonekena kwa wale wanaotalii saiti za wasio na dini na Waarabu wakanao Mun-

gu, haswa katika ukosoaji wao kwa Uislamu, ni hizi zifuatazyo:

1- Kuchukua sehemu ya matini bila ya kuangalia maana ya jumla ya muktadha ili kutoza hukumu zinazopingana na maana iliyokusudiwa kwa matini.

2- Ujinga wa kilugha, na wakati mwingine nia ya kuficha maana sahihi ya baadhi ya matini, ambayo husababisha mkanganyiko katika kuelewa maana iiyokusudiwa.

3- Kutegemea udanganyifu wa kisayansi na dhana potofu haswa wakati unapozungumzia suala la dini kutoka mtazamo wa kisayansi au suala la sayansi kutoka mtazamo wa dini, kuonesha kuwa uko ubishani kati ya sayansi na dini, na kuonesha kuwa matini ya dini hayawezi kusimama mbele ya ukweli wa sayansi wala hayawezi kuukosoa au kuushinda; kutokana na ujinga wao, na kutaka kwao kuwapoteza watu.

4- Kufuata dhana na maoni yasiyo ya kawaida na dhaifu, na kudai kwamba yanawakilisha dini ya kweli, kisha wanayatilia shaka, wakipuuza msimamo wa kweli wa wasomi waliyokosoa.

5- Kujaribu kuthibitisha ngano ya mzozo unaodaiwa baina ya dini na sayansi, kwa kuwasilisha nadharia za kisayansi kama ukweli, hakika, na nadharia zilizothibitishwa na sayansi kama vile nadharia ya mageuzi na upandisho, ambayo kwa kweli sio chochote ila mawazo ambayo hayajathibitishwa mbele ya ukosoaji ambao umetolewa dhidi yake.

6- Kutafuta baadhi ya matini ya kidini, ambayo maana yao ya kidhahiri inadhaniwa yanapingana na nyingine, na kudai kwamba kuna ubishani unaoashiria ubinadamu wa maandishi, halafu kukana hifadhi ya Wahyi, na utukufu wa matini ya kidini.

7- Anayechunguza fasihi zao anaona ukosefu wao wa maadili ya mjadala na njia za kujadili,

na vilevile njia zao za udanganyifu, wingi wa matusi, kejeli isio na msingi, na njia yao ya kuchanganya maudhui na maswala kwa njia ambayo inasababisha kujishughulisha na mambo madogo madogo, na kupotoka kutoka katika madhumuni ya kweli ya suala linalojadiliwa. Na iliyo muhimu zaidi, ni ujinga wao wa asili ya maswala ambayo wanatoa wakati wa majadiliano.

## Sababu za kuibuka kwa Ukanamungu

Ukanamungu haukushuhudia maenezi wala nguvu kama ilivyotokea katika nyakati za hivi karibuni. WakanaMungu walikuwa vikundi vilivyotawanyika huko na kule, lakini ni vic` hache. Hali hii iliendelea hadi miaka mia tano iliyopita, ambapo cheche ya kwanza ya Ukanamungu iliibuka kutoka moyoni mwa ulimwengu wa Magharibi, na kutoka hapa tunaweza kuanza moja kwa moja kutafuta sababu zilizosababisha kuibuka kwa wazo hili la Ukanamungu.

**Kwanza: Sababu za Kuibuka kwa Ukanamungu Katika Ulimwengu wa Magharibi:**

Inatajwa kuwa kitabu cha kwanza kilichotaja Ukanamungu wazwazi na kilichoulingania kilieneza barani Ulaya mnamo mwaka wa 1770 BK, nacho ni kitabu kinachoitwa "Mfumo wa Maumbile" kilichotungwa na Baron de Holbach, aliye-

sisitiza kuwa ni muhimu kwa wanadamu kuacha yaliyoko nje ya ulimwengu kwendea ulimwengu mwenyewe; anasema: Mwanadamu yuko katika maumbile, na ni mtiifu kwa kanuni zake, wala hawezi kujikomboa nazo.

Ukanamungu huko Ulaya ulikumbatiwa na wanafalsafa na wanahistoria wakuu, kama vile Nietzsche, Voltaire, Karl Marx, Engels, Russell, Comte, na wanafalsafa wengine, wanasosiolojia, na wanahistoria wakuu. Ni jambo lililowasababisha watu kuwaamini wanafalsafa hao, na kugeuzia maoni yao kama majibu ya misimamo ya kiradikali ya kidini, na pia kutokea kwa mzozo kati ya imani potofu na uvumbuzi wa kisayansi.

Tunaweza kugawanya sababu zilizopelekea nchi za Magharibi kuelekea Ukanamungu kama ifuatavyo:

**1- Sababu za Kiutambuzi:**

Sababu za kiutambuzi zilizosababisha Ukanamungu katika nchi za Magharibi zinaweza kufu-

pishwa kwa sababu kuu mbili:

**A- Uvumbuzi wa kisayansi:**

Hadi miaka mia tano iliyopita, chanzo kikuu cha maarifa huko Ulaya kilikuwa ni maoni ya kisayansi ya Aristotle na Ptolemy juu ya ulimwengu, sayari ya ulimwengu, fizikia, kemia, na historia ya asili ambavyo waliviunganisha kwa dhana zao takatifu. Na kwa msingi wa vyanzo hivi, mwanadamu wa karne za kati huko Ulaya aliweza kubuni picha ya ulimwengu.

Tangu mwanzo wa mwamko (Renaissance), maendeleo ya kisayansi na kuibuka kwa uvumbuzi wa kisayansi ambao unapinga kile kilichokazwa akilini mwa jamii ya Ulaya kama ukweli wa kisayansi na dini wakati huo huo, mapingano mazito na makali yakaanza kati ya yale ambayo watu wa zamani walifikiria kwamba yanawakilisha dini, na uvumbuzi mpya ambao unawakilisha ukweli wa kisayansi. Hapa mtaalamu wa hesabu "Cooper Nikos" na hesabati zake, na "Galileo" na darubini

yake, walithibitisha kwamba Dunia sio kitovu cha ulimwengu, bali ni sayari inayozungukia jua. Kwa hivyo madai ya kwamba Dunia imewekwa katikati ya ulimwengu, na kwamba jua, mwezi na sayari zingine zinazunguka katika miduara yake yameanguka. Na, madai haya yalipoanguka, imani nyingi zilianguka kwa sababu ya uvumbuzi wa kisayansi, jambo lililowashawishi watu kuamini kuwa dini inasimama kama kikwazo mbele ya maendeleo ya kisayansi, na hapo akili zilianza kuhoji misingi ya dini tatu, ambayo ni kukiri kwamba:

1) Kuna Mungu aliyeumba ulimwengu.

2) Kuna mpango wa kilimwengu na kusudi la kilimwengu, ambalo linaitwa teleolojia (teleology).

3) Ulimwengu unawakilisha mpango wa maadili uliowekwa na Mungu.

Kwa majilio ya nadharia ya "Darwin" - iliyokuwa ni mojawapo ya nadharia iliyoenea katika

jamii ya kisayansi na ilisababisha mvumo kubwa katika sekta mbali mbali za ulimwengu - wengine walidhani kuwa itachukua mahali pr dini katika kujibu maswali makuu yanayohusu uumbaji wa ulimwengu; mwanzo wake, makusudio ya uwepo wake, na hatima yake, na kwa hivyo ilikubaliwa sana kati ya makundi ya wakanaMungu.

Ijapokuwa nadharia hii ilianguka katika karne ya ishirini, lakini ilibaki kama itikadi ambayo ilishikiliwa na watetezi wa wazo la Ukanamungu, na ilikuwa marejeo ya maoni yao katika kipindi hiki cha kihistoria. Miongoni mwa athari za nadharia ya mageuzi na maoni potofu juu ya kuendeleza wazo la Ukanamungu ni pamoja na:

1) Udanganyifu kwamba wazo la Ukanamungu lina msingi wa kisayansi.

2) Madai ya kuwa yale wayoyaamini waumini juu ya uwepo wa Mungu muumba na Sheria na dini zinazowatawala wafuasi wake sio chochote ila ni matokeo ya maendeleo ya kielimu

ambayo ilitimiza jukumu lake katika kipindi fulani cha maendeleo ya wanadamu, ambayo haifai tena kwa zama hizi.

3) Kushikilia dini hizi ni kurejea nyuma kwenye enzi za ujinga.

4) Kuachana na dini na madili, ili kusababisha kuenea kwa Ukanamungu, ukosefu wa maadili, na kuharibu maadili ya kila aina.

**B- Tuhuma za Kifalsafa:**

Tunaweza kuainisha mzizi wa wazo la Ukanamungu kwa sura yake ya kifalsafa tukirudia zama za Ugiriki, kwani enzi hii ambapo wanadamu walikuwa bado wanatambaa; hakukuwa na uvumbuzi wa hali ya juu wa kisayansi au maarifa makubwa ya vitu vilivyokuwapo. Lakini, wanafalsafa wengine wa Ugiriki waliwasukuma wanadamu kwenye Ukanamungu kwa mapendekezo yasiyothibitika kuhusu metafizikia, ambapo watetezi wa mwelekeo wa falsafa waliwasilisha dalili za kifalsafa zin-

azokana dhana fulani, kama vile kufuta kanuni ya sababu, kukosoa kanuni ya uumbaji, kupendekeza swala la mema na mabaya, kutowezekana kwa ufunuo, na kukosoa vitabu vitakatifu vya dini, kutowezekana kwa maisha baada ya kifo (swala la kuishi milele), au kufuta dhana yake ya kidini kwa kuthibitisha isotopu (version) zake zingine, kama vile kuunganishwa (cloning) au kurudi kwenye uhai. Na aina hii ya majadiliano ya Ukanamungu inayotegemea uthibitisho wa kukana uwepo wa Mungu, na kwa hivyo inaenea zaidi katika uwanja wa vita vya kiakili kati ya imani na Ukanamungu.

Kutokana na hoja hizi za kifalsafa, tunaweza kuzingatia madai ya wale wasemao kuwa sababu za kuacha imani katika asili ya uwepo wa Mungu, ni sababu tatu kuu:

Sababu ya kwanza: Madai ya kuanguka kwa dalili za uwepo, ambazo zinaamini – kikweli au kiuwongo - kuanguka kwa dalili zote zinazothibitisha uwepo wa Mungu, kulingana na misemo

ya baadhi yao – na miongoni mwao ni, "David Hume, Emmanuel Kant na Bertrand Russell" -: kuwa hakuna mtindo wa kiutambuzi unaofaa kuthibitisha suala kama hilo. Wengine walisema kwamba misingi inayoitumia dalili hizi haifai kuthibitishia yaliyomo nje ya mipaka ya uzoefu na hisia, au kwamba tafiti za majaribio katika fizikia kwa kiwango fulani zimethibitisha kuwa hakuna kanuni kamili za ukweli zinazotumika kama dalili za kuthibitisha uwepo wa Mungu.

Sababu ya pili: Tatizo la uovu. Sababu hii inahusika na madai ya kuweka dalili ya kuwa ulimwengu haukutengenezwa na Mungu, na kwa hivyo hakuna Mungu kwa ulimwengu huu, kwa sababu ulimwengu huu ukiwa umeanzishwa na kutengenezwa na Mungu aliyeuumba na kuupanga, usingekuweko humo aina yoyote ya upungufu au uharibifu, kwa sababu Mungu akiwa yupo, angekuwa kamili ambaye hakuna kikomo kwa ukamilifu wake, maarifa yake, uwezo wake, na wema wake. Basi inawezaje kuwa ulimwengu un-

aosifiwa una upungufu, ufisadi, na uovu - ambao ni ulimwengu – ulioumbwa na Mungu mkamilifu ambaye hakuna kikomo kwa ukamilifu wake, maarifa yake, uwezo wake, na wema wake? Na kama matokeo ya udanganyifu huo wa uwongo, wanadai kuwa ulimwengu wetu hauna Mungu, yaani sisi hatuna Mungu.

Sababu ya tatu: Madai ya kutowezekana kufikiria wazo la Mungu. Sababu hii inahusika na madai ya kuthibitisha kuwa wazo lile lile la Mungu haliwezekani, kwa kubainisha kwamba Mungu anayedaiwa uwepo wake lazima asiwe na sifa zile zile za ulimwengu ambao tunaishi ndani yake; kwa sababu sifa hizo hizo zinatumika kuthibitisha kuwa ulimwengu unahitaji Mungu. Hii inamaanisha kuwa Mungu anayedaiwa kuwepo, hawezi kuwa na mwili, kuwepo mahali fulani, kwa wakati fulani, au kuwa na sura. Lakini wazo la Mungu ambaye hana sifa hizi zote sio chochote ila ni neno tupu lisilo na maana yoyote, kwa sababu tukijitahidi kutafuta maana yoyote na kuileta akilini

mwetu, tusingepata ila umbo linaosifiwa na mojawapo ya sifa hizo. Je! tunawezaje kuwaza kitu ambacho sio mwili, sio umbo, hakipo mahali, au wakati? Wazo la Mungu sio wazo, bali ni jina lililopewa kile kilichokosekana sifa zote, na kutokuweko kwa sifa hizi hufuta maana yake.

### B- Sababu za kiustaarabu:

Tatizo la kiustaarabu limetokana na maendeleo ya kiustaarabu ya kisasa ya nchi za Magharibi, kwani iliimarika katika ufahamu wa Magharibi kwamba dini iliyoenea kwao kama walivyoiamini na kuielewa ni kizuizi kwa kila aina ya maendeleo ya kisayansi au ya kiustaarabu. Na – kutokana na ujinga na uwongo – walidai kuwa kuiondoa dini hii na kukana uwepo wa Mungu au nguvu isiyoonekana inayosimamia na kuendesha ulimwengu huu, ndio njia bora ya kuendeleza ustaarabu wa kisasa wa kimagharibi na ku ueneza ili kuwakomboa wanadamu na kutimiza ustawi wao. Hakuna shaka kwamba wazo hili limetokana

na kosa lililoenea katika uwanja wa kukosoa maoni kwa nia au kwa sababu ya ujinga. Kosa lenyewe ni kuchanganya ukamilifu wa kanuni na upungufu wa matumizi yake, na kutuhumu "wazo" kwa mabaya yanayofanywa na watetezi wake.

### C- Sababu za kiuchumi:

Mojawapo ya sababu zilizosaidia kueneza wimbi la Ukanamungu ni kuibuka kwa madhehebu ya kiuchumi yanayoshikilia Ukanamungu, hasa Ukomunisti ulioiwasilishwa na Karl Marx. Ingawa madhehebu hii imetokana na msingi wa kiuchumi na ililenga kushughulikia dhuluma iliyosababishwa na ubepari, na kutawala jamii ya ujamaa, lakini wafuasi wake wameipa pande nyingine zisizo za kiuchumi, hadi wakadai kuwa watu wanapaswa kuishi maisha haya na kunufaika na manufaa yake yote ya kinyenzo, kwani hapatakuwa na ufufuo, hesabu, wala Mungu., Pia walidai kuwa kuibuka kwa dini kulizuliwa na matajiri ili kuwatawala masikini.

### D- Sababu za kijamii:

Inadaiwa kwamba hali mbaya sana za kijamii zilizosumbua Ulaya kutokana na kuenea kwa malalamiko makubwa, kuibuka kwa matabaka tofauti na ubaya ulioachwa, kutofaulu kufikia dhamana ya haki katika jamii, haya yote yalikuwa sababu miongoni mwa sababu za kukuza wazo la Ukanamungu ambalo lilichochea akili kukataa wazo la Mungu anayeshughulikia maslahi ya watu.

### E- Sababu za Kisaikolojia:

Mwanasaikolojia Mmarekani “Paul Fitz” alifanya uchunguzi mpana kuhusu hali ya kisaikolojia ya watu na jamii zinazoshikamana na Ukanamungu na sababu zake, na kuchapisha kitabu kiitwacho "Saikolojia ya Ukanamungu" ambapo amefungua mlango wa kuchunguza sababu za kisaikolojia za Ukanamungu. Katika uchunguzi huu anathibitisha kwamba kizuizi na imani ya uwepo wa Mungu, na kisha kutomuamini na kukubali wazo la Ukanamungu, mara nyingi huambatana

na sababu za kisaikolojia, kibinafsi au za kijamii. Kwa hiivyo, katika kitabu chake, Fitz anasema: Imani yangu ni kwamba kuna mambo mengi ya kisaikolojia na ya kibinafsi nyuma ya kila mkanamungu, na kuna sababu za kisayansi au za kimantiki zinazomsukuma Ukanamungu.

Machafuko ya kisaikolojia yanaweza kusababibisha - kwa sababu ya kutokea kwa shida za kibinafsi au za jumla - uwezekano wa kukubali Ukanamungu au sababu zinazoelekeza moja kwa moja kwao, "au wakati mwingine kwa sababu ya kutojua asili ya uhusiano kati ya Mola na waja, au kutojua maana za shida, na kutojua hekima ya uwepo wa maovu kwenye ulimwengu".

Kwa kweli, jamii ya Magharibi ilipatwa na usumbufu wa kiakili na wa kiutambuzi, mawimbi kasi ya ukosefu wa utulivu, na tuhuma baada ya mapinduzi ya kisayansi yaliyowakumba ambayo pia yaliambatana na mapinduzi mengine makubwa ya kitasnia ambayo yalibadilisha uso

wa maisha ya kiuchumi na ya kijamii, yaliyoanzisha matabaka ya kijamii yaliyowaingiza kwenye machafuko makubwa, yaliyowafanya wakakimbilie kwa kasi kwenye njia za kiustaarabu na wakafanya pupa ya kuvamia vipawa vyake vikubwa, na kujizamisha katika kutafuta sana ladha za kihisia. Hapana shaka kwamba vipawa hivi vilivyouwa vya kiustaarabu, kitamaduni au vya kielimu, ambavyo vilijiweka mbali na mwongozo sahihi wa kidini, viliweza kuunda nia ya kisaikolojia iliyotafuta Ukanamungu kwa nia ya kujikomboa kutokana na vikwazo vya kidini ambavyo walihisi vinawalazimisha kuachana na matamanio yao ila kwa mujibu wa kanuni tu. Zaidi ya hayo, kupotea au kuanguka kwa mfano mzuri kama chanzo cha maadili na desturi husababisha kuanguka kwa ngome ambayo inazuia vijana kuathiriwa kisaikolojia na mvuto wa mambo tuliyoyataja hapo juu, ambayo yalioneshwa na Fitz na nadharia ya “mpotelewa na baba”.

Pili: Sababu za Kutokea kwa Ukanamungu katika Ulimwengu wa Kiarabu:

**(1) Sababu za Kiutambuzi:**

Uamsho wa kisayansi ambao ulianza katika nchi za Magharibi na kuhamia za Mashariki, mawazo ya uyakinifu (materialism) nayo yalihama kama sehemu ya fikira za Magharibi, na kusababisha wimbi la Ukanamungu kwa sababu ya imani za baadhi ya wale walioathiriwa na mawazo haya na wakayatetea, na hii ilionekana katika mawazo ya wengine waliokuwa wanafunzi wa maprofesa wa Magharibi.

Zaidi ya hayo, hamu na sayansi ya kifizikia ya majaribio ilisababisha upanuzi mkubwa katika kujali mitindo ya kimajaribio, na kukataa mitindo mingine ya kiutambuzi, ambayo ilisababisha wengine kukataa kila ukweli ambao haufuati mitindo hiyo.

Pia, mafundisho mengine ya kiakili ambayo yameingia katika ulimwengu wa Kiarabu, kama vile Udhanaishi (existentialism), yamekuwa sababu ya Ukanamungu, kwani ni fundisho linalomtaka kila

mtu kufikia sababu za kuwepo kwake kama anavyoona, na kulingana na kile anachotaka, bila ya kujifunga na mila, desturi, wala dini.

**2-Sababu za Kiustaarabu:**

Baadhi ya Jamii za Kiarabu zimeathirika na sifa za Ustaarabu wa Kimaghribi wa kisasa, kwa kuwa walishangazwa sana na mwendo wake mwepesi ulioelekea upeo wa mwanzo wa starehe za kifikira na uyakinifu (materialism), na kwa hivyo zikashikwa na hamu ya kufuata Magharibi, huku zikitawaliwa na mtazamo kamili wa ustaarabu, kwa hivyo, ikaimarika akilini mwa baadha ya wenyeji wa ulimwengu wa Kiarabu kuwa maendeleo ya kiustaarabu ya Magharibi yalikuwa ni matokao ya utenganisho baina ya dini na sayansi, ukataaji wa dini na kutoiijali, hali iliyowapa dhana kuwa maisha ya Wamagharibi yamefanikiwa, na wakachunga maendeleo ya kitasnia, ya kimaarifa, na ya kiustaarabu yaliyoambatana na Umagharibi.

Zaidi ya hayo, uwazi wa ulimwengu kutokana na mitambo ya hewa kwa pande zake mbili: Vituo vya satellite, mtandao ya kijamii, matamanio na tuhuma zanazotangazwa kwake; kila moja inawatawalia vijana na wavulana; jambo ambalo linawezesha uhamiaji wa mawazo upesi upesi, wakati ambapo hazipo juhudi za kusaidia vijana kukabili athari zake.

**3- Sababu za kisaikolojia:**

Sababu za kisaikolojia na kibinafsi ni nyingi, miongoni mwake ni:

1- Kujithamini kupita kiasi, na kujaribu kwa kila mtu kutosheleza hamu yake kwa kujiona kuwa yeye ndiye bora zaidi, na kwamba akili yake na uhodari wake uko juu ya watu, , na kuwa watu wote ni duni kwake, basi hapo huona Ukanamungu ni kama njia ya kukidhi matamanio yake kutokana na udanganyifu na ujinga, akijaribu kujishawishi kwamba Ukanamungu ni kilele cha ubingwa na uteule; cheo

ambacho hawakifikii ila wenye akili za pekee, ambao yeye ni miongoni mwao, na kuwa wote wanaomzunguka ni wajinga kwa sababu wanaamini nguvu zisizoonekana, na wanajisumbua kwa ibada, na kujinyimia ladha na matamanio. Watu kama hawa wanasifika kwa usaliti, kejeli, sitihizai, kuwadharau wengine, na kujivuna sana.

2- Kujiona huru kupita kiasi hadi kushikwa na kiburi, kukataa kanuni ya amri na kukataliwa, na hamu ya kujitenga na wajibu za kidini na vizuizi vya kijamii, kujisukuma katika matamanio na kutokujali, shida za kisaikolojia, magonjwa ya kiakili, shida za kujitilia wasiwasi kwa yanayozingatiwa sana, na nyingineyo.

3- Kujaribu kuondokana na hali ya kutojiamini, duni (inferiority complex) na hisia za udhalili ambazo huingia ndani ya mtu kama ni matokeo ya kushindwa kisaikolojia, yanayotokana na kulinganisha vibaya baina ya baadhi ya

jamii za Kiarabu na jamii nyingine, hasa katika uwanja wa sayansi ya kisasa. Kwa hivyo, utamuona anaunganisha kila upungufu na baadhi ya Waislamu na Uislamu, na anaunganisha kila mafanikio na maendeleo ya huko Magharibi au Mashariki na Ukanamungu.

4- Uradikali wa aina yoyote ikiwa kidini, kijamii, au nyingineo, kujiadhibu sana, kujizuia, na kufungwa kwa akili mbali na sharia, akili, na silika, kwa hivyo roho inajaa hofu. Na hapo Ukanamungu unakuja kama majibu yaliyojaa hasira. Na yeyote anayepoteza dira ya ufahamu hupelekwa na upepo kwa mwelekeo wowote. Hadithi ya Mtume (SAW) inasema: "Waangamizwe wenye misimamo mikali". (Sahih Muslim: No. 2670)

5- Machafuko ya kisaikolojia yanayotokana na kutoweza kulinganisha baina ya uzowefu wa vyeo vya juu vya kidini na kushughulikia matokeo ya ustaarabu wa uyakinifu (materialism) wa kisasa, na kwa sababu ya kutofahamu daraja za matendo ya Kiislamu yanayohitajika ku-

tendeana na udhaifu wa nafsi ya kibinadamu. Watu wengi wanachagua kuachana na dini kwa kukataa mfumo wote wa dini ili kukidhi matamanio yao bila ya vizuizi au masharti.

**4- Sababu za kijamii:**

1) Tatizo la kutokujua kusoma na kuandika - tunakusudia kutokuwa na ujuzi wa ufahamu na maarifa, sio kusoma na kuandika tu - ambalo linawapelekea watu kuwa na akili finyu, hawawezi kubatilisha mafundisho ya mawazo yaliyopotoka, hivyo wanaanguka mvunguni mwa Ukanamungu kwa kuwa utamaduni wao ni wa chini sana.

2) Ukosefu wa elimu ya kidini, ambao ni hatari kubwa, hasa kwa kuzingatia hali ya utandawazi na uwazi wa kiutamaduni kwa mwingine, na mawasiliano ya haraka kupitia vyombo vya mawasiliano vya haraka, ambavyo vimesababisha ulimwengu kuwa kijiji kidogo, na maeneo mengi ya saiti za machafuko, na wingi wa uchafu unaopitishwa kupitia tovuti za mawasiliano

za ulimwengu, zimevumilia hata matukano na dharau ambayo hutoka kwa washambuliaji juu ya Mwenyezi Mungu, manabii na wajumbe, amani iwe juu yao.

Vilevile kama Ukanamungu unavyoweza kukutana na moyo mtupu na kuujaza, inaweza pia kukutana na akili tupu na kuiharibu. Vijana, kwa sababu ya ukosefu wa elimu, wanaweza kupatwa na maoni ambayo huleta Ukanamungu.

3) Kujitokeza wazi kwa tuhuma bila ya kujikinga hata kwa kadiri chache sana ya elimu, na kuingia katika majadiliano na watu wakanao Mungu na kudharau dini, ambapo wanapuuza uwezo wa mpinzani kuleta tuhuma na kuharibu mawazo ya vijana. Vijana wengi hushikwa na jambo hili linalowafanya kuhisi hali ya kutolewa na ukombozi, na kupinga nasaha kutoka kwa wasomi au watu wenye uzoefu.

4) Kupanua upungufu wa wenye dini na kunasibisha athari zake kwa dini yenyewe. Haijalishi ikiwa upungufu huo ziwe ni ule unazohusiana

na upungufu wa kibinadamu, kama kutokuwa na uwezo, dhuluma, ujinga, uchoyo, uvivu, na utafutaji wa matamanio na mengineyo, au unahusiana na kasoro katika utumizi wa dini kwa ufahamu uliopotoka au tafsiri ya mbali ya matini za dini.

5) Vijana kukumbatia mafunzo ya dini ya kiroho au na kivitendo, na kuridhika na masomo ya elimu kavu ya kijuujuu au na mahubiri ambayo hayana uasisi na ubunifu.

6) Hamu ya vijana wengi ya kuasi mila na desturi zilizoenea katika jamii za Kiarabu, ambazo huziona kama ni vizuizi na zipo kinyume cha wazo lao la uhuru wa kibinafsi.

7) Misimamo mikali na ugumu wa kidini, husababisha kupindukia dini na ibada. Idadi kubwa ya wale wanaokanamungu, wamefanya hiivyo kama ni majibu ya kisaikolojia kutokana na misimamo mikali ya kidini, kijamii, au kifamilia, na uradikali wa kifikira.

8) Kuwepo kwa nadharia za kiakili au maswali ya kiawali yaliyomo akilini mwa vijana, yanayohusiana na Muumbaji na viumbe na ambayo yanatafuta majibu. Pindi masuali hayo yanapokabiliwa na makandamizo au maonevu, vijana wengi hukumbatia Ukanamungu. Hufanya hivyo kutokana na kuwa majibu ya maswali yao hayakuzitotosheleza akili zao, basi kwa hivyo hutafuta majibu ambayo hayawapatii chochote cha maana.

5- Misimamo Iliyopindukia Mipaka ya Vikundi Vyenye Misimamo Mikali:

Hakika njia za kuzidisha ukali wa kidini hadi kufikia hatua ya kukufurisha, malipuko, ugaidi, kumwaga damu na kuwatisha watu watulivu, kunakofanywa na vikundi vyenye misimamo mikali, kunawapelekea wengine kuyapinga matendo hayo kwa misimamo mikali pia, jambo kama hilo limewapelekea watu wengine kutoamini dini zote.

***

## Hatari za Ukanamungu Juu ya Mtu, Familia, na Jamii

Ukanamungu ni uzushi wenye hatari kubwa ambao huathiri mtu mmoja mmoja, familia, jamii na kadhalika. Mtu – kama ilivyojulikana – ni chanzo cha familia, na familia ni chanzo cha jamii.

Sharia zote za mbinguni zimewafikiana kwa yale yaliyo na heri kwa wanadamu, yanayoleta usalama wa nafsi, mali, heshima, na maadili za uadilifu, usawa, ukweli, uaminifu, hekima, utengenezaji wa nchi na watu, na mengineyo. Mambo hayo yanajulikana kwa jina la "makusudio ya kisharia", nayo ni misingi ya kibinadamu kwa ujumla ambayo hayahitalifiwi na sharia za mbunguni, wala hayakufutwa katika sharia yoyote.

Lakini Ukanamungu una mabaya na madhara yasiyohesabika yanayomsibu mtu, jamii, umma, na madola. Miongoni mwa madhara hayo

ni: machafuko ya maadili, kuenea kwa uhalifu, kusambaratika kwa familia na jamii, utupu na machafuko ya kisaikolojia, kuenea kwa matukio maovu kama vile kujiua, ushoga, na unyogovu wa kisaikolojia.

Kwa kuwa anayeenda njiani humo anajiangamiza kidunia na kidini, ukweli wa wakanaMungu ni mchungu na umejazwa na magonjwa ya kiwiliwili na kisaikolojia kutokana na ushoga, ukware, unyogovu, kuenea kwa uhalifu, upanuzi wa kujiua, kuua, na kulipuka. Mwenyezi Mungu anasema: ﴿Na atakayejiepusha na mawaidha yangu, basi hakika yeye atapata Maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua nah ali ni kipofu (124), Atasema: Mola wangu! Mbona umenifufua kipofu, nah ali nilikuwa (duniani) ni mwenye kuona? (125) Atasema: Ndivyo vivyo hivyo, Aya zetu zilikufikia, ukazisahau. Na hivi ndivyo leo utasahauliwa (126), Na hivi ndivyo tutakavyomlipa kila apitaye kiasi n ahakuamini Aya za Mola wake, na bila shaka adhabu ya Akhera na kali zaidi na yenye kudumu zaidi (127) ﴾ (20:124-127)

Na Anasema: ﴿**Na waliokufuru, waangamizwe, na vipotee vitendo vyao**﴾ (47:8).

Hayo yanathibitisha kuwa dini ni msingi wa maisha na nguzo yake. Maisha bila ya dini ni maisha bila ya maadili, sharia, wala uongofu. Dini ni mgongo unaodhibiti mwenendo wa wanadamu kwa njia iliyonyooka, na adhabu ya kidunia yoyote na mila na desturi peke yake haziwezi kudhibiti taharuki ya mtu duniani, isipokuwa ameungana vyema na Muumba wake.

Kwa hivyo, yafuatayo yanaeleza hatari za Ukanamungu:

**Kwanza:** Hatari za Ukanamungu kwa mtu.

**Pili:** Hatari za Ukanamungu kwa familia na jamii.

**Kwanza: Hatari za Ukanamungu kwa Mtu:**

Hatari za Ukanamungu zinaonekana wazi juu ya mtu asiyefuata njia nyoofu ya Mwenyezi Mun-

gu, kwani Ukanamungu unapoteza makusudio ya sharia ambayo yanampasa kila mtu ayaangalie, nayo ni: kuhifadhi dini, nafsi, vizazi, akili, mali, na nchi vilevile.

Ili kubainisha athari za Ukanamumgu juu ya kila kusudio, na juu ya mtu, tutaeleza kila kusudio kinaganaga kama ifuatavyo:

**Kusudio la kuhifadhi dini:**

Dini ni Sharia za Mungu ambazo Mwenyezi Mungu amewatuma Mitume kwazo kuwaongoza watu kwenye ukweli wa akida, na heri ya mwenendo na kutendeana baina yao. Basi, kwa kuingia ndani ya Sharia hiyo na kuinyenyekea, wanapata uchangamfu wa dunia na akhera. Mwenyezi Mungu anasema:  Basi yule atakayefuata uongufu wangu, hatapotea wala hatapata mashaka * Na atakayejiepusha na mawaidha yangu, basi hakika yeye atapata Maisha yenye dhiki (20:123-124).

Hakuna shaka kuwa Ukanamungu kwa maana zake mbili, nazo: kukana uwepo wa Mwenyezi Mungu, au kukana dini, inafuta kusudio hilo kikamilifu, kwani unamaanisha hakuna anayestahiki kuabudiwa, na hivyo, hakuna dini.

Hii inamaanisha kuwa mtu anaishi kama wanyama, bali duni ya wanyama, kama alivyosema Mwenyezi Mungu: ﴿**Hao si chochote ila kama wanyama , bali wao ni wenye kupotea njia zaidi**﴾(25:44). Anaeneza uharibifu ardhini bila ya kitisho wala vizuizi, akiabudu matamanio yake kama alivyosema Mwenyezi Mungu:﴿**Je! Umemuona yule aliyefanya matamanio yake kuwa ndiyo Mungu wake, na Mwenyezi Mungu akamuacha kupotea pamoja na kuwa ana ujuzi, na akapiga muhuri juu ya masikio yake na moyo wake, na akajaalia kifuniko machoni mwake? Basi ni nani atakayemuongoza baada ya Mwenyezi Mungu? Basi je! Hamkumbuki?**﴾ (45:23)

Hakika, wakanamungu hawasukumwi ila kwa ujinga na matamanio; ujinga unawapeleka ku-

kana vitu visivyoweza kukanwa kama udharura wa kuwepo kwa muumbaji kwa kila kiumbe. Na matamanio yanawasukuma kujiepusha na vizuizi vya dini na Sharia zake ili wacheze na kula na kustarehe, kama alivyosema Mwenyezi Mungu: ﴿**Lakini waliokufuru hujistarehesha (duniani) na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makazi yao,**﴾ (47:12).

**Kusudio la kuhifadhi nafsi:**

Mwenyezi Mungu alimuumba mwanadamu, akamvaza mavazi ya heshima, na akampa fadhila juu ya viumbe vyingi kwa kumzawadia akili, elimu, kusoma bayana, umbo, sura nzuri, maumbile sharifu, mwili mnyoofu, kupata maarifa kwa uchunguzi na fikira, kujipamba kwa maadili mema, na akamhifadhi kwa uangalizi na utunzaji tangu alipokuwa tumboni mwa mama yake katika vipindi vyote vya kuwemo humo mpaka akawa kiumbe kingine; ametukuka Mwenyezi Mungu, Mbora wa waumbaji.

Hifadhi ya nafsi ni kuilinda na maangamizi, ikiwa ya mtu mmoja au ya wengi, kwani ulimwengu (jamii) umetungwa kwa watu mmoja mmoja, na kila mmoja ana sifa zake zinazochangia maendeleo ya ulimwengu.

Hifadhi ya nafsi haimaanishi kuihifadhi kwa kisasi, kama walivyosema baadhi ya wasomi, kwani kisasi ni fidia baada ya nafsi kwisha kuharibika, lakini hifadhi ya nafsi inamaanisha kuihifadhi isije ikaharibika, wala haimaanishi kuihifadhi kiwiliwili tu, bali kuihifadhi kiroho pia kwa lengo la kuiwezesha kutekeleza ujumbe wake wa kuendeleza ulimwengu na kuhakikisha sababu za kuweko kwake ardhini.

Kusudi kubwa la hifadhi ya nafsi katike ujumbe wa Uislamu ni kuitukuza na kuitakasa, Mwenyezi Mungu anasema: ﴿**Mola wetu! Watumie Mtume anayetokana na wao, awasomee Aya zako, na awafundishe Kitabu na Hekima na awatakase. Hakika Wewe ndiwe Mwenye nguvu, Mwenye**

**hekima.**﴾ (2:129) na anasema: (Yeye ndiye aliyeleta Mtume katika watu wasiojua kusoma, anayetokana na wao, awasomee Aya zake na kuwatakasa na kuwafunza Kitabu na Hekima, na hali wao kabla ya haya walikuwa katika upotevu dhahiri) na anasema: ﴿**Bila shaka Mwenyezi Mungu amewaneemesha waumini alipowaletea Mtume miongoni mwao, akiwasomea Aya zake, na kuwatakasa, na kuwafundisha Kitabu na Hekima, na ijapokuwa bila shaka walikuwa kabla ya hapo katika upotevu dhahiri,**﴾ (3:164). Kwa hivyo, miongoni mwa dua ya Mtume (SAW) ilikuwa: "Ewe Mola wangu! Ipe nafsi yangu uchamungu wake, na itakase, Wewe ni Mbora wa wenye kuitakasa, Wewe ni Mola wake na Bwana wake". Na Mwenyezi Mungu aliapa viapo kumi na moja kuhusu mafanikio ya aliyeitakasa nafsi yake, na upotofu wa aliyeichafua, kama ilivyotajwa katka Suratush-Shams: ﴿**Bila shaka amefaulu aliyeitakasa (nafsi yake), Na bila shaka amepata hasara aliyeichafua (nafsi yake)**.﴾ (91:9-10).

Utakaso huu una mitindo ya kiroho, baadhi yake ni kidhahania na mingine ni ya vitendo ili nafsi itakaswe kwa fadhila, na isafishwe na maovu. Miongoni mwa ile ya kidhahania ni pamoja na: Kumpwekesha Mwenyezi Mungu, kutubu, kuwa na subira, ukweli, kujiangalia, kujitahidi na mingineyo. Na miongoni mwa ile ya vitendo ni: swala, Saumu, Hija, Zaka, Dhikri, kutafuta elimu, na mingineyo.

Lakini Ukanamungu unasababisha uharibifu wa nafsi kwa kujiua au kuishi kama wanyama bila ya lengo wala kusudio.!

"Hakika mtindo wa wakanamungu haukuwapa nafasi ya kupata amani, matumaini, wala uchangamfu, na dalili ya hayo ni takwimu za kimataifa (international statistics) zinazozungumzia kiwango cha moja kwa moja (direct rate) baina ya Ukanamungu na kujiua". Ukanamungu unaweza kuiletea nafsi mauti ya kimwili kwa kujiua, na pia unaweza kuwa mauti kidhahania in-

ayomfanya mtu aishi bila ya maana wala thamani kama wanyama au chini kuliko wanyama!

Wakati ambapo Uislamu unalenga kuitakasa nafsi, Ukanamungu unaichafua na kuizamisha kikamilifu katika madhambi na maasi, na kwa hivyo inaiepusha na fadhila na kuijaza machafu.

**Kusudio la kuhifadhi vizazi:**

Hakuna hitilafu kuwa hifadhi ya vizazi, hifadhi ya ukoo, na hifadhi ya heshima ni miongoni mwa makusudio ya kimisingi. Na ikiwa hifadhi ya vizazi ni muhimu kwa binadamu, basi, hifadhi ya ukoo ni muhimu kwa familia, na hifadhi ya heshima ni muhimu kwa mtu binafsi, na uko uhusiano mkubwa baina ya pande hizi tatu, kwa kuwa hifadhi ya heshima huleta hifadhi ya ukoo, na hifadhi ya ukoo huleta hifadhi ya vizazi.

Hakuna shaka kuwa athari mbaya za Ukanamungu zinapoteza kusudio hilo; maadili yanabomoka, na mahusiano ya kifamilia yanaporomoka,

na familia zenyewe zinasambaratika, na zinaposambaratika, ukoo, nasaba, na heshima zote zinaharibika.

**Kusudio la kuhifadhi akili:**

Mwenyezi Mungu amewafadhilisha wanadamu kwa akili, na kwayo amewapendelea kuliko viumbe vyote kwa ajili ya kutafakari na kuzingatia na kutofautisha, na aliwakemea wale wasiojali neema hizi wala hawazipi haki zake, akasema Mwenyezi Mungu: ﴿**Je hawatambui**﴾ (36:68), ﴿**Je, hamtafakari?**﴾ (6:50), ﴿**Je! Hamkumbuki?**} (6:80) ﴿**Basi je! Mbona hawaizingatii Qur'ani? Au katika nyoyo zao kuna kufuli?**﴾ (37:24), na kwa akili hii, mwanadamu amekuwa khalifa ya Mwenyezi Mungu ardhini mwake.

Hakuna anayepinga kuwa akili ni manufaa makubwa, cheo cha juu, na sifa nzuri. Ili kupata manufaa ya dunia na akhera lazima kuna Sharia, na Sharia haifai bila ya akili, kwa sababu akili ndiyo msingi wa utaklifu.

Uislamu umethamini akili sana, na ukashughulika sana na kuihifadhi na kuikuza, maana Uislamu ulifungua mlango mbele ya akili kufikiri na kuzingatia. Hakuna Aya wala Hadithi inayozuia akili au kufunga njia yake.

Lakini Ukanamungu kwa mitindo yake hauheshimu akili, kwa kuwa mitindo ya wakanamungu na mbinu zao katika kujadiliana na kuhojiana zinategemea mtindo wa kujadili kwa kutumia makosa na uwongo kwa lengo la kumbabaisha mpinzani, nao kwa mtindo huu hawaheshimu mitindo ya kielimu iliyo sawa katika mjadala.

Hakika mtindo wa kikanamungu ni mtindo unaojipinga; unaamini kitu fulani na kukikataa wakati ule ule. Kama vile, unakataa kuwa Mwenyezi Mungu alimuumba Adamu (Amani iwe juu yake) kutokana na udongo, kisha alizaa vizazi kadhaa, kwa sababu mambo haya ni ghaibu (hayaonekani), pindi unaamini kuwa asili ya binadamu ni chembe hai iliyopatikana kabla ya mamilioni ya miaka, kisha ikaongezeka kwa uzazi wa kitabia, ijapokuwa hii ni jambo la ghaibu pia, lakini

wanalikubali kwa sababu chanzo cha fikira hii kinatokea kwa mkanamungu. Lakini hawalikubali swala la kuzaliwa kwa Adamu, kwa sababu kunatokea kwa Wahyi. Maana yake, mtindo wa Ukanamungu unajipinga, hauna sharia ila matamanio, kwa hivyo, wakanamungu ni maadui wa akili hata wakidai kuwa wao ni watu wa akili.

Kwa hivyo, tunaona Anthony Flew, mkubwa wa wakanamungu katika nusu ya pili ya karne ya ishirini anarudi baada ya safari ndefu kuamini kuwa Mungu yupo, baada ya kufikia miaka themanini. Alitowa kitabu katika mwaka 2007 akieleza humo sababu za mgeuko wake, zinazoweza kufupishwa katika uvumbuzi wa kisayansi ya kisasa ulioonesha utatuzi wa kushangaza sana wa maumbile na uanzishaji wa ulimwengu na uhai.

**Kusudio la kuhifadhi mali:**

Miongoni mwa uhakika ambao hakuna mtu awezaye kuutilia shaka ni kuwa mali ni mojawapo ya nyenzo muhimu za maisha ambapo hapana

yeyote anayeweza kujiepusha nayo katika nguvu yake, mavazi yake, wala makao yake. Kutokana na mali mtu huweza kukidhi haja zake za lazima, na za kujiboresha kihali.

Mali imetajwa katika Qur'ani katika Aya nyingi, na katika Sunna vile vile. Nayo ni mojawapo ya vitu viwili ambavyo ni mapambo ya dunia, kama alivyosema Mwenyezi Mungu: ﴿**Mali na watoto ni pambo la maisha ya dunia.**﴾ (18:46). Uislamu unawaita watu kukusanya mali kwa njia iliyo halali, na kuitumia katika mambo halali vilevile, na ilitukataza tusifanye ubadhirifu au kuitawanya bure.

Lakini Ukanamungu kama unavyoharibu makusudio tuliyoyataja juu, unaharibu mali pia, kwani Ukanamungu haulei dhamira ya mtu, wala haumtishi na Mungu mwenye nguvu anayeweza kuangalia mwenendo wake na matendo yake katika ardhi, kwa hivyo mkanamungu hukua na moyo mgumu bila ya hisia, akidharau sababu ambazo humkataza asifanye dhuluma na humuamrisha afanye hisani na mema.

Kinyume cha hayo, Ukanamungu unawafundisha wafuasi wake kuwa wameibuka kwa bahati, wala hawakuumbwa na Muumbaji, au wamejiumba, na kuwa wao ni wanyama wa kiardhi kama wanyama wengine. Na kwa hivyo, hisia zao zimekuwa ngumu, na huzidi kuwa za kinyama na kiduni, hadi huwapeleka kukidhi haja zao za matamanio na matashi kwa kupindukia mipaka.

Na wakinyimwa na matokeo ya maisha au kanuni za kubuni kufikia malengo na matashi yao ya kinyama, wanajitahidi kupindukia kanuni kwa hila na vitimbi, au kwa nguvu na mashindano, na katika hali hizi mbili, mkanamungu haoni makatazo ya kindani kwa sababu haogopi Mola wala hatazamii malipo. Maana Ukanamungu unapinga makusudio ya Sharia kuhusu hifadhi ya mali. Ni kinyume na Uislamu ambao unawaita wanajamii kukusanya mali kwa njia zilizo halali, na kuitumia katika njia zilizo halali pia, na kuihifadhi isitawanyike bure. Kwa mnasaba huo, tunaona kwamba Ukanamungu unawaita watu kufanya yaliyo kinyume cha hayo.

**Kusudio la kuhifadhi nchi:**

Hakuna shaka kuwa upendo wa nchi na kuihifadhi ni silika ya kibinadamu iliyosisitizwa na Sharia tukufu. Masilahi za nchi ni mojawapo ya kiasili ya makusudio ya dini yasiyoachika nayo. Tumezaliwa na kukua tukijifunza kuwa kulinda nchi ni mojawapo ya mambo mawili: Wajibu juu ya kila mtu binafsi, au wajibu juu ya umaa kwa jumla.

Basi, umma ukiwa unaishi katika usalama na utulivu, haishambuliwi kwa ugaidi wala uadui, ulinzi wa nchi itakuwa wajibu juu ya umma kwa jumla, yaani wajibu huu ukitimizwa na baadhi ya wazalendo, wengine hawatalaumiwa, wala hawatakaripiwa.

Lakini nchi zikitokezewa na hatari yoyote, kutakuwa na wajibu juu ya kila mtu binafsi kuzilinda kwa hatari hizo, kila mtu lazima afanye anayoagizwa au awezayo kufanya mwenyewe ili kuiokoa nchi yake.

Hakuna shaka kuwa Ukanamungu ni hatari kubwa juu ya mtu, jamii, nchi, na umma wa Kiarabu wote, kwani unatishia umoja wa jamii na fikira kwa upande mmoja, na kutishia usalama wake wa kimataifa kwa upande mwingine. Chini ya jina la 'uhuru wa akida', maadui wa umma wanalenga kurarua umoja wake, na kuondoa utulivu wake katika kila uwanja wa maadili na wa desturi kwa njia zote na mitindo yote ya kishetani, na kwa kuchochea madai ya kijinsi, kikabila, na kikundi, na kwa njia hii Ukanamungu huelekezwa kisiasa na kimali, kwa kusudi la kuchochea fujo na michafuko…

Mipango ya maadui huwa yanalenga pande zote za maisha yetu na nguzo zake; jambo ambalo linahitaji kuwaamsha watu kukabiliana na hatari za kila mizushi miovu. Mipango yao hii inalenga kuondoa maadili mema moyoni mwa mkanamungu, na kuujaza kwa kila jambo la kumhamishia maadili na kujiangalia binafsi; yaani kutoangalia dhamira yake, na wala Muumbaji wa ulimwengu na uhai.

Hakika Ukanamungu ni tasnia ya maadui wa umma huu waliofeli kueneza fitina katika kitambaa chao cha kimataifa kilichofungamana sana, kwa hivyo, walijitahidi – miongoni mwa juhudi zao nyingine – kuporomoa umma huu, na kung'oa misingi yake kwa kueneza mahangaiko na shaka nyoyoni mwa wenye nyoyo dhaifu, na kwa kuwashawishi kuwa kuacha dini zao thabiti kutafungua milango ya uhuru wa matamanio na matashi yao bila ya kujisumbua kwa dhamira, au udhibiti wa mamlaka yoyote ya kiimani.

Wasomi wa Fiqhi waliamua kuwa jeshi la adui likiingia nchi moja ya kiislamu, basi jihadi itakuwa ni wajibu juu ya kila mwenyeji wa nchi hiyo akiwa mwanamume au mwanamke, mkubwa au mdogo, mzima au dhaifu, mwenye silaha au bila ya silaha; kila mmoja na uwezo wake, hata wakiuawa wote. Ikiwa ulinzi wa nchi si mojawapo ya makusudio muhimu ya Sharia, watu wangeruhusiwa kuacha nchi na kujiokoa. Mojawapo ya sababu kubwa za Ukanamungu ni mapenzi makubwa ya mata-

manio na matashi ya nafsi na kujizamisha katika uhuru usio na maadili. Mapenzi haya hulingana na Ukanamungu usiokiri halali wala haramu katika mamlaka yake, wala haukiri mwangalizi, hesabu, wala malipo, wala haukiri yanayoitwa kwa lugha ya kisasa "dhamira ya kujilaumu", yaani "nafsi inayojilaumu" inayompiga Mwislamu kwa mjalada wa majuto kwa kufanya maovu. Kwa hivyo, wengi wa wanaouelekea Ukanamungu wanasukumwa na matashi peke yeke; jambo linalotia nchi hatarini, na kuifanya bila ya maana katika macho ya wale wakanamungu ambao wamejisafisha nayo ila kwa kadiri inayowatekelezea matamanio yao, na hivyo wanajipoteza na kuwapoteza walio karibu nao.

Hakika Ukanamungu ni hatari juu ya makusudio ya Sharia inayojumuishwa katika kuleta masilahi kwa wanadamu, na kuwauepushia uharibifu, kwani unaangamiza makusudio haya na humletea mtu kinyume chake. Hatari hiyo inayompata mtu katika masilahi yake ya kimsingi inaathiri familia

na jamii, kwa sababu mtu ni mbegu wa familia, na familia ni chembe hai ya jamii.

Wakati wakanamungu wanadai usikivu na utekelezaji wa masilahi kwa upande mmoja, makusudio ya Sharia ndiyo yanayowakabili kwa nguvu na kwa ujumla wake.

## Pili: Hatari za Ukanamungu juu ya Familia na Jamii

Hatari ya Ukanamungu haiathiri mtu pekee, bali inaathiri familia na jamii, kwa kuwa jamii zinazoshikilia Ukanamungu zimenyimwa uongozi wa Mwenyezi Mungu ambao ameuteremsha katika vitabu vyake, na kwao ametuma Mitume yake na inayojumuisha rehema, uadilifu, na hekima.

Na kama tunavyojua, familia ni seli ya kwanza ya jamii, ambapo ikioza, mahusiano ya kifamilia na kijamii yanaoza vilevile. Hakuna kitisho chochote katika jamii zinazoshikilia Ukanamungu; hakuna dhamiri inayokaripia, wala Mola anayeogopwa, wala Siku ya mwisho inayoangaliwa.

Sifa hizo zinatambulisha fikira ya uyakinifu (wa kikanamungu) ambayo haiamini Akhera wala malipo, na inayotegemea kupata manufaa ya uyakinifu (materialism). Fikira hiyo huona kuwa kuwasaidia wengine ni upumbavu na ubaradhuli, madamu hakuleti manufaa ya karibu.

Matokeo mabaya ya Ukanamungu hayakufungiwa tu katika ufisadi wa familia, kwani athari zake haziwezi kuhesabiwa; bali zinazungukia upande usioonekana wa mtu na jamii ya kibinadamu. Aidha, zinapinga dini, maadili, na Sharia moja kwa moja, na hubomoa nguzo, misingi, na asili zake.

Ulimwengu wa kisasa unateseka na shida nyingi. Ingawa maendeleo makubwa ya uyakinifu na faida kubwa ambayo sayansi imetoa kwa maisha na ustawi wa binadamu, kuna shida ambazo huleta shida nyingine, na kila moja huathiri uwepo wa nyingine. Miongoni mwa shida hizi ni wasiwasi wa kisaikolojia, machafuko, uhalifu ulioenea, ukose-

fu wa maadili, ubinafsi, dhuluma kwa maana na aina zake zote, na uharibifu. Maendeleo ya mwanadamu hayakuweza kupunguza shida hizi, badala yake, kila mtu alipozidi kupenda vitu vya kimwili, shida hizi huzidi kuibuka na kuenea.

Ijapokuwa kuna idadi kubwa ya shida na namna zake mbalimbali, shida iliyo kubwa zaidi na yenye athari ya uharibifu, mtikisiko na wasiwasi ni shida ya Ukanamungu, kwa sababu Ukanamungu una hatari kubwa ya kujitenga na silika sahihi na itikadi safi ya Umoja halisi. Silika ya mtu ikivunjwa, atavua mavazi ya Imani, na hatakuwa na cha kumlinda na shari na fitina. Ukanamungu unaambukiza akili kwa udhaifu ambao unazidi kutokana na sababu alizozitaja Dr. Abdul-Halim Mahmoud katika kitabu chake "Uislamu na akili" akisema: "Hakika tofauti ya akili za watu inasababishwa sana kwa sababu za nje: Mazingira, majirani, utamaduni, marafiki, hewa, masilahi, na nyinginezo, haya yote yanaathiri – kama atakavyo Mwenyezi Mungu – akili na matokeo ya zile akili, na kwa

wakati madhehebu zinazidi na vikundi vinazidi vilevile".

Ukweli unashuhudia kuwa wakanamungu wanafanya nishati kubwa kueneza upotevu wao, hasa miongoni mwa waislamu, maana walizidi, na sauti yao ikawa kubwa. Watakuwa nguvu inayoathiri jamii ya kiislamu na inayoweza kufanya itakavyo kulingana na matamanio yao. Wengi wa wakanamungu wanatafuta masilahi yao ya binafsi, na hawatafuti ila matashi tu.

## Njia za kueneza fikira za Ukanamungu:

Ukanamungu unafuata njia mbili: Njia ya tuhuma, na njia ya matamanio. Mtetezi wake anajifungulia milango ya fitina na tuhuma, na kuruhusu akili yake iogelee katika mawazo na ndoto mbaya, hapo anajijaza akilini tuhuma moja baada ya moja. Kisha anazitilia Sharia na hukumu za Mwenyezi Mungu shaka, sio haya tu, bali pia anamtilia Mwenyezi Mungu mwenyewe na sifa zake shaka ili avunje kiungo cha Umoja mbali na shingo lake, na kumkana Mola aliyemuumba kutokana na ukosefu, ilhali amemwekea Sharia inayomtengenezea hali yake na mwisho wake, ili asizame katika bahari za matamanio na matashi au asiingie milango yake ya kudharau huruma. Na atakapofika upeo wa mbali sana nafsi yake itadhikika, na ataona kuwa ardhi ni finyu ijapokuwa ni pana sana, na huku anapinga huruma za Mwenyezi Mungu, na akadhani – baada ya kupofuka

– kuwa dini ni kizuizi kizito na Muumba hayupo.

Kukumbatia itikadi haribifu ni hatari kubwa, na matokeo yake Akhera ni mabaya sana, kwa kuwa kuzieneza katika vikundi vya jamii za Kiislamu ni shari isiyo na mipaka; mkanamungu anabeba dhima yake mwenyewe na ya itikadi yake, na Mwenyezi Mungu atamhesabu kwa aliyoyafuata na aliyoyatenda. Lakini akielekea kueneza tuhuma ya kidini na fikira za kikanamungu, hapo anawadhuru watu wote. Akida ni msingi wa mwenendo, na Imani ni chanzo cha matendo, basi zikitikisika akida za jamii, na zikitetemeka itikadi zao thabiti, mienendo yao itapotea, na hapo, hawatakuwa na sifa zinazowatambulisha, hawatakuwa na dhamiri na utakaso, uhalifu utaenea ukosefu wa usalama utajaa, na zitapotea mila na ibada, na kuharibu mahusiano, na hiyo ni misiba na madhambi anayoyabeba anayekusudia kueneza fikira zake mbaya na Ukanaamungu wake mwuovu tu, bila ya kupunguza madhambi ya wafuasi wake hata chembe. Hapa jamii inalazimika kusimama kidete

dhidi ya mtu yeyote anayejaribu kueneza tuhuma za kidini zinazovuruga mawazo safi ya Kiisilamu, au zinazotilia shaka Mungu mwenyewe na mafundisho ya Qur'ani. Mapinduzi ya kimaarifa, na mchupo mkubwa wa kiteknolojia unaoshuhudiwa ulimwenguni hayafichiki kwa yeyote, hata kuwasilisha mawazo na kuyafikia kukawa jambo rahisi; fikira yoyote ikiwa ya heri au shari inayotangazwa katika mitambo ya mawasiliano ya kijamii, inawafikia watu tele.

Njia wanazozifuata wakanamungu kuwafikia vijana waislamu – wanawake au wanaume- ni nyingi. Miongoni mwao ni: Vitabu, vya Ukanamungu vinavyouzwa au kutangazwa katika mitandao; si lazima viuwasilishe Ukanamungu moja kwa moja, bali vinaweza kuwa wazi, au vinatoa yale yanayoitwa "utamaduni wa shaka", au madai yanayodhoofisha imani kwa matini, au kuchukiza dini moyoni mwa msomaji na kuionesha katika sura ya vizuizi na vikwazo, na hivyo wakanamungu wanatupa mawindo yao kwenye pwani ya Ukanamungu,

maana yake, wanatekeleza malengo yao kupitia vipindi, sio kipindi kimoja.

Miongoni mwao pia wanatumia: Vituo vya satellite; kwa kuonesha dhana wazi au zisizo wazi za Ukanamungu, kupitia programu, mazungumzo, mijadala, au filamu - kwa watu wazima au watoto – nk….

Bali, inaweza kuwa kwa kupitia: programu za kisayansi ambazo zina mizizi ya nadharia inayountetea Ukanamungu, kama vile nadharia ya Darwin.

Miongoni mwa nyenzo wanazotumia pia ni: Mikutano ya moja kwa moja na vijana, kupitia vikao maalumu, mikusanyiko ya watu, au mabaraza ya kitamaduni, ambapo maoni na tuhuma zinawasilishwa.

Njia mbili zilizobakia ambazo ni hatari zaidi katika kuvamia akili za vijana na wavulana, ni hizi zifuatazo:

Ya kwanza: Mitandao "Internet":

Mitandao Imekuwa na nafasi kubwa ambayo haiwezi kufuatiliwa wala kuangaliwa kwa urahisi, na matumizi yake katika kueneza Ukanamungu yana njia nyingi. Miongoni mwao ni:

1- Vyombo vya mawasiliano vya kijamii: Ukweli unathibitika leo kwamba ni wimbi la kitamaduni lenye ushawishi mkubwa; wako watu ambao hukaa masaa mengi mbele yake kila siku; maana vinavutia sana.

Wakanamungu kupitia mlango huu wanawasilisha mipango na nishati zao kwa hamu kubwa, kwa kutumia mtindo wa dhahiri wakati mmoja, na kwa kujificha wakati mwingine. Wanawaslisha nadharia zao mbovu kwa maneno mazuri, kwa kujivuna kwa wakuu wao na matokeo yao ya kifikira, kuzitangaza tuhuma zisizo wazi na zenye usumbufu, kudhoofisha imani ya watu na wasomi, au kuimarisha mawazo na nadharia zinazofungua njia kwa fikira zao, kama vile, kulalamikia utunzaji

wa akili, na kuizunguka kwa milango ya kichuma, na wito kwa uwazi usio na mipaka, na kuelekeza maswala haya mabaya yanayochambua Uislamu na yaliyopambwa kwa njia za kujitenga nao.

2- Tovuti (saiti) za Kubadilishana na kutangaza video - maarufu zaidi ni “YouTube” - na huenda watazamaji wake ndio wakaotumia mtandao zaidi.

Wakanamungu hutangaza filamu zinazoimarisha Ukanamungu, au kuwakaribisha watu nao. Miongoni mwa hila zao mbaya ni kuwa wanatumia anuani au maneno yanayowavuta vijana zaidi kama vile, "mechi" au "mabao" au majina ya waigizaji, wachezaji, filamu, na sereali, kwa kuwa wanajua kuwa vijana wanatafuta namna hizi za filamu, na vijana wanapoona hizi filamu zenye sumu; wanavutiwa kuziangalia, na hapo zinaumia nyoyo zao.

Maendeleo ya mawasiliano ya kiteknolojia kupitia Internet yalichangia kuimarisha msingi wa

ubinafsi, na wa kuwatenganisha watu wanaoishi pamoja katika familia. Halafu, yametokea mageuzi katika nyavu za mahusiano ya kijamii, ambapo kila mtumiaji wa Internet akaanzisha mitandao yake hasa, kwa kusudi la kupata habari, kufanikisha hamu yake ya kupata msaada na ushirikiano, au kuunda mtandao mpya wa mahusiano ya kijamii.

Hii inadhihirika katika mikusanyiko ya kidhahania (virtual groups), ambayo huundwa kupitia vyumba vya gumzo, vikundi vya habari, na vikao kupitia "mtandao", jambo lililoleta mabadiliko yaliyo wazi katika uhusiano wa kifamilia na mahusiano mengine yenye aibu ya kuongeza ubinafsi na kupunguza hali ya kijamii iliyokuwa inatambulisha mahusuiano baina ya wanafamilia.

3- Mabaraza ya jumla ya watu: Kwa maana wakanamungu wanapanua nyavu zao humo - hasa mabaraza makubwa yanayohudhuriwa na watu wengi, wakipiga ndege wawili kwa jiwe moja - kama inavyosemekana-: wanatangaza

tuhuma, na kukamata mawindo yao kupitia "kuangalia", kisha "kukaribiana", kisha "kutilia shaka", kisha "kuweka misingi".

Ikiwa wanapata mshiriki - wa kiume au wa kike –anayeonekana kuwa ni rahisi kuvutwa, maana ni mwenye tabia ya ukombozi na uwazi, au chuki dhidi ya mila na ada, wanajitahidi kusifu maoni yake kwa maneno mazuri, na kwa njia hii, wanajenga mahusiano naye, kisha wanaendelea kidogo kidogo, kwanza, wanawasiliana naye kupitia barua pepe zao hasa, kisha wanazungumza moja kwa moja, kisha kushirikiana katika kundi barua pepe na kumpelekea makala, vitabu, na viungo vya tovuti (saiti) na anuani za blogi ambazo mwanzoni si lazima ziwe wazi, kisha mambo yanaendelea mpaka wanamkamata kama windo jepesi, wakamuangusha katika bwawa tuli.

4-Blogi za tovuti za Ukanamungu, ambazo ni sumu, wanazotaka kuwavutia vijana.

Tukiziangalia blogi hizi, kwa upesi, tutaona kuwa wanaozitembelea ni wale wavulana au wa-

sichana wasio na misingi madhubuti ya elimu za kidini, na baada ya kuangalia yaliyomo humo hawatatoka kama walivyoingia, kwa sababu wakanamungu wana mitindo madhubuti, tuhuma, na uwongo unaoingia ndani sana kwenye nyoyo za vijana wadogo, ikiwa kwa mvuto wa kihemko, udanganyifu wa kiakili, kuchochea tuhuma, kugeuza hakika, kejeli, hekaya, mashairi, na mengineyo.

**Ya pili: Riwaya potofu:**

Kwazo tunakusudia riwaya za uongo kiakida, nazo hutumika kama ni kifaa cha kukomesha imani, kwa sababu riwaya ni hadithi, na roho mara nyingi huwa zinapenda hadithi, hasa kwa kuwa nyingi ya hadithi zao zinachochea uhemko, upendo, na matashi. Na kwa kweli namna hii ya riwaya huwa inawavuta sana wasichana na wavulana wengi wanye hamu kubwa ya kumiliki riwaya.

**Athari na matokeo ya Ukanamungu:**

Tufikirie umma wa wakanamungu tu, au umma ambao wengi wake ni wakanamungu, na

tuangalie vipi utakuwa mwenendo wake. Hakuna shaka kuwa utakwenda kombo, na mwishowe utaanguka chini sana, maana wakanamungu wanahalalisha zinaa na maovu mengine kama ulevi, wala hawaoni haya kula mali za wengine bila ya haki. Ni kweli maadili yana athari katika kupunguza maovu, lakini hayaweki hali ya jamii sawa ila zikiwa chini ya uangalizi wa akida thabiti ya kidini.

Ukanamungu wa kisasa umeacha athari zake juu ya mwenendo wa binadamu na maadili ya umma, kwa kuwa Mungu akifa, kila kitu kitakuwa halali, na ikiwa "akida ya Ukanamungu" ni kukana ghaibu zote, na mwanzoni kabisa ni kumkana Mungu.... basi "kanuni ya Ukanamungu" ni nini? Kanuni hii inaweza kufupishwa kwa msemo wa Dostoevsky katika kazi yake bora "Ndugu Karamazov": Mungu akifa, basi kila kitu ni halali.

Athari za Ukanamungu juu ya familia na jamii ni nyingi, miongoni mwao ni:

**Machafuko ya kisaikolojia:**

Hakika jamii iliyo chini ya mamlaka ya Ukanamungu imekuwa inafanana na jamii ya msituni; kila mnyama aliyemo humo anajaribu kuwinda mwingine, na kwa hivyo, dhaifu anajaribu kujificha na kudanganya wengine, na mwenye nguvu anaamua ukandamizaji, ukatili, na ujeuri. Unyonyaji, udhalimu, na unafiki zikawa tabia, dini, na njia mpya kwa jamii ambazo ziko mbali na njia ya Mungu.

**Masumbuko na Kutojali:**

Kuruka mipaka katika uwiano kumesababisha dhana nyingi za kisilika na za kiasili za binadamu kama furaha na masumbuko kutiliwa shaka kwa sababu ya ukosefu wa vipimo na kutoweza kuamua.

Mtu aliyepotea kimaadili na uongofu kwa jumla hawezi kujenga ustaarabu au kuuhifadhi, na dalili iliyo wazi ya haya ni jinsi "Stalin" alivyo-

tendeana na dini wakati wa Vita vya Pili vya Dunia. Alipojua kwa yakini kuwa itakayosukuma jamii ya Kirusi kulinda nchi na umma wao ni dini, aliipa dini heshima na thamani yake. Jambo linaloshangaza sana ni kuwa takwimu zilionyesha kuwa zaidi ya 70% ya jamii ya Urusi wakati huo walikuwa wanaficha imani yao, kwa sababu Ukanamungu haukuweza kutosheleza mahitaji yao ya kiroho au ya kimwili.

**Ubaradhuli na Ushoga:**

Uyakinifu (materialism) wa Ukanamungu unaamsha matashi ya ngono, hadi kufikia matukio ya ubakaji ulioenea, ingawa eneo la kujiridhisha ngono yao ni wazi kwao.

Machafuko ya uhusiano wa kingono yana athari zake: ukosefu wa ndoa, na kuibuka kwa magonjwa ya kuambukiza. Labda utafutaji huu wa raha safi ya kingono unaelezea kuongezeka kwa ushoga katika jamii zinazokumbatia Ukanamungu.

Mapinduzi ya kingono yanaweza kufupishwa kwamba ni matamanio ya kingono yanayopeperushwa kutoka kwenye akili zao, na badala ya kumkomboa mtu, yanamtenga hadi yanamfanya awe mtumwa wa uasherati ambao huenea na ukawa ni jambo la "kawaida". Kama kwamba lengo la uasherati halikuwa kutosheleza matamanio tu, bali kumpunguza mwanadamu asiwe chochote zaidi ya mwili, kwa hivyo uchi huanza na mwili na kuishia na kumwondoshea mtu mfumo wa ubinadamu wake. Kwa haya yote, ngono huzingatiwa kwa njia isiyo ya kawaida kama kwamba ni shughuli ya kibaolojia iliyotengwa na maadili. Kwa hivyo, ukahaba sasa unatajwa katika jamii zingine za kikanamungu kama shughuli ya kiuchumi, ni tendo la misuli ambalo halitofautiani na kazi zingine. Kwa hivyo, makahaba sasa huitwa katika jamii kadha "mfanya biashara ya ngono".

Hii yote ina lengo la kuitenganisha ngono mbali na madhumuni yake ya kijamii na ya kibinadamu, ili iwe ni mwenendo wa vitendo kwa

ajili ya furaha na raha tu. Mtenda ngono anakuwa amejitenga na urithi wake wa zamani, na uwepo wake wa kibinadamu, kwa hivyo anaishi katika mwili akitafuta raha ya moja kwa moja ambayo haina uhusiano wowote na uzuri au ubaya.

**Miongoni mwa ushoga ni ndoa ya jinsia moja:**

Hakuna shaka kwamba mahusiano ya jinsia moja na ndoa ya jinsia moja yamekuwa ni "majanga" ambayo hayawezi kukataliwa katika jamii ya Uyakinifu (materialism) na wazo la kikanamungu, na wafuasi wa njia hii wanazingatia kuwa jambo hilo ni uhuru wa kibinafsi na wanalilinganisha na uhusiano kati ya wanaume na wanawake.

Takwimu zinaonesha kuwa idadi ya watu wanaojiua miongoni mwa watu wa jinsia moja ni mara kumi na nne kulingana na watu walio sawa. Tafiti pia zimeonesha kuwa watu hawa hutumia dawa za kulevya zaidi ya wengineo, na wanakabiliwa zaidi na shida za kisaikolojia na kitabia.

**Masambaratiko ya Familia:**

Zamani, jamii nyingi za kibinadamu zilijaribu "kuleta utulivu" moyoni mwa mwanadamu, ili kudumisha uwiano baina ya nafsi yake na tabia. Jamii za kibinadamu haziwezi kuendelea bila ya kuimarika mahusiano ya baina ya mtu na makundi ya kijamii ili kuhifadhi masilahi yao na kudhamini uwepo wao.

Hakuna shaka kuwa udini ni sababu nzuri ya kufahamiana, maelewano, ushirikiano, na msaada, kwa kuwa Imani ni imani ya maadili na desturi za maishani, mbali na mali, ufahari na vifaa vya ulimwengu, bali jambo la mwanzoni kabisa ni kuishi kibinadamu, kiadabu, kimwenendo, na kujithamini.

Na kwa kweli dini inaimarisha sana uhusiano baina ya mume na mke, kutokana na utukufu wa uhusiano wa ndoa, na kuimarisha mahusiano ya familia yaliyopo baina ya wazazi na wana, na kuuhimiza ukoo uwasiliane, na kuhifadhi haki

za majirani, na kuonesha huruma kwa watu na kuwakaribia katika mfumo unaorudisha wanadamu wote katika asili moja na chanzo kimoja, na Muumbaji mmoja; Mwenyezi Mungu anasema: ﴿**Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni mataifa mengi na makabila mbali mbali ili mjuane. Hakika mwenye heshima zaidi miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni mwenye kumcha-Mungu zaidi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye elimu, Mjuzi**﴾ (49:13), na anasema: ﴿**Basi je, haielekei mkitawala, mtafanya uharibifu katika ardhi na kuwakata jamaa zenu? Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu aliwalaani, akawatia uziwi na kuyapofua macho yao**﴾ (47:22-23). Tunakuta kuwa kitu chenye thamani kubwa kilichovurugwa na Ukanamungu katika binadamu ni familia, kutokana na machafu uliyoyaleta, na uhuru wa tabia ya ngono bila ya ndoa, hadi ukasababibisha upotofu wa nasaba, ambapo wazaliwa wamekuwa hawapati uangalifu wala familia za kunasabishwa nazo ili kumlinda.

Kwa njia hii, lilizalika rika lisilojua mahusiano yanayotawala mwenendo wake duniani isipokuwa mahusiano ya uyakinifu na ya kimasilahi binafsi; Wenye rika hilo wanaona kwamba uhusiano wa ndoa ni kama vikwazo, na hivyo hawaoni umuhimu wa kuwa na familia au watoto, kwa sababu masambaratiko ya familia huzaa yule mtu anayefikiri katika kutekeleza mahitaji yake bila ya kujali mahitaji ya wengine wala haki zao.

Zaidi ya hayo, mkanamungu ni mtu mbinafsi anayedai kujitosheleza, asiyekubali wala kujali mipaka, vikwazo, wala madaraka. Anataka kukidhi matashi yake papo kwa papo (sasa na hapa), hasa tukijua kuwa jamii ya kikanamungu ni jamii ambayo haijali ila masilahi yake tu, na miongoni mwao hakuna anayejua maadili yanayomsaidia kupita mipaka membamba ya dhati yake mwenyewe. Hakika mtu kama huyu hawezi kukubali kamwe mpango wa familia, kwa hivyo anazidi kukataa kupata watoto au kufunga ndoa, na wakati huohuo zinazidi hisia zake za kuwa familia ni mzi-

go usiokubaliki, na kuwa kuwalea watoto ni majukumu yanayopita mipaka ya uwezo wa binadamu.

**Uhalifu:**

Uhalifu katika jamii za kikanamungu haukusababishwa na ufukara wala umaskini, bali unasababishwa na silika za kihalifu zinazaosababishwa na madai ya uhuru na mawazo ya uyakinifu, na mashindano kwa ajili ya matamanio na matashi ya maisha yanayotishia mfumo wa kimataifa kwa kueneza fujo na uasherati miongoni mwa mataifa, kwa kusaliti na kudai madai mabaya juu ya akili za wenyeji wake, na kuharibu nguzo zote za dini, uzalendo na tabia njema.

**Njia za kukabili Ukanamungu**

Utangulizi juu ya kufahamu makusudio ya Sharia na jukumu lake katika kukabili uzushi wa Ukanamungu:

Miongoni mwa maana kubwa katika Qur’ani tukufu ni kuteremka kwa Kauli ya Mwenyezi

Mungu isemayo: ﴿**Leo nimekukamilishieni dini yenu, na ukutimizieni neema zangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe dini.**﴾ (5:3) uUsiku wa Siku ya Arafa, siku ya Ijumaa, kwa kusudi la kuwasilisha habari hii kuu kwa maelfu ya watu; Myahudi mmoja alisema juu yake: “Aya hii ingelikuwa imeteremka kwetu sisi mayahudi, tungelifanya siku ya kuteremka kwake ni Sikukuu”.

Hakuna shaka kuwa Uislamu ni mfumo wa maisha, kwa Sharia yake, Fiqhi yake, makusudio yake, na misingi yake kama alivyosema Mwenyezi Mungu: ﴿**Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote. Kisha kwa Mola wao watakusanywa**﴾ (6:38), na msemo wa Abu-Bakr As-Siddiq: "Ingelipotea Kamba ya ngamia ningeliikuta katika kitabu cha Mwenyezi Mungu". Mwenyezi Mungu amrehemu mshairi Ahmad Shawky aliyesema: Sikuona hukumu isipokuwa hukumu ya Mwenyezi Mungu, wala sikuona mlango isipokuwa mlango wa Mwenyezi Mungu.

Maana ya kilugha ya neno Fiqhi kwa Kiarabu ni kufahamu kwa jumla, yaani huwa na elimu na utambuzi madhubuti. Lakini maana yake ya kiistilahi wakati wa mwanzoni mwa majilio ya Uislamu ilikuwa ni sawa na maneno ya "Sharia" na "Dini", yaani inajumuisha hukumu zinazohusu akida, maadili, ibada, au miamala. Na hali hii iliendelea mpaka wakati wa Abu-Hanifa aliyeita elimu ya Umoja ('ilmut-Tawhiid): "Fiqhi kuu".

Kisha maana ya Fiqhi ikabadilika tena, na ikawa inamaanisha elimu ya hukumu za kisharia za vitendo tu kutokana na dalili zake za kiutondoti zinazomaanisha: Dalili pekee ambazo kila moja yake imehusika na hukumu fulani, kama vile, msemo wa Mwenyezi Mungu: {**Na simamishseni Swala**}, (2:110), na {**Wala msikurubie zinaa** } (17:32) msemo wa kwanza ni agizo "wajibu", na wa pili ni katazo linalomaanisha "haramu". Makusudio ya Sharia – yaani malengo yake- yamejumuika katika "ketekeleza masilahi ya waja, na kuwaondolea madhara" duniani na Akhera, na kwa

makusudio haya,  furaha yao ya kweli duniani na Akhera itatekelezwa, na kwa sababu hii Uislamu ukawa rehema kwa viumbe vyote, Mwenyezi Mungu anasema: ﴿**Na Sisi hatukutuma ila uwe rehema kwa viumbe vyote**﴾ (21:107).

Hakika, Sharia ya Kiislamu - ni kama sharia yoyote ya mbinguni – imelenga kuhifadhi mambo maalumu waliyoyaita wasomi wa asili za dini "Makusudio (ya Sharia) ", nayo ni: Dini, nafsi, akili, uzazi, mali, na nchi. Ikiwa kuhifadhi akili ni mojawapo ya makusudio makuu ya Sharia, na kusudio hilo haliwezi kutekelezwa ila kwa kuihifadhi akili na upotovu unaoweza kuwa sababu ya kuiangamiza, kuiharibu, na kuiondoa mbali na silika yake safi, basi tunahitaji ufahamu sahihi wa makusudio ya Dini, ili utusadie kutatua uzushi huu wa hatari kwa njia ya vitendo.

Inaonekana kuwa mizushi ya kijamii inatofautiana na mizushi ya uyakinifu. Mizushi ya uyakinifu inayotokea inakuwa na sababu maalumu, ikipa-

tikana sababu, uzushi utapatikana, lakini mizushi ya kijamii ni migumu na imetatizika zaidi, kwa sababu haitokei kwa sababu moja, bali kwa sababu mbalimbali, na sababu hizi huweza kutofautiana kwa hitilafu ya hali na jamii, maana sababu zinazoleta uzushi katika jamii fulani huweza kutofautiana na sababu zinazoleta uzushi uleule katika jamii nyingine. Na hata zikiwa sababu ni zile zile katika jamii mbalimbali makisio ya kiidadi (quantitative assessment) ya sababu hizi yanaweza kutofuatiana kutoka kwa jamii moja hadi nyingine, na kutoka kwenye kesi moja hadi nyingine, na hali hii ndiyo inayotumika katika Ukanamungu.

Kwa mujibu wa maelezo hayo, hata kama tutaweza kuainisha moja ya sababu za Ukanamungu, hali hiyo haitamaanisha kuwa sababu hii peke yake huweza kuleta Ukanamungu, kwa kuwa sababu yaweza kuwepo, lakini uzushi usiwepo, kwa sababu uzushi huu huweza kutokea na sababu nyingine ikiwa ni za kiakili, kisaikolojia, au kijamii.

Kwa hivyo, njia za kukabili Ukanamungu lazima ziendane sambamba na njia mbili zifuatazo:

Ya kwanza: Njia za kuzuia:, njia hii huzuia sababu zinazotayarisha Ukanamungu kutokea katika jamii kwa njia ya kuangalia zaidi ulezi wa watoto, kushughulikia udhaifu wa kimaarifa, kuweka misingi madhubuti ya utambuzi sahihi wa kidini kupitia mitaala ya kielimu na kimaarifa, na kutekeleza uadilifu wa kijamii.

Ya Pili: Njia za maponyeo: Njia hii hutekelezwa kupitia kuchechemua jukumu la vyombo vya habari, taasisi za kielimu na kitamaduni, mashirika ya kienyeji na ya kihisani, vyama vya wafanyakazi, vyama vya haki za binadamu, na kujibu tuhuma za wakanamungu kwa pande za kielimu na kifalsafa.

Njia za kuzuia Ukanamungu

Kujenga jamii iliyo na misingi sawa na madhubuti – inayoshughulika na kuwalea watoto kwa njia sahihi, kujenga mfumo wa kimaarifa unaoan-

galia mabadiliko ya kimataifa, kuhifadhi kiini cha jamii na itikadi yake thabiti, pamoja na kutunza thamani ya mtu katika jamii hii, na kutekeleza uadilifu na mshikamano baina ya watu wake – kunafanya jamii kuongoka na wala haikubali kupotoka, bali hujilinda na mbinu za ushindi wa kiakili. Kwa hivyo, mambo yafuatayo ni muhimu sana katika kuzuia Ukanamungu:

**Kwanza: Jukumu la malezi mema katika kukabili Ukanamungu:**

Malezi ya kijamii yana jukumu la kuotesha uaminifu na maambatanisho rohoni mwa vijana, kuwafundisha na kuwazoeza watoto kutekeleza wajibu wao, na kuwaunganisha na jamii. Malezi ya kijamii ni "Mchakato wa ujifunzaji wa kijamii ambapo mtu hujifunza, akiwa mtoto au mtu mzima, kwa njia ya kushirikiana katika wajibu wa kijamii, hujitayarisha kupata mazoea ya kijamii na maelekezo ya kisaikolojia, na hujifunza jinsi ya kutimiza majukumu yake kwa njia ambayo jamii na jamaa zake wanayakubali".

Ijapokuwa msingi wa mchakato wa malezi ni kuwatayarisha watoto kujiunganisha na jamii zao, malezi ya kijamii hayahusiki na kipindi maalumu, bali jamii huenda ikayahitaji katiki vipindi mbalimbali, kwa sababu mwanajamii katika vipindi hivi anajiunganisha na makundi mbalimbali, na hutekeleza majukumu mapya yanayomlazimu kubadilisha mwenendo wake na kupata mbinu mpya za kuamiliana na watu.

Ni wajibu wa jamii kuunganisha juhudi zake wakati wa kutimiza mchakato wa malezi kwa njia sahihi, maana mchakato wa malezi ni sababu muhumu zaidi ya kuwepo maendeleo ya jamii.

Yafuatayo ni malengo ya kiujumla ya mchakato wa malezi, miongoni mwa jamii:

A- Kuthamini sana uhusiano wa mapenzi baina ya mtoto na mama yake, na kuweka mipaka ya kuvutwa na wengine.

B- Kuwafundisha watoto mifumo ya jamii wanayoishi ndani yake, ili iwe rahisi kuhama ku-

toka kwa mafunzo na mila za jamii kuelekea kushawishika na kufuata utamaduni wa jamii husika.

C- Kuwafundisha watoto kuwa na hamu zaidi ya kuishi katika utamaduni huu.

D- Kuwafundisha watoto majukumu ya kijamii.

E- Kuwapatia watoto stadi zinazosaidia kujipatanisha na watu wa jamii, na kupata vifaa vinavyowasaidia kuungana na vikundi kama vya lugha nk.

F- Kuimarisha maadili na malengo ya kikundi ambacho mtoto ni mmoja wake, na ambayo huunda utamaduni wa jamii anamoishi, kutimiza matarajio ya majukumu atakayoyakabili siku moja, kama vile kumuandaa mtoto kutekeleza jukumu la kuwa kaka, mtoto, rafiki na baba.

G- Kumpatia mtoto vipimo vya maadili ambavyo vinasimamia uhusiano kati ya mtu na kikundi,

na vipimo hivi vinawakilisha mamlaka ya nje juu ya mtu.

Ama kuhusu jukumu la kuwalea vijana kukabili Ukanamungu na mawazo ya uharibifu, kutatua utatuzi wa tatizo hili unaanzia katika malezi ya kijamii, maana ni mchakato ulio muhimu sana kwa upande wa athari zake juu ya vijana katika vipindi mbalimbali vya maisha yao. Malezi haya yana jukumu la kimsingi katika kuunda utu na utimilifu wake. Aidha, ni mmoja wapo ya michakato ya kujifunza mambo ambayo kwa njia yake watoto wanajipatia mila, desturi, mwenendo na maadili yaliyopo katika mazingira yao na yanayohusu jamii wanamoishi.

Mchakato wa malezi wa kijamii hutimizwa kupitia njia nyingi ambazo ni pamoja na: Familia, taasisi za kielimu, kutoka katika skuli na vituo vya maandalizi hadi vyuo vikuu, vilabu, jamii, viwanja vya vijana, nyumba za ibada, vituo vya kitamaduni, na vyombo vya habari.

Jukumu la Taasisi hizi ni kushughulikia mambo yafuatayo:

1- Kupandikiza itakadi sahihi rohoni mwa watu kwa njia mbalimbali, kama vile, mafundisho, mihadhara, mawaidha, hotuba, programu, mitaala, na zaidi.

2- Kuhimiza vijana kujiamini sana, na kuamini ustaarabu na maadili yao kuliko ya wengine. Njia ya kutimiza jukumu hili ni kuwapa mifano ya kihistoria na ya kisasa kutoka katika madola yaliyoweza kuchangia katika ustaarabu wa kimataifa.

3- Kuimarisha hisia ya fahari kwa imani na yakini, na matumaini yanayoyatokea kwa mtu na jamii.

4- Kudhihirisha upeo wa hatari za Ukanamungu juu ya watu, maana hatuwezi kuona kuwa watu wa jamii fulani au wanadamu wote ni sawa, isipokuwa tukiamini kuwa uhakika wa binaadamu umejengeka kwa vitu viwili tofauti

navyo ni mwili wake, na roho, vitu ambavyo vipo sawa kwa watu wote. Haiwezekani kwa madhehebu yoyote yasiyoamini ila mwili tu kumwona mtu kwa njia hii.

5- Kudhihirisha upeo wa hatari za Ukanamungu katika jamii, na athari zinazotokana nao, kama vile, viwango vya juu vya uhalifu, na kueneza machafuko.

6- Kudhihirisha upeo wa hatari za Ukanamungu, na kuwa hauwezi kujenga ustaarabu kwa kutoa dalili ya kihistoria inayothibitisha kuwa hakuna ustaarabu ulioishi karne kadhaa isipokuwa ulikuwa umejengwa juu ya mhimili wa Imani.

7- Lazima kuwepo juhudi za makusudi za kitamaduni zinazojaza mwanya wa kiutamaduni kwa vijana, na kuwajulisha viongozi wa utamaduni katika jamii zetu, na mafanikio yao. Hii itakuwa kinga kwao kutokana na mvuto wa tamaduni nyingine, zikiwa nzuri au mbaya.

8- Lazima jamii ijitahidi kujenga mfumo wake maalumu wa maadili na kuulinda kwa nji ya kuwalea watu wake kuukubali, na kuurithisha kwa kizazi hadi kizazi. Mfumo huo ni lazima uwe kamili, wenye uwiano, na uwezo kuwajengea kinga dhidi ya mikondo iliyopotoka.

**Familia na jukumu lake katika kuwalea Watoto:**

Kipindi cha Utoto ndicho kipindi kilicho muhimu zaidi katika malezi ya binaadamu. Kwa maana hiyo, mtoto asipojaliwa tangu mwanzoni mwa maisha yake, aghalabu hukua huku akipotoka kimaadili na ada za jamii yake, na huwa mpotovu, mwenye kutenda maovu, mwovu na aliye mbali na mwenendo ulio sawa. Kwa hivyo, jukumu la kimsingi katika kipindi hikii lipo kwa familiya ambayo ndiyo imetwishwa mzigo huu ulio muhimu zaidi katika kuwalea watoto. Watoto wanapokea ustadi na maarifa ya awali katika familiya. Vilevile, familiya ni mwangalizi wa kwanza wa njia nyingine za kuwalea watoto zinazowaelekeza

na kuwaongoza watoto. Jmbo hili linabainika katika mienendo na utu wao (their personality), ukiwa mzuri au mbaya. Kwa hivyo fungamano la familia na uwezo wa kuwaongoza watoto wao ipasavyo, na kutowaacha wawe mawindo rahisi kwa wale wenye fikira na itikadi potofu au zisizo za kawaida, na kuwapa mifano mizuri, ni miongoni mwa njia zilizo bora zaidi za kuwalinda na Ukanamungu.

Mchakato wa kuwalea Watoto kijamii ni changamoto iliyo kubwa zaidi inayokabili familiya. Kukosea kufanya hivyo husababisha watu kuishi maisha ya shida wakati wote. Wanakosa uwezo wa kuzoea, wanapata tangamano duni, na kuweka vizuizi katika njia ya wengine, na labda husababisha uharibifu wakati mwingine kama inavyotokea katika jamii nyingine. Vita, kama walivyosema wengine, sio ila matokeo ya kushindwa kwa michakato ya kuwalea watoto katika baadhi ya jamii.

Na kwa sababu ya kukosea kuwalea baadhi ya watu, tunawakuta wakitawaliwa na unywaji ulevi

au dawa za kulevya. Aidha, wanaweza wakawa na mitazamo ya kiradikali, au wakawa mashoga, wagonjwa wa maradhi ya kisaikolojia, au wakanamungu. Ziko jamii nyingine ambazo ingawa ni zenye maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia, lakini maradhi ya kijamii yanaenea sana baina ya wanajamii wao kwa sababu ya ukosefu wa malezi ya kijamii katika jamii zao.

**Pili: Kutatua tatizo la udhaifu wa maarifa:**

Taasisi za kielimu zina jukumu muhimu katika kukabili uzushi huu. Lengo la kujenga shule na vyuo kikuu ni kujenga utu ulio sawa na ulionyooka, unaofuata dini, ada, desturi, na mila zisizopinga Sharia na zilizoridhiwa na jamii, kujitahidi kulinda nchi na maendeleo yake, na kulinda akili za vijana kupitia elimu inayofaa.

Hakuna shaka kuwa taasisi za kielimu – zikiwa shule, taasisi, au vyuo vikuu – ni ngome za kukabili uzushi huu wa hatari; uzushi wa Ukanamungu, kwa kuwa unasawiri fikira za binadamu tangu

utotoni. Mtoto anaanza kujifunza mnamo mwaka wa nne wa umri wake, na zamani walisema: kufundisha watoto utotoni ni kama kutia nakshi juu ya jiwe, na baada skuli za Maandalizi huingia katika vipindi mbalimbali vya elimu. Taasisi za kielimu huweza kukabili uzushi huu kupitia mambo yafuatayo:

1- Kuandaa mitaala inayolinda fikra za wanafunzi:

Hakika mitaala na madhumuni yake inayofundishwa kwa wanafunzi katika vipindi mbalimbali vya elimu, wale wanaoitayarisha lazima waangalie kuwa ina madhumuni yanayotengeneza fikra za wanafunzi kitamaduni, na kuhifadhi akida, silika, na maadili yao.

Zaidi ya hayo, lazima ziwepo mada katika shule za upili na sekondari zinazowatayarisha kupinga wimbi jipya la Ukanamungu. Mada hizo ni lazima ziandaliwe na wataalamu wabobezi wanaoweza kujibu masuali yanayoshughulisha wanadamu na kuwahangaisha kwa muda mrefu.

2- Kuandaa walimu wanaoweza kufikiri kwa mujibu wa mambo mapya:

Ikiwa elimu peke yake ndiyo iwezayo kujenga shakhsia sawia iwezayo kupinga mawazo mapotofu, basi inazilizimu taasisi za kielimu kuandaa mwalimu mzingativu aliyejikita katika aina zote za maarifa, awezaye kuwasilisha yaliyomo mitaalani kwa wanafunzi wake kwa njia nyepesi, na vilevile awezaye kukabili mabadiliko na mageuzi ya kisasa, akawafikisha wanafunzi wake kwenye usalama na amani. Mwalimu kama huyu anaweza kuanadaliwa kwa njia zifuatazo:

- Kumpatia stadi za kuamiliana na mambo mapya, na kujibu tuhuma za wakanamungu kupitia kozi za maendeleo ya kibinadamu na nyinginezo.

- Kuwakinga wanafunzi wanaosafiri kwenda nchi za kigeni kusoma na fikira za wale wanaojaribu kuwatilia shaka, ili wasiathirike na mawazo yao, ambayo huenda wakaja kuyafiki-

sha kwa wanafunzi wao hapo baadaye.

- Kumuelimisha mwalimu na kumpa ujuzi wa lazima wa maisha.

- Kutoa nafasi zinazofaa kwa mwalimu kama vile kujishughulisha na kusoma na kufanya utafiti na kutalii yale yote yaliyo mapya katika uwanja wake wa kielimu, na nyanja nyinginezo pia.

Miongoni mwa jukumu la lazima kwa taasisi za kielimu ni kueneza elimu zenye manufaa zinazolingana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah za Mtume wake (SAW), maadili mema, na kuimarisha misingi ya kifikira na kiakida inayobeba maana za wastani na kiasi, kwa sababu taasisi hizo ni sampuli ndogo ya jamii kamili.

Hoja zifuatazo zinaweza kujumuishwa katika jukumu la elimu katika harakati za kukabiliana na Ukanamungu:

1- Kujali sana kiwango cha elimu ili kumpatia mwanafunzi maarifa madhubuti ya kiutam-

buzi yanayomwezesha kukabiliana na hoja za uharibifu kwa ujumla.

2- Kujali sana kumjengea mwanafunzi akili changanuzi, kwa sababu mtindo wa kumhifadhisha mwanafunzi masomo ambayo hayaelewi vyema mantiki yake unaweza ukamzoeza kufuata fikra za wengine tu, na kudhoofisha uhuru wake wa kifikra; jambo linaloweza kumsababisha awe mwepesi wa kuwaathiri vijana na kuwashawishi kwa fikra yoyote hata ikiwa haina thamani yoyote.

3- Mwalimu lazima awe chanzo cha maarifa ya kidini kwa wanafunzi wake, naye ndiye awekaye misingi anayoitumia mwanadamu kujenga maisha yake ya kimaarifa. Msingi ukinyooka, jengo pia litanyooka, na kama ukipotoka, basi jingo pia litapotoka.

4- Mitaala ya kielimu inapaswa kuwa na kiwango muhimu cha maarifa ya kidini yaliyo sahihi na ya wastani ambayo mwanadamu anayahitajia katika dini, akida, ibada, na mwenendo wake.

5- Mitaala ya kidini lazima ihimize Imani, na kujumuisha akili na mawazo kwa upande mmoja, na kumwimarishia hemko ya kidini na ya kiroho kwa upande mwingine.

6- Umoja wa malengo baina ya mitaala ya kidini na ya kielimu ni muhimu sana. Kwa hiyo ndiyo njia sahihi inayotimiza malengo haya yaliyoainishwa hapo kabla bila ya kupingana.

**Tatu: Kuhuisha jukumu la dini katika malezi na uelimishaji:**

Ipo haja ya hali ya juu ya kuipa dini jukumu la kimsingi katika malezi ya jamii na katika mitaala ya elimu na malezi, kwa sababu dini ni njia ya pekee yenye kujibu masuali yanayozuka akilini wakati inapojaribu kumfikia Mola wake, kwa hivyo dini ni mshiriki wa kimsingi katika kukabiliana na Ukanamungu.

Elimu imehusika na kuchungua tabia, mizushi ya ulimwengu, mifumo yake, kanuni zake, na

sehemu zake, bila ya kuchungua asili yake wala sababu ya kuwepo kwake. Lakini falsafa inachungua majibu ya masuali haya ikitumia akili tupu ili kuyafikia majibu haya. Wengine wangefikiri kuwa elimu na falsafa hukidhi mahitaji ya kimwili ya mwanadamu, kiakili, kisaikolojia, na kimaadili. Kwa hivyo hakuna haja ya dini. Lakini kazi ya dini na umuhimu wa jukumu lake viko katika nukta zifuatavyo:

1- Dini ni njia ya pekee ya kumjua Mwenyezi Mungu vyema (Utukufu ni wake), na kujua kanuni za ulimwengu, madhumuni yake, umilele wake, na jinsi mja anavyohusiana na Mola wake.

2- Dini inapanga mwenendo wa mwanadamu na mahusuiano yake na wengine.

3- Dini ndiyo inayokidhi mahitaji ya kiroho ya mtu. Basi likidhoofika jukumu lake hili linabadilishwa na ulaghai na ushirikina.

4- Dini ndiyo inayomsukuma mtu kutafuta elimu, kuamsha akili yake, kujitayarisha kwa yoyote, kuunganisha baina ya upande wa ibada na upande wa elimu. Mwenyezi Mungu amesema: ﴿**Hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake in wanachuoni**﴾ (35:28)

Kwa hivyo, inatupasa kuanza malezi ya msingi wa kidini, na kuendeana na wanafunzi hatua kwa hatua mpaka wafike kiwango kinachowakinga na tuhuma za wakanamungu, na kinachowawezesha kujibu tuhuma zao.

**Zifuatazo ni njia za kuamsha dini kukabiliana na Ukanamungu:**

1- Kuandikwa upya hotuba za kidini.

2- Kuchunguza hotuba mbalimbali za kidini zinazoenea hivi sasa, kwa lengo la kuwahi kujua migogoro, na kuweka mipango ya kuitatua.

3- Kusisitiza kuwa wanachuoni lazima warudie matini na watoe hukumu kutoka kwake. Laz-

ima wajue kuwa kuamua kuwa kitu fulani ni haramu hakujuzu ila kwa mujibu wa matini; Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mwenye haki ya kuhalalisha na kuharamisha, - swala lisilo na matini wazi, wanachuoni wajitahidi kutoa hukumu yake, wala haliachwi wazi kuhalalishwa au kuharamishwa, kama walivyofanya wanachuoni wa ijtihadi katika mambo yasiyo na matini wazi; walikuwa wanasema: Siipendi au hakuna lawama (yaani kufanya lile jambo au kutolifanya), lakini hawasemi: ni haramu, wala ni hahali.

4- Kuchochea kanuni ya kubadilisha Fatwa kwa mujibu wa mabadiliko ya hali zake nne (wakati, mahali, hali, na watu), na kutengeneza upya misingi ya ijtihadi katila kila zama. Watu wa kila zama hawana budi kuwa na ijtihadi mpya inayowafikiana na mabadiliko ya zama zao, na inayotatua matatizo yao.

5- Kuhifadhi mitindo ya Lugha ya Kiarabu na kanuni zake za kueleza matini na kutoa maana

yake, kama hatua ya kwanza ya kutengeneza upya hotuba za kidini.

6- Kushughulikia changamoto zinazotokana na urithi wetu wa kimaarifa, na kutotegemea daima maarifa ya zamani, kwa kubuni mitindo ya kisasa ya kutambulisha elimu, pamoja na kuhifadhi urithi wetu wa kimaarifa kama ni mojawapo ya mfululizo wa jengo la kimaarifa la umma huu.

7- Kusisitiza umuhimu wa Uislamu wa wastani, na kuchekecha mawazo ya kidini ili kuondoa mawazo magumu yanayosababisha uzito, au uzembe unaosababisha kutoshikilia dini wala maadili.

8- Kushughulikia akili na jukumu lake katika kuelewa matini za kidini, mchango wake katika ujenzi wa ulimwengu, au uzowefu wake mbalimbali katika maisha.

9- Kuepuka ushirikina, na kuangalia zaidi kujenga akili za kiuchambuzi, sio akili za ushirikina.

Miongoni mwa mambo yanayoleta Ukanamungu ni kuamini kupita kiasi mizushi isiyo ya kawaida wala asili inayoyashikiliwa na baadhi ya wafuasi wa dini.

Taasisi za kidini zina jukumu lenye athari kubwa katika kukabiliana na uzushi wa Ukanamungu ambalo linaweza kutimizwa kwa kufuatwa njia mbili:

1- Kuwafahamisha watu jinsi ya kuyaelewa makusudio ya Sharia tukufu:

Hakika wasomi wa Umma huu ni watu wake waaminifu waliotimiza ahadi waliyomuahidi Mwenyezi Mungu; baadhi yao wameshakufa, na wengine wanangojea, wamerithi elimu kutoka kwa Manabii, Mtume wetu mlindwa amesema: (Hakika wasomi ni warithi wa Manabii, na hakika Manabii hawakurithisha Dinari wala Dirhamu, lakini walirithisha elimu, basi, anyeichukua, atachukua sehemu tele) (Imetolewa na Abu-Dawud. Kitabu cha Elimu, No. 3641). Kwa hivyo tunasisitiza kuwa

kutafuta elimu, ni wajibu wa kila mwislamu, na kuwa Mwenyezi Mungu huwapandisha daraja na vyeo vya juu waumini na wenye kutafuta elimu, kama ilivyobainishwa katika Qur'ani tukufu kuwa wasomi ni wale wanaomcha Mwenyezo Mungu zaidi katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake in wanachuoni**﴾ (35:28).

Kwa hivyo, jukumu la wanazuoni ni kubwa, na madaraka yao ni yenye shani, kwa kuwa watu wa kawaida wanawaona ni mifano ya juu kwao katika kila jambo. Kwa hivyo inawapasa kujitahidi sana kuwaelezea makusudio ya dini katika Sharia ya Kiislamu, na kuwabainishia pia kuwa dini si panga iliyowekwa juu ya mashingo yao, bali ni nuru inayowatoa kutoka kwenye giza la ujinga, kuwaondolea moto wa ushirikina, na kuwatimizia furaha ya dunia na Akhera. Hii ni kwa kuwa Uislamu ni Sharia ya yule aliyeumba mbingu na ardhi, na ni wajibu ya wanazuoni kuwaelimisha walinganiaji na wahubiri hukumu za mambo ya kisasa yanayozuka upya.

Na ikiwa tunaomba kutengenezwa upya hotuba za kidini tunazofikisha kwa wengine katika zama za utandawazi, ni wajibu wetu zaidi kutengeneza hotuba zinazofikishwa kwetu sisi wenyewe, na wanaolingania watu lazima wawe na kiwango cha elimu na uhodari unaowatayarisha kuwa maimamu wanawaongoza watu.

Wahubiri na watoao mawaidha inawapasa wawe wenye kiwango cha wastani, na kuwalingania watu kutenda mema, kuangalia majirani wao vyema, kutendeana wema, kuwa na ikhlasi katika kazi, na kujitahidi sana kupandisha juu nchi yao.

Ni wajibu wao kuwabainishia wanaowalingania kuwa Uislamu unalingania mtu kutenda mema, unakataza kila la uovu, humnyanyua kwenye cheo cha shani, na humwondolea kila linalosababisha upotovu wa akida, au maradhi mwilini. Mwaminifu ni yule mtu mnyoofu ambaye akilini na moyoni mwake hukutana na Sharia ya Mwenyezi Mungu na silika sawa za kibinadamu,

huishi akifurahia dini yake pamoja na wanadamu, hutendeana na watu kwa wema, na humpendelea ndugu yake yale anayoyapenda kwa nafsi yake mwenyewe.

Ni wajibu wao vilevile kuwabainishia watu yaliyo halali na yaliyo haramu, kuwasaidia kumfikia Mola wao, kuwaelezea kuwa Uislamu ni mfumo wa maisha, Sharia yake ni ya wastani katika kila jambo, hamna kushikilia maoni makali wala ya kupita mipaka, kuhifadhi akili ni miongoni mwa makusudio yake, na kutafakari sana katika viumbe vya Mwenyezi Mungu mbinguni na ardhini, kwa hivyo ameharamisha kila linalomdhuru au kumuweka mbali na lengo aliloumbiwa, na awe mfano wa hayo yote.

A- Kuwafahamisha watu Fiqhi ya vipaumbele na Fiqhi ya ulinganishi:

Hayo yaweza kufanyika kwa kuweka Fiqhi ya Umma katika mkabala wa Fiqhi ya mtu binafsi iliyotawala Fatua na kutoa hukumu kwa karne

nyingi. Misingi ya Fiqhi hii ilikuwa ni ile aliyoiandika Imam Ash-Shatibiy katika kitabu chake "Al-Muwafaqaat", na aliyoiandika Imamu wa Al-Haramain Al-Juwaini katika kitabu chake: "Uokoaji wa Umma kupitia kuondoa dhuluma", na vingine miongoni mwa vitabu vinavyoshughulikia mambo haya.

Ni wajibu wa wanazuoni wa Umma kuwabainishia watu dini sahihi kwa mujibu wa Fiqhi ya Umma. Na Fatwa ya wanazuoni lazima itolewe baada ya kujua ukweli wa mambo na kulinganisha baina yake na matini. Na wanazuoni lazima waangalie hali ya Umma sio hali ya mtu, kwa kuwa wengi wa vijana waliopotoka na dini, waliiacha kwa jumla kwa sababu ya Fatwa ngumu zisizo za kawaida, na ambazo haziangalii makusudio ya Sharia nyoofu.

Nne: Kuamsha jukumu la watu kakabiliana na Ukanamungu:

Watu wana jukumu muhimu lisilopungua jukumu la vyama na taasisi katika kukabiliana na

Ukanamungu. Jukumu hili linawakilishwa katika mielekeo miwili: Wa kwanza: Kujilinda na kuanguka katika mtego wa uzushi huu. Wa pili: Kuwalingania watu kwa Mwenyezi Mungu kwa hekima na mawaidha mema, ili wampende Muumba wao, na kulinda mawazo na itikadi yao; kisha dini yao.

1- Kujilinda mtu mwenyewe asianguke katika Ukanamungu:

Ikiwa watu kwa jumla na waislamu hasa wanajitahidi sana katika maisha yao kutimiza furaha na starehe zao, na kunyanyua kiwango cha pande zote za maisha yao ya kidunia, basi wanaitwa wakati uleule kujilinda na kuwalinda watoto wao dhidi ya mikondo ya kigeni, hasa ile inayohusika na dini na itikadi, kama vile, mkondo wa kisasa, na kampeni za kuwatenganisha na utamaduni wao (alienation campaigns) na orientalismi zinazomletea mtu shaka katika mambo madhubuti ya dini yake, kukana baadhi ya matini yake tukufu, au kujaribu kuiepusha dini na maisha yake; jambo ambalo linaweza kumvuta kwenye kukana dini.

Ulinzi huu unaweza kutimizwa kwa njia zifuatazo:

A- Ulinzi wa kimwili: Huu unatimizwa kupitia mambo mbalimbali, miongoni mwake ni:

- Kuamsha jukumu la kutoa Zaka:

Ulinzi huu unatimizwa kwa njia ya kuamsha jukumu la kutoa Zaka, na kubainisha kuwa kuna haki nyingine katika mali. Umaskini pamoja na ujinga, na maenezi ya maradhi ni miongoni mwa sababu za udhaifu wa Imani, na unamsukuma mtu kukana uwepo wa Muumbaji, na kumkataa. Kwa hivyo si ajabu kumwona Nabii wetu (SAW) akimwomba Mola wake asubuhi na jioni amkinge na ukafiri na umaskini.

Kutokuwepo kwa nguzo ya Zaka na kutoangaliwa na waislamu wengi kumechangia kueneza umaskini, ujinga, na maradhi, nayo ni nguzo inayounda mshikamano wa kijamii kati ya watu. Zaka imewajibika kutimiza mshikamano wa kijamii kati

ya watu, na Mwenyezi Mungu ameijaalia kuwa ni mojawapo ya nguzo za dini kwa sababu ya umuhimu wake katika kukinga utulivu na starehe za jamii.

Utoaji wa Zaka umeainishwa na Mwenyezi Mungu katika Kauli yake: ﴿**Hakika Sadaka ni kwa mafukara, na maskini, na wanaozitumikia, na wanaotiwa nguvu nyoyoni mwao, na kuwakomboa watumwa, na wenye deni, na katika njia ya Mwenyezi Mungu, na wasafiri walioharibikiwa. (Sadaka hizi) ni faradhi itokayo kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye elimu, Mwenye hekima**﴾ (9:60), nao ni namna nane za watu; ya kwanza ni mafukara na maskini, nao ni wale wasiopata kinachowatosheleza, mbali na kuishi vyema. Waislamu hapo ni lazima wawape kutoka kwenye mali za Zaka inayowatosheleza na kulinda maisha yao, na kuwaepusha na udhalilifu wa uombaji, na hivyo, huwahifadhia dini yao na kuwakinga na wale wanaotumia ufukara wao kwa kuwaelekeza huko na huko.

Hakuna shaka kuwa Uislamu ulipokuja ulielekeza uangalifu wake wa kwanza kwenye wale watu wenye haja, na uliwajaalia sehemu kubwa zaidi katika mali za Zaka hasa, na katika mali ya taifa kwa ujumla. Mwelekeo huu bora wa kijamii ni mchango mkubwa katika uwanja wa kifedha. Mpango huu wa ushuru na matumizi ya serikali haukujulikana kwa binadamu ila baada ya karne nyingi.

- Kutoa (mali) katika mipaka ya Sharia:

Heshima ya Uislamu kwa uhuru wa mtu binafsi wa kumiliki, haimaanishi kuwa mtu ni huru kutumia mali yake atakavyo, lakini matumizi ya mali imewekewa mipaka katika Sharia. Kwa hivyo, kama mtu atakusanya mali kwa njia ya halali, inampasa kuitumia kwa njia ya halali pia, kwa kuwa "Matumizi na ukuzaji wa mali ni kazi ya kijamii, Mwenyezi Mungu ameiwajibisha, na akaijaalia miongoni mwa matakwa ya kumuamini Mwenyezi Mungu na Watume wake", Mwenyezi

Mungu amesema: ﴿**Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na toeni katika yale aliyokujaalieni kuwa waangalizi wake**﴾ (57:7). Al-Fakhr Ar-Razi anasema: "Mafukara ni watoto wa Mwenyezi Mungu, na matajiri ni wenye hazina za Mwenyezi Mungu, kwa kuwa mali iliyoko mikononi mwao ni mali yake, na Asingeliitupa mikononi mwao, wasingalimiliki hata chembe kutoka kwake ……. Si mbali na akili kuwa Mwenyezi Mungu angemwambia mwenye hazina yake: Toa sehemu kutoka kwa yaliyomo katika ile hazina kwa wenye haja miongoni mwa waja wangu".

Hivyo, ulitubainikia upande mmoja wa kazi ya kijamii ya mali katika Sharia, nao ni kuitumia katika njia ya maslahi kwa jumla. Basi, uangalizi – kama ilivyopita – unamlazimu mwangalizi atii amri ya Mwenye mali na kuitoa katika njia zilizoainishwa, lakini kuitoa katika njia nyingine ni dhuluma na ujeuri, vilevile, Imani inawajibisha kumtii Mwenyezi Mungu kama alivyotaka.

Kutokana na mwelekeo huu, tumeona kuwa Sunnah tukufu inaamua kuwa: "Iko haki nyingine katika mali pamoja na Zaka", nayo ni haki ya jamii katika mali ya mtu binafsi, hasa wakati wa dharura ambapo hatari inaizunguka nchi, au kutokuwa na pesa nyumba fulani, yanapotokea maafa, au watu wanapokabili namna yoyote ya majanga.

Al-Qurtubi anasema: "wanazuoni wamewafikiana kuwa Waislamu wakipatwa na shida baada ya kutoa Zaka, inawapasa kutoa tena mali kwa ajili yao. Imam Malik (Mungu amrehemu) amesema: Inawapasa watu kufidia mateka yao hata wakitumia mali zao zote, wanazuoni wote wameafikikana na hilo".

**B- Ulinzi wa kiutamaduni:**

Nao hutimizwa kwa kuoma Qur'ani na Sunnah, kuzihifadhi moyoni, kuzifahamu, na kuzizingatia. Hakika huo ni ulinzi unaolinda vijana wasianguke katika hatari, na kukinga ni bora kuliko kutibu. Vilevile, kila mtu binafsi lazima atafute elimu safi ya

kisharia kutoka kwa wanazuoni wakuu, na kujali sana kujiimarisha kielimu ili aweze kujadili kindani mawazo ya kiakida na kifikra za kikale na za kisasa, na kuelewa kindani maswala ya kifalsafa na asili za mawazo kwa kuzichungua nyanja hizi vyema.

Watu wenyewe lazima wajue vyema walimu wao, na kutembelea vituo maalumu vilivyoidhinishwa kufuatilia maoni yasiyo ya kawaida na yaliyopotoka yanayotangazwa katika tovuti (saiti) za mitandao, na maandishi mbalimbali na kuyajibu kwa lengo la kujikinga nazo ili wengine wasianguke katika mitego ya mawazo haribifu.

Vilevile, lazima waimarishe mahusiano yao na vituo vinavyojishughulisha na pande za miujiza ya kielimu katika Qur'ani na Sunah tukufu, na kuzikamilisha kwa tafiti za kukabiliana na Ukanamungu, ili sura sahihi ikamilike akilini mwa wanaojali uwanja huu, pamoja na kuzitilia hamu tafiti za "Dalili za Utume", ambazo ni sehemu ya miujiza

inayokuza Imani na yakini ya usahihi wa Utume wa Nabii Muhammd (SAW). Mambo haya humkinga mtu asiathirike na mawazo ya wakanamungu, pamoja na mbinu nyingine zinazowalindia watu dini yao na kuwakinga na kampeni zinazojitahidi kubomoa dini kwanza, kisha kumbomoa mtu mwenyewe baadaye.

Umuhimu wa kuwalingania watu kwa Mwenyezi Mungu kwa hekima na mawaidha mema:

Kuwalingania watu kwa Mwenyezi Mungu ni muhimu, bali ni wajibu, kwa kuwa ni kuelimisha na kulea, na furaha ya dunia na Akhera inakutegemea. Mwenyezi Mungu alimwamrisha Mtume wake kwake, akasema: ﴿**Ulinganie katika njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mema**} (16:125), na aliwaamrisha waumini pia kwake akasema: ﴿**Na uwe kutokana na nyinyi umma unaolingania heri na kuamrisha mema na kukataza maovu**﴾ (3:104)

Mtume wetu vilevile alituamrisha kwa kusema: ﴿**Mfikishe kwa niaba yangu japo Aya moja" Baada**

**ya kuamrisha kulingania Uislamu, aliwapendezesha watu kufanya hivyo sana. Ikawa hadhi ya Umma na alama ya heri yake akasema Mwenyezi Mungu: ﴿Nyinyi mmwekuwa umma ulio baora Zaidi uliotolewa kwa watu; mkiamrisha mema na kukataza maovu﴾** (3:110).

Na Uislamu ulionya tusiwe na uzembe na ulegevu katika kulingania, na aliwadharau watu kwa hivyo. Akasema (Utukufu ni wake): **﴿Waliokufuru miongoni mwa Wana wa Israili wamelaaniwa kwa ulimi wa Daudi na 'Isa bin Mariyamu, hayo ni kwa sababu waliasi na walikuwa wanavuka mipaka * Walikuwa hawakatazani mabaya waliyoyafanya. Hakika yale waliokuwa wakiyafanya ni mabaya yaliyoje﴾** (5:78-79).

Katika Utafiti huu "kumlingania Mwenyezi Mungu" kunamaanisha kuwa: Ni kila wito unaolenga kuwajulisha watu Muumba wao, kuwakaribisha kwake, kuwajulisha hukumu za Sharia yake nyoofu, na hivyo inajumuisha pia: wito wa kusomesha Qur'ani tukufu, kueleza hukumu

zake, kuifasiri, elimu zilizotoka kwake, hotuba, na masomo ya elimu ya kisharia, yakiwa ni semina, mihadhara, jioni za kidini, na kadhalika.

Pia inajumuisha mambo yanayohusu Sunnah tukufu na elimu zake, na mengineyo kama vile, Akida. Sharia, Maadili, Ibada, Mu'amala. Qur'ani na Sunnah zinatokana na chanzo kimoja.

Wito kwa heri unaelekezwa kwa kila mtu na kutoka kwa kila mtu, lakini lazima uwe kwa hekima na mawaidha mema, na anayeitwa lazima aone katika mwitaji mfano wa vitendo wa wito wake, kupitia mwenendo na matendo yake, kwa kuwa watu wanaamini utu wa mwitaji kabla ya kuamini ujumbe na wito wake.

Ulinganiaji unayokusudiwa hapa ni kuwaita watu kwenye maadili mema, kuwa mbali na machafu na kila linalopunguza utu wa mtu na cheo chake kizuri alichomuumba Mwenyezi Mungu kwacho. Lakini wito kwa maana yake hasa ni kuwafundisha watu mfumo wa dini yao na ku-

wasaidia kumfikia Mola wao kupitia elimu ya kisharia. Hakuna shaka kuwa mambo haya yanahitaji wanazuoni wabobezi, ili wasije wakaingia uwanja huu wasio na elimu, na hapo madhara yake yatakuwa makubwa sana kuliko manufaa yake.

Wito kwa Mwenyezi Mungu, bila shaka ni ngome na boma lenye nguvu ambapo mashambulio na kampeni za Ukanamungu hushindwa kupenya, kwa sababu unawasaidia watu kumfikia Muumba wao, kuwapa matumaini juu ya mwisho wao, na kuwatimizia furaha ya dunia kwa kuridhika na hatima yao kutokana na Imani yao thabiti waliyonayo. Vilevile unawatimizia furaha ya milele ya Akhera kutokana na kumtii Mola wao, na kujiepusha na kila linalomghadhibisha. Zaidi ya hayo, unawalinda watu na jamii ili wasishikwe na uzushi muovu, yaani uzushi wa Ukanamungu ambao ukienea utakomesha kila jambo lenye manufaa kwa watu, na kubomoa ujenzi wa mataifa.

Njia za kutatua tatizo la ukanamungu

Kutatua suala la ukanamungu ni sehemu ya kujikinga nao, ikiwa kwa kujaribu kumrudisha aliyegeukia ukanamungu kwenye Imani, au kwa kukabiliana na walinganiaji ukanamungu kwa kujibu tuhuma zao. Watu hawa wanaingiza mawazo yao akilini mwa jamii, kwa hivyo, kukabiliana nao ni sehemu ya kukinga wengine wasianguke katika ukanamungu na shaka.

Tunaweza kukabiliana na uzushi wa ukanamungu kupitia njia zifuatazo:

**Kwanza:** Jukumu la taasisi za kidini.

**Pili:** Jukumu la taasisi za utamaduni na kuelimisha.

Tatu: Jukumu la mitandao ya kijamii.

Nne: Kufuata mbinu ya mazungumzo na kushawishi, na jukumu lake katika kujibu tuhuma za ukanamungu.

**Kwanza: Jukumu la taasisi za kidini:**

Hakuna shaka ya kuwa taasisi za kidini zina jukumu muhimu katika kukabiliana na uzushi

wa ukanamungu, kwa sababu zina cheo kikubwa moyoni mwa watu, na taathiri yake kupitia mawasiliano moja kwa moja nao kupitia hotuba, masomo, mihadhara, vitabu, semina, na mikutano inayofanywa kusahihisha maoni potofu, kueneza utambulizi, kukabili misimamo mikali, kubainisha makusudio ya Sharia za mbinguni na kufafanua kuwa hazipingani na silika sawa, Mwenyezi Mungu anasema: ﴿**Ndiyo silika Mwenyezi Mungu aliyowaumba watu; hakuna mabadiliko katika (silika ya) viumbe vya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo dini iliyonyooka, lakini wengi wa watu hawajui**﴾ (30:30).

Na hakuna shaka kuwa Sharia za mbinguni zimeafikiana juu yaliyo heri kwa binadamu, na yanayowaletea usalama wa nafsi, mali, na heshima, pamoja na maadili ya uadilifu, usawa, kusema kweli, uaminifu, upole, msmaha, kuhifadhi ahadi, kurudisha amana, kuwasiliana na ukoo, kuangalia haki za majirani, kuwatii wazazi, kuhifadhi mali za yatima, kutafuta yaliyo heri kwa watu na nchi,

kwa kuwa “panapokuwepo masilahi, ipo Sharia ya Mwenyezi Mungu”, nayo ni misingi ya ujumla ya kibinadamu ambayo Sharia za mbinguni hazikutofuatiana juu yake, wala hayakufutwa katika Sharia yoyote miongoni yake.

Kwa kuzingatia mashambulio yanayoyakabili nchi zetu kupitia vita vya kizazi cha nne vinavyolenga kurarua jamii na kuzipasua pande zote za maadili kwa njia mbalimbali: ugaidi, ukanamungu, na kusababisha matatizo ya kikabila au ya kijinsia. Ukanamungu ulielekezwa kisiasa na kimali kwa kusudi la kueneza fujo na misukosuko, hakuna anayekana juhudi wazi zinazofanya taasisi za kidini kusahihisha fikira potofu nyingi, kutengeneza upya hotuba za kidini na kuzirudisha baada ya kunyakuliwa kwa miongo kadhaa. Tunasisitizia umuhimu wa kuunganisha juhudi na kuzipanga vyema, kutoa juhudi na kazi zaidi kwa pamoja kutatua mizushi mibaya yote, na kuimarisha maana na maadili mema.

Mduara wa mpango huu lazima upanue kujumuisha wizara, jumuia, taasisi zote za Kiarabu na Kiislamu zinazoshughulika na fikira na ujenzi wa watu kukabiliana na changamoto hizi zote.

Haya yote yanahitaji wenye akili, wenye hekima wa Umma, wapendao nchi yao, wenye ushupavu wa dini na nchi zao waangalie vitimbi hivi vyote visivyosaidia ila maadui wa taifa na vikosi vya ubeberu katika nchi zetu wa Kiarabu, neema zake, na uwezo wake wa kiuchumi na kijiografia. Hivyo, inatuhimiza kusimama pamoja kama tukiwa mtu mmoja mbele ya changamoto hizi zote, na kujitahidi tukishikilia msingi wa kiimani na kitaifa, kukubaliana na ukanamungu na kujibu tuhuma za wakanamungu.

Kati ya juhudi za wizara ya Waqfu ya Misri kukabiliana na uzushi wa ukanamungu, tunataja zifuatazo:

1- Kufanya kazi kupitia hotuba, masomo, semina, makala na hotuba za vyombo vya habari, ma-

zungumzo ya wanahabari, misafara ya kulinganía, kozi za mafunzo, kufungua shule za kisayansi na za Korani kuimarisha hali ya imani, na kuwalinda vijana na hatari ya fikira za ukanamungu.

2- Kutolea kozi za mafunzo kwa maimamu wapya juu ya "mbinu za ukanamungu, na ujuzi wa mawasiliano na mazungumzo".

3- Uanzishaji wa mikutano ya Waqfu ya Utamaduni, chini ya kichwa "Ukanamungu, sababu zake na hatari zake, Je! Ni jambo la kudumu au linaloisha upesi?"

4- Kuanzisha "Jukwaa la Mawazo la Kiislamu" chini ya kichwa: "Kati ya uradikali na ukanamungu".

5- Kupanga semina kadhaa na mihadhara mikubwa ya kielimu chini ya kichwa: "Hatari ya ukanamungu na Njia za Kuukabili".

6- Kushirikiana na Wizara ya Vijana na Michezo

katika mpango wa "Hivyo, kwa akili" kwa mazungumzo yanayolenga shabaha maalumu na kukanusha tuhuma za wakanamungu kwa hoja na ushahidi.

Pili: Jukumu la taasisi za utamaduni na kuelimisha:

Taasisi hizi zina athari kubwa moyoni mwa watu, na hakuna shaka kuwa kutatua uzushi wa ukanamungu na kuukabili – kwa upande wa utamaduni na kuelimisha – ni madaraka ya waandishi, wenyefasaha, wenyefikira na walimu. Pia ni jukumu la watu wa sanaa na ukumbi wa michezo, na waandishi wa riwaya na sanaa nzuri (fine arts) na wengineo ambao wana mchango mkubwa katika uwanja huu, kwa kuwa wana wafuasi wengi wanaoathirika na kazi zao. Wajibu wa hao ni kubwa sana, maana ni wajibu wao watoe kila linalosidia dini, akida, na nchi yao. Pia ni jukumu lao kukabili mashambulio mabaya yanayolenga akida, kwa kusudi la kuwakinga vijana na kampeni za kigeni,

hasa vile vitendo vinavyovamia nyumba zetu katika enzi hii ya mbinguni wazi (open skies), na ambavyo baadhi yake huelezea tamaduni na maadili tofauti ambayo yanaweza kupunguza thamani na hadhi ya dini na kuikana.

Jukumu la fasihi – mashairi, maandishi, na sanii – halikaniki katika kukabiliana na uzushi wa ukanamungu. Sanii zina athari kubwa rohoni mwa wadogo na wakubwa, fasihi, ukumbi wa michezo, sanaa, riwaya, hadithi fupi na sanii zingine nzuri, pamoja na njia zingine, zinaweza kuwa ukuta wa kujizuia dhidi ya maoni potofu ya kigeni na ya ndani.

Vilevile, jukumu la elimu, wanachuoni, na waandishi wa mitaala ni kubwa zaidi katika kuamsha utambuzi wa kielimu na kiuchunguzi katika jamii juu ya misingi yenye mitindo madhubuti. Hivyo, jukumu hili linawezesha mtu kufahamu zama yake na mafinikio yake, na kushiriki katika utengenezaji wa matukio yake na ustaarabu wake

wa kisasa, bila ya kushikwa na taathira zinazomtupa nyuma, wala kukata tamaa kuwa na utu na dhati ya kistaarabu.

Kwa hivyo, inwapasa wenye madaraka ya utamaduni na kuelimisha washirikiane na taasisi za kidini na mitandao kulinda jamii yetu kwa jumla na vijana hasa wasivutwe na fikira hizi potofu na itikadi batili zinazoleta hasara kubwa. Pia lazima wawasilishe madhumuni ambayo hukinga akida, kutetea dini, na kuisaidia nchi.

Tatu: Jukumu la mitandao ya kijamii:

Hakuna akanaye kuwa mitandao ya kijamii zina uchawi unaoathiri nafsi, akili na nyoyo za watu. Tumeshasikia, kuona na kuangalia kuwa media zinaathiri vikundi mbalimbali vya watu, wakiwa wakubwa au wadogo. Pia tukawa na yakini kuwa zinaweza kuwa sababu ya kuwanyanyua watu na kuwadunisha wengine kupitia vyombo vyake maarufu  vinavyosomwa, vinayosikilizwa, au vinavyoangaliwa.

Ikiwa katika uchunguzi wetu wa sababu za kuenena kwa uzushi wa ukanamungu tunakiri kuwa vyombo vya taifa na taasisi zake mbalimbali zina jukumu muhimu sana katika kukabiliana na uzushi huu, kweli mitandao ya kijamii ni mojawapo ya vyombo hivi.

Mitandao ya kijamii ina jukumu katika kueneza fadhila kupitia mialiko kwa kuelewa dini kwa njia sahihi inayolingana na roho na mahitaji ya wakati wa kisasa, na kubainisha umuhimu wake kutimiza furaha ya watu na utulivu wa jamii.

Mitandao ya kijamii mbalimbali inaweza kukumbatia kampeni kwa kuamsha utambuzi wa vijana na hatari za ukanamungu juu ya watu na jamii. Maana ulisukuma watu kadhaa kujiua na kukomesha maisha yao walipowahi kujua kuwa kuwepo kwao hakuna maana, na kuwa maisha yao hayana thamani, kwa hivyo walikimbilia mauti bila ya hofu. Watu kama hao wanajitahidi kubomoa jamii zao na kuziangamiza badala ya kuzihifadhi na kuzifurahisha.

Kati ya juhudi za kampeni hii ni kuamsha utambuzi wa watu kwa umuhimi wa kuelewa makusudio ya dini, na kuwa dini ni Sharia ya Mwenyezi Mungu iliyokuja kutimiza faraha yao duniani, na starehe na mafanikio katika Akhera.

Miongoni mwa mbinu za kueneza fadhila baina ya watu ni kukataza machafu katika jamii, Mwenyezi Mungu anasema: ﴿Hakika wale wanaopenda mambo machafu yaenee miongoni mwa walioaminiwatapata adhabu yenye kuumiza katika dunia na Akhera. Na Mwenyezi Mungu ndiye anajua na nyinyi hamjui (4:19), hiyo ni kwa sababu maenezi ya machafu katika jamii yanaleta ukosefu wa kuamini heri, heshima, na usafi, na kutojizuia na kafanya maovu, ili kuonesha kuwa maovu yameenea humo. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu amewaahidi wale wanaoeneza machafu miongoni mwa waumini kwa adhabu inayoumiza duniani na akhera.

Nne: Kufuata mbinu ya mazungumzo

na kushawishi, na jukumu lake katika kujibu tuhuma za ukanamungu:

Miongoni mwa njia zilizo bora zaidi ni njia ya kuzungumza na kushawishi, na kujibu hoja kwa hoja ili tuweze kutoa ushahidi unaoteketeza madhehebu ya wakanamungu na kubomoa tuhuma zao. Qur'ani tukufu imetumia njia ya kuzungumza kutoa ushahidi juu ya wapinzani, Mwenyezi Mungu amesema: Je! Hukumuona yule aliyehojiana na Ibrahimu kuhusu Mola wake kwa sababu Mwenyezi Mungu alimpa ufalme? Ibrahimu aliposema: Mola wangu ni yule ambaye huhuisha na hufisha, akasema: Mimi pia nahuisha na kufisha, Ibrahimu akasema: Hakika Mwenyezi Mungu hulichomozesha jua mashariki, basi wewe ulichomozeshe magharibi, akaduwaa yule aliyekufuru, na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu (2:258). Pamoja na kujibu tuhuma za kila mtu binafsi, kuna vituo vya ujumla ambavyo lazima vishughulikiwe na mazungumzo; vilivyo muhimu zaidi ni:

Kituo cha kwanza: Kinahusika na swala la chanzo cha ulimwengu na kuwajibia wafuasi wa Darwin, na kuwajibu wale waliosema kuwa ulimwengu ulianzishwa kwa bahati na maendeleo, na kutoa ushahidi juu ya kuwa uliumbwa.

Lazima tufahamu – tunapozungumza na wakanamungu – kuwa wanaanza maswala yao ya msingi - kama kusema kwamba ulimwengu uliibuka binafsi, na kuwa maisha ni uwepo wa uyakinifu, na kuwa akili ya kibinadamu ni matukio ya tabia – wanatolea maswala haya kutokana na mawazo, lakini bila ya elimu; wao wanaamini mawazo haya lakini hawana dalili ya kielimu au ya kifalsafa juu yake.

Jamii ya kielimu kwa ujumla huamini uumbaji. Walisukumwa na nadhariya ya "Ubunifu werevu" kuamini kuwa Mungu yupo, ile nadharia iliyomfanya mkubwa mmoja wa wakanamungu katika karne ya ishirini kukiri kuwa Mungu yupo, naye ni "Antony Flew" aliyekiri mwishoni mwa umri

wake kuwa Mungu yupo, na akaandika kitabu kinachoitwa "Mungu yupo", akasimulia humo kisa chake kutoka ukanamungu hadi Imani.

Kwa mujibu wa haya, kujibu hoja za wakanamungu katika upande huu kutakuwa kwa kutumia maoni ya wale wanachuoni, ambao magunduzi yao ya kisayansi yameleta vidokezo vinavyobomoa mizizi ya nadharia ya ukanamungu. Magunduzi yaliyo muhimu zaidi yaliyomsukuma Antony Flew kusema kuwa Mungu yupo ni:

**Kwanza**: Ulimwengu una mwanzo, na ulianza kutokana na chochote (hiyo waliyothibithisha wanasayansi wa 'Fizika ya quantum').

**Pili:** Tabia inakwenda kwa mujibu wa kanuni thabiti zilizofungamana.

Tatu: Uhai ulianza pamoja na umadhubuti wote uliomo humo, kutokana na mwili usio hai.

**Nne**: Ulimwengu, pamoja na kanuni na vitu vilivyomo humo, unatayarisha hali nzuri zaidi

kwa mtu kupatikana na kuishi ardhini, hiyo inajulikana kwa “msingi wa kibinadamu”.

**Tano:** Uwezo wa juu sana wa akili hauwezi kuwa matokeo moja kwa moja ya shughuli za umeme-kemia (electro-chemical activity) za akili.

Sayansi ya kisasa imewavamia wakanamungu na ukanamungu vibaya, walipothibitisha wanasayansi wa Fizika ya quantum mambo muhimi mawili:

**Kwanza:** Ulimwengu una mwanzo, na sio bila ya mwanzo, na mwanzo wake ni mnamo miaka 13.7 bilioni iliyoopita.

Pili: Ulimwengu ulianza kutokana na chochote, kupitia mlipuko mkubwa (big bang); jambo ambalo linathibitisha hoja za waumini tangu kale na kale.

"Ushahidi wa kilemwengu" Ubunifu werevu:

Ushahidi wa Ubunifu werevu hufanywa kwa mujibu wa tuliyoyasema juu,, nao unategemea

kuwa "umadhubuti wa jengo la ulimwengu pamoja na mpango na mfumo ulioko katika tabia unathibitisha kuwa yuko "Mbuifu mwerevu". Basi ulimwengu na ukubwa, upana, na utofauti wake unaendelea chini ya sheria zinazoendana kwa kawaida na utaratibu. Ule utaratibu ndio unaozipa kanuni za tabia ushahidi wa Muumbaji.

Ushahidi wa "kipindi cha kuachwa":

Wakanamungu huenda wakajaribu kukimbia ukweli huu kwa kusema kuwa ulimwengu na maji na nishati zilizomo humo – ambao umeanza kutokana na chochote kama wanavyosema wanasayansi wa fizika ya kisasa – ulianzi binafsi bila ya kuhitaji muumbaji, na usemi huu ulikanushwa na wanafizika.

Basi majibu yao ni ushahidi wa kifalsafa anayouita Richard Swinburne "Ushahidi wa kipindi cha kuachwa". Richard Swinburne alisema kuwa amepata ushahidi huu kutokana kwa wasomi wa theolojia Waislamu, nao: "Ukiwa wakati wa kikale

ulidumu bila ya mwisho, na ukiwa ulimwengu una mwanzo, basi kwa nini ulimwengu ulianza katika ule wakati ulipoanza? Kwanini haukuachwa kwa muda fulani katika wakati usio na mwisho, kisha ulionekana? Lazima iwe sababu iliyoutokeza".

Kituo cha pili: Kinahusika na jibu la tatizo la shari na uhusiano wake na kitendo cha kiungu.

Swala hili ni miongoni mwa sababu zinazosukuma kwenye ukanamungu, Antony Flew anasema: "Moja ya sababu za mwanzo za kukimbilia kwangu kwa ukanamungu ni hisia yangu ya uovu na maumivu". Tuhuma hii imesababisha watu wengi kuwa wakanamungu, maana jinsi gani Mungu huwepo na kuruhusu maovu haya yote?

Hakika swala la heri na shari halihusiki na kuwepo kwa Mungu, bali na sifa zake. Kwa hivyo, wataalamu Waislamu wa theolojia walijumuisha swala hili katika mazungumzo yao juu ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu kwa ujumla, na katika mazungumzo juu ya vitendo vyake (Utukufu ni

wake), yaani kuwepo kwa maovu, madhambi, na upungufu sio ishara ya kuwa Mungu hayupo.

Hakika, watu wa dini walijibu tuhuma hiyo kwa majibu tofauti, miongoni mwao:

1- Mwanadamu ameumbwa na kupewa uhuru wa hiari na madaraka juu ya matendo yake. Kuwepo kwa shari ni matokeo ya hiari ya binadamu nayo ni balaa kwa binadamu. Basi maumivu yanapompata mtu huweza kuwa matokeo ya dhambi aliyoifanya, na Mwenyezi Mungu anataka kumsafisha nayo, au huweza kuwa yametokana na Mwenyezi Mungu na atamfidia mtu nayo Siku ya Kiyama. Au huweza kuwa yametendwa na mwanadamu kwa mwanadamu mwingine na Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu atamlipiza kisasi yule aliyetenda maovu.

2- Wakanamungu walitegemea katika kukana uwepo wa Mwenyezi Mungu juu ya kuwepo kwa shari na madhambi, kwa kuwa yanaleta

upungufu wa Mungu, hayo hujibiwa kwa dhana tatu za kiakili:

1- Mungu yupo lakini haumbi kitu.

2- Mungu kamili yupo na anaumba ulimwengu mfano wake katika ukamilifu.

Na dhana hizi mbili haziwezekani kabisa.

3- Inabakia dhana ya tatu, nayo ni: Ulimwengu wetu huu pamoja na pungufu na maumivu yaliyomo humo. Ugumu wa kufikiria dhana hii ni chache kuliko kufikiria dhana mbili za kwanza.

Kueleza hayo tunasema: "Mungu Muweza asiyeumba chochote, kama ilivyo hali ya dhana ya kwanza, ni upungufu usioweza kupatikana kisemi wala kififikiri, kwa kuwa Uweza hauna maana ila kuweza katenda lolote, pia ukamilifu kabisa ambao huumba ukamilifu mfano wake, kama ilivyo hali ya dhana ya pili, pia ni upungufu usioweza kupatikana kisemi wala kifikiri, kwa kuwa ukamilifu

kabisa ni sifa ya pekee isiyokubali mipaka, haina mwanzo wala mwisho, wala haina nafasi kwa iliyo kamili wala iliyo kamili zaidi. Ni jambo la msingi kuwa Muumbaji ni kamili zaidi kuliko kiumbe, na kwamba kiumbe lazima kiwe na upungufu ambao Muumbaji lazima kuachana nao. Maana yake, uwepo wa uovu ulimwenguni haupingani na ubora wa ukamilifu na uwezo wa kiungu, na bila shaka dhana hii ni karibu zaidi kwa akili kuliko dhana mbili nyingine".

Antony Flew anaeleza yaliyomshawishi kuhusu swala la shari akisema: "Shari ni namna mbili, namna inayotokea kwa mwanadamu, na hurejeshwa kwa mapungufu yaliyoko katika nafsi ya binadamu, maana Mungu aliacha jamii kwa matendo ya binadamu, maana Mungu aliacha jamii kwa matendo na hiari ya binadamu ambaye wakati mwingi humfanyia ndugu yake madhara, udhia na maumivu. Kwa upande mwingine, iko shari ambayo mtu hana madaraka nayo, kama vile, mitetemeko ya ardhi, mafuriko na magon-

jwa. Nimeweza kufahamu kutokea kwa shari hizi katika mfumo wa Mungu wa hari, kupitia maelezo kadhaa:

1- Maumbile hayo yana sheria zinazoruhusu matetemeko ya ardhi, vimbunga na majanga mengine kutokea. Wakati huo huo, maumbile hayawezi kuachwa bila sheria hizi. Yakiachwa, yatakuwa chini ya machafuko na fujo. Yaani, tunaishi chini ya sababu na athari za sheria hizi.

2- Changamoto hizi za asili humwongoza mwanadamu kufanya bidii kukabiliana nazo, jambo lililosababisha maendeleo ya vitu na maendeleo ya ustaarabu yanayoonekana wazi.

3- Uzoefu wa wanadamu wa dhiki na majaribio haya husababisha maendeleo ya kiroho na ya kimaadili ambayo tunahisi wakati tunapokabiliwa na shida.

4- Hakuna shaka kuwa mtazamo wa dini katika maisha baada ya kifo, na malipo anayoyapata

mtu Akhera kwa kusubiria balaa ni maelezo kamili ya tatizo la shari na maumivu.

Kutegemea yaliyotajwa juu, tunasisitiza mambo mawili:

Kwanza: Maendeleo si badala ya Mungu. Maendeleo kama nadharia yanaweza kueleza baadhi ya maswala ya kisayansi, lakini hayawezi kueleza makusudio ya ulimwengu na uhai, na vipi uhai ulianza kutokana na kitu kisicho hai, na jinsi yanavyoeleza utambuzi na fikira na vinginevyo. Kwa hivyo, mweka nadharia ya maendeleo mwenyewe, aliyutuhumiwa kwa ukanamungu, hakuweza chochote mbele ya haya, kwa hivyo, alitaja katika bibliografia yake kuwa anaamini kuwa Mungu yupo. Akasema: "Akili inaniambia: Ni ngumu sana bali ni muhali kutambua ulimwengu huu mkubwa na mzuri, pamoja na mwanadamu awezaye kuangalia zama za kale sana, na kwenda kwa akili yake kuzingatia wakati mbali ujao, kisha inaniambia kuwa ulimwengu huu uliumbwa kwa bahati potofu, au kwa lazima. Ninapozingatia

haya najiona nililazimishwa kukubali sababu ya kwanza ambayo ina akili hodari inayofanana, kwa kiasi fulani, na mtu, hapo ninastahiki kusifiwa kama muamini wa Umoja".

Pia, wengi wa wale wanaokumbatia nadharia ya maendeleo waliipa nafasi kwa dini na kwa kusema kuwa Mungu yupo, kama vile, Herbert Spenser, anaposema: "Ni muhali kufikiri kuwa maarifa yetu hayana madhumuni pasi na yanayoonekana, bila ya kufikiri wakati ule ule kuwa kuna kitu ambacho maonekano hayo yanakiwakilisha. Hakika sisi tunapofikiria kitu kinachoisha, tunafikiria kitu chenyewe na mwisho wake, lakini tunapofikiria kitu kisichoisha, tunakana mwisho, lakini hatukani kitu chenyewe".

**Pili:** Hakika wanathelojia Waislamu na juhudi zao kujibu tuhuma na kuthibitisha Imani kwa kutumia akili wana athari kubwa. Dalili zao walizounda husaidia wakanamungu mpaka sasa kutoka shaka kwenda yakini. Haya huonesha nguvu

ya akili zao na ufahamu wao. Tukilingania dalili za wale wanathelojia na zile alizozitaja Antony Flew, na tukiona mlingano baina ya dalili hizi, basi inamaanisha kuwa dalili ya Ubunifu werevu ni dalili ya uhodari walioitumia wanathelojia Waaislamu kuthibitisha kuwa Muumbaji yupo, na kuwa ni Mwenye elimu, Mwenye uweza.

Ama kuhusu ushahidi wa "kipindi cha kuachwa" uliochukuliwa na wanathelojia Waislamu, hakuna kitabu hata kimoja cha theolojia ya Kiislamu ambacho hakiutaji, nao "haiwezekani kuainisha wakati ambapo ulimwengu ulipatikana bila ya sababu hasa, ijapokuwa nyakati zote ni sawa kuuanzisha (yaani ungeweza kuanzishwa wakati wowote)" . Kusudio la misemo ya wanatheolojia, hata ikitofautiana juu ya ushahidi huu, ni kusema: "Iliyopatikana baada ya kuwa haiko, na ilipatikana katika wakati halisi au wakati uliokadiriwa ni moja ya vitu viwili: Kitu ambacho ni lazima kupatikna katika wakati maalumu, au ambacho inajuzu kupatikna katika wakati maalumu. Basi

mtu akikadiria kuwa kupatikana kwake wakati maalumu ni jambo la lazima, kadirio lake ni batili kwa pande mbalimbali: Mmoja: Ikiwa kupatikana kwake wakati maalumu ni lazima, basi, kwanini kitu hiki hasa kimewajibika kupatikana pasi na vitu vilivyo sawa nacho! Vitu vilivyo sawa ni sawa katika hali zote, yaani ikiwa kupatikana kwa kitu kimoja katika wakati maalumu ni lazima, basi kupatikana kwa vitu vingine vyote vilivyo sawa nacho, hamna budi kuwa ni lazima kupatikana pia wakati ule ule; vyote lazima vipatikane wakati mmoja. Inayoeleza hayo: Uwajibu wa kupatikana kwa kitu fulani katika wakati maalumu ni sawa na kupatikana kwake katika wakati ulio kabla au baada ya ule wakati, yaani nyakati zote ni sawa, na sababu ya kudai kuwa kupatikana kwake katika wakati maalumu ni lazima, ni sawa na kudai kuwa kupatikana kwake katika wakati mwingine ni lazima".

Pia, hoja aliyoitegemea "Abraham Verges", aliyeandika hatima ya kitabu cha "Mungu yupo"

kujibu tuhuma za wakanamungu zinazosema: "Ikiwa Mungu ameumba ulimwengu, basi nani aliyeumba Mungu? " kuwa hiyo ni dhidi ya mantiki, kwa kuwa inaleta mfululizo ulio ni muhali kiakili, nayo ni dalili ile ile walioitegemea wanatheolojia na wanafalsafa waliothibitisha kuwa Mungu yupo.

Dhana ya Antony Flew juu ya Mungu inaafikiana na misemo ya wanatheolojia waislamu, maana Mungu asiye mwili na aliye nje ya mipaka ya wakati na mahali; walipinga kumweka Mungu chini ya mipaka ya wakati au mahali, basi haiwezi kusema: Mungu yupo nje ya ulimwengu au ndani yake.

Muktadha hapa sio kurekodi nafasi ya ukuu au ukubwa wa wanatheolojia wa Kiisilamu juu ya wanatheolojia wa Magharibi, ijapokuwa ni wanafunzi wao kikweli, lakini ni kuwapa wasomi waislamu haki zao, na kuashiria juhudi zao kubwa katika uwanja huu, ambazo zinaendelea kuwa na athari katika kukabiliana na mikondo mikali, kielimu na kiitikadi.

Hatimaye, lazima tuseme kuwa akida ya kukana mungu kwa wakanamungu si ya lazima, kwa hivyo "Richard Dawkins" katika kitabu chake "Udangayifu wa Mungu" ("The God Delusion") aliandika sura kwa kichwa cha: ﴿**Kwa nini kuna uwezekano mkubwa kwamba hakuna Mungu". Huu ni utapeli mkubwa na uharibifu wa nadharia na maoni ya ukanamungu, kwa sababu mkanamungu ndiye anayepata hasara zaidi ikiwa uwezekano dhaifu - kwa maoni yake – wa uwepo wa Mungu utatimizwa. Lakini muumini hatapotea chochote; Qur'ani tukufu ilitaja hoja hii kwa ulimi wa mwaminifu wa watu wa Firauni: Na mtu mmoja mumini katika watu wa Firauni anayeficha imani yake akasema: Mtamuua mtu kwa sababu anasema Mola wangu ni Mwenyezi Mungu? Na yeye amekujieni kwa hoja zilizo wazi kutoka kwa Mola wenu. Na akiwa ni mwongo basi uwongo wake ni juu yake mwenyewe. Na akiwa ni mkweli, yatakupateni baadhi ya hayo anayokuahidini. Hakika Mwenyezi Mungu hamuongozi mwenye kupita kiasi, muongo mkubwa**﴾ (40:28).

# Misamiati na Istilahi

## Kiarabu – Kiingereza - Kiswahili

| Kiswahili | Kiingereza | Kiarabu | |
|---|---|---|---|
| Ubaradhuli | Libertinism | الإباحية | 1 |
| Ukiritimba | Monopoly | احتكار | 2 |
| Takwimu ya kimataifa | International statistics | الإحصاءات الدولية | 3 |
| Uvumbuzi wa kisayansi | Scientific inventions | اختراعات علمية | 4 |
| Dini za mbinguni | Divine religions | أديان سماوية | 5 |
| Dini za kishirikina | Pagan religions | أديان وثنية | 6 |
| Dini za kubuni | Human-made religions | أديان وضعية | 7 |
| Ugaidi | Terrorism | الإرهاب | 8 |
| Sababu za kijamii | Social reasons | أسباب اجتماعية | 9 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Sababu za kiustaarabu | Civilizational reasons | أسباب حضارية | 10 |
| Sababu za kiutambuzi | Cognitive reasons | أسباب معرفية | 11 |
| Sababu za kisaikolojia | Psychological reasons | أسباب نفسية | 12 |
| Kushughulikakisomi na Mashariki | Orientalism | استشراق | 13 |
| Sababu za kiuchumi | Economic reasons | أشباب اقتصادية | 14 |
| Asili ya spishi | Origin of species | أصل الأنواع | 15 |
| Machafuko ya kisaikolojia | Psychological disturbances | اضطرابات نفسية | 16 |
| Ubakaji | Rape | اغتصاب | 17 |
| ukanamungu | Atheism | الإلحاد | 18 |
| Uwazi wa kiutamaduni | Cultural openness | الانفتاح الثقافي | 19 |
| Uzemba | Negligence | إهمال | 20 |
| Kipaumbele | Priority | أولوية | 21 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kiutondoti | In details | بالتفصيل | 22 |
| Ushahidi wa kilimwengu | Universal evidence | البرهان الكوني | 23 |
| Barua pepe | E mail | البريد الالكتروني | 24 |
| Kutengeneza upya | Renewal | تجديد | 25 |
| Mikusanyiko ya kidhahania | Virtual groups | تجمعات افتراضية | 26 |
| Udini | Religiosity | تدين | 27 |
| Urithi wa maarifa | Heritage | التراث | 28 |
| Malezi | Upbringing | تربية | 28 |
| Msimamo mkali | Fanaticism | التشدد | 30 |
| Ubunifu werevu | The intelligent design | التصميم الذكي | 31 |
| Uradikali | Radicalism | التطرف | 32 |
| Kuelimisha | Education | تعليم | 33 |
| Kuchechemua | Activation | تفعيل | 34 |
| Masambaratiko | Disunity | تفكك | 35 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Masambaratiko ya familia | Family disintegration | التفكك الأسري | 36 |
| Makisio ya kiidadi | Quantitative estimation | تقدير كمي | 37 |
| Uzalishaji upya wa roho | Reincarnation | تناسخ الأرواح | 38 |
| Ukuaji | upbringing | تنشئة | 39 |
| Kuangazia | Enlightenment | التنوير | 40 |
| Mapinduzi ya kingono | Sexual revolution | الثورة الجنسية | 41 |
| Harakati za kuangazia | Enlightenment movement | حركات التنوير | 42 |
| Kampeni za utenganishi kitamaduni | Alienation campaigns | حملات التغريب | 43 |
| Hotuba ya kidini | Religious discourse | الخطاب الديني | 44 |
| Udarwini | Darwinism | الداروينية | 45 |
| Dahriya | Time aethiesm | الدهرية | 46 |
| Ndoa ya jinsia moja | Same-sex marriage | الزواج المثلي | 47 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Tuhuma za kifalsafa | Philosophical suspicion | شبهات فلسفية | 48 |
| Tuhuma | Suspicion | شبهة | 49 |
| Shakhsia sawia | Sound personality | شخصية سوية | 50 |
| Ushoga | Homosexuality | شذوذ – مثلية جنسية | 51 |
| Harakati ya kiwatu | Populist movement | الشعوبية | 52 |
| Matashi | Lust/desire | الشهوانية / الشهوة | 53 |
| Mabaraza ya kitamaduni | Cultural saloon | الصالون الثقافي | 54 |
| Mwamko | Renaissance | عصر النهضة | 55 |
| Udunia | Secularism | العلمانية | 56 |
| a vitendo- | Practical | عملي | 57 |
| Mchakato wa kuelimisha | Educational process | العملية التعليمية | 58 |
| Utandawazi | Globalization | عولمة | 59 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kipindi cha kuachwa | The gap period | فترة الترك | 60 |
| Ubinafsi | Individualism | الفردية | 61 |
| Falsafa ya kimaadili | Ethical philosophy | الفلسفة الأخلاقية | 62 |
| Falasafa ya enzi ya kuangazia | Philosophy of the age of enlightenment | فلسفة عصر التنوير | 63 |
| Fizika ya quantum | Quantum physics | فيزياء الكم | 64 |
| Kutojua | Gnosticism | اللاأدرية | 65 |
| Uyakinifu | Materialism | المادية | 66 |
| Ubora | Idealism | المثالية | 67 |
| Blogi | Blog | مدونة | 68 |
| Mkushughulika-kisomi na Mashariki | Orientalist | مستشرق | 69 |
| Makusudio ya kisharia | Purposes of Sharia | مقاصد الشريعة (الكليات الخمس) | 70 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (Tovuti (saiti | Site | موقع على الإنترنت | 71 |
| Kiwango cha moja kwa moja | Direct rate | نسبة طردية | 72 |
| Mfumo wa maumbile | The system of nature | نظام الطبيعة | 73 |
| Mfumo wa kimataifa | The world system | النظام العالمي | 74 |
| Nadhariya ya maendeleo ya mbele au ya upandisho | Evolutionism progression or ascendance | نظرية التطور التقدمي أو التصاعدي | 75 |
| Nadhariya ya kutokea wakati mmoja | Theory of contemporaneous existence | نظرية التعاصر الزمني | 76 |
| Nadhari ya mageuzi na upandisho | Theory of evolution | نظرية النشوء والارتقاء | 77 |
| Nadhariya ya usilika wa umoja na uhalisi wake | Theory of innateness and authenticity of monotheism | نظرية فطرية التوحيد وأصالته | 78 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Isotopu | Version | نظير / نسخة | 79 |
| Ukosoaji | Criticism | نقد | 80 |
| Utapeli | Refutation | نقض | 81 |
| Udhanaishi | Existentialism | الوجودية | 82 |
| Mitandao ya kijamii | Social media | وسائل التواصل الاجتماعي | 83 |

## Misamiati na Istilahi

## Kiswahili – Kiingereza - Kiarabu

| | Kiswahili | Kiingereza | Kiarabu |
|---|---|---|---|
| 1 | a vitendo- | Practical | عملي |
| 2 | Asili ya spishi | Origin of species | أصل الأنواع |
| 3 | Barua pepe | E mail | البريد الالكتروني |
| 4 | Blogi | Blog | مدونة |
| 5 | Dahriya | Time aeth-iesm | الدهرية |
| 6 | Dini za kishiriki-na | Pagan reli-gions | أديان وثنية |
| 7 | Dini za kubuni | Human-made religions | أديان وضعية |
| 8 | Dini za mbin-guni | Divine reli-gions | أديان سماوية |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9 | Falasafa ya enzi ya kuangazia | Philosophy of the age of enlighten-ment | فلسفة عصر التنوير |
| 10 | Falsafa ya kimaadili | Ethical phi-losophy | الفلسفة الأخلاقية |
| 11 | Fizika ya quan-tum | Quantum physics | فيزياء الكم |
| 12 | Harakati ya kiwatu | Populist movement | الشعوبية |
| 13 | Harakati za kuangazia | Enlighten-ment move-ment | حركات التنوير |
| 14 | Hotuba ya kidini | Religious discourse | الخطاب الديني |
| 15 | Isotopu | Version | نظير / نسخة |
| 16 | Kampeni za utenganishi kitamaduni | Alienation campaigns | حملات التغريب |
| 17 | Kipaumbele | Priority | أولوية |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 18 | Kipindi cha kuachwa | The gap period | فترة الترك |
| 19 | Kiutondoti | In details | بالتفصيل |
| 20 | Kiwango cha moja kwa moja | Direct rate | نسبة طردية |
| 21 | Kuangazia | Enlighten-ment | التنوير |
| 22 | Kuchechemua | Activation | تفعيل |
| 23 | Kuelimisha | Education | تعليم |
| 24 | Kushughulikia kisomi na Mashariki | Orientalism | استشراق |
| 25 | Kutengeneza upya | Renewal | تجديد |
| 26 | Kutojua | Gnosticism | اللاأدرية |
| 27 | Mabaraza ya kitamaduni | Cultural saloon | الصالون الثقافي |
| 28 | Machafuko ya kisaikolojia | Psychological disturbances | اضطرابات نفسية |
| 29 | Makisio ya kiidadi | Quantitative estimation | تقدير كمي |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 30 | Makusudio ya kisharia | Purposes of Sharia | مقاصد الشريعة (الكليات الخمس) |
| 31 | Malezi | Upbringing | تربية |
| 32 | Mapinduzi ya kingono | Sexual revolution | الثورة الجنسية |
| 33 | Masambaratiko | Disunity | تفكك |
| 34 | Masambaratiko ya familia | Family disintegration | التفكك الأسري |
| 35 | Matashi | Lust/desire | الشهوانية / الشهوة |
| 36 | Mchakato wa kuelimisha | Educational process | العملية التعليمية |
| 37 | Mfumo wa kimataifa | The world system | النظام العالمي |
| 38 | Mfumo wa maumbile | The system of nature | نظام الطبيعة |
| 39 | Mikusanyiko ya kidhahania | Virtual groups | تجمعات افتراضية |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 40 | Mitandao ya kijamii | Social media | وسائل التواصل الاجتماعي |
| 41 | Msimamo mkali | Fanaticism | التشدد |
| 42 | Mwamko | Renaissance | عصر النهضة |
| 43 | Mwenye kushu-ghulika kisomi na Mashariki | Orientalist | مستشرق |
| 44 | Nadhari ya mageuzi na upandisho | Theory of evolution | نظرية النشوء والارتقاء |
| 45 | Nadhariya ya kutokea wakati mmoja | Theory of contem-poraneous existence | نظرية التعاصر الزمني |
| 46 | Nadhariya ya maendeleo ya mbele au ya upandisho | Evolutionism progression or ascen-dance | نظرية التطور التقدمي أو التصاعدي |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 47 | Nadhariya ya usilika wa umoja na uhalisi wake | Theory of innateness and authenticity of monotheism | نظرية فطرية التوحيد وأصالته |
| 48 | Ndoa ya jinsia moja | Same-sex marriage | الزواج المثلي |
| 49 | Sababu za kijamii | Social reasons | أسباب اجتماعية |
| 50 | Sababu za kisaikolojia | Psychological reasons | أسباب نفسية |
| 51 | Sababu za kiuchumi | Economic reasons | أشباب اقتصادية |
| 52 | Sababu za kiustaarabu | Civilizational reasons | أسباب حضارية |
| 53 | Sababu za kiutambuzi | Cognitive reasons | أسباب معرفية |
| 54 | Shakhsia sawia | Sound personality | شخصية سوية |
| 55 | Takwimu ya kimataifa | International statistics | الإحصاءات الدولية |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 56 | (Tovuti (saiti | Site | موقع على الإنترنت |
| 57 | Tuhuma | Suspicion | شبهة |
| 58 | Tuhuma za kifalsafa | Philosophical suspicion | شبهات فلسفية |
| 59 | Ubakaji | Rape | اغتصاب |
| 60 | Ubaradhuli | Libertinism | الإباحية |
| 61 | Ubinafsi | Individualism | الفردية |
| 62 | Ubora | Idealism | المثالية |
| 63 | Ubunifu werevu | The intelli-gent design | التصميم الذكي |
| 64 | Udarwini | Darwinism | الداروينية |
| 65 | Udhanaishi | Existential-ism | الوجودية |
| 66 | Udini | Religiosity | تدين |
| 67 | Udunia | Secularism | العلمانية |
| 68 | Ugaidi | Terrorism | الإرهاب |
| 69 | ukanamungu | Atheism | الإلحاد |
| 70 | Ukiritimba | Monopoly | احتكار |
| 71 | Ukosoaji | Criticism | نقد |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 72 | Ukuaji | upbringing | تنشئة |
| 73 | Uradikali | Radicalism | التطرف |
| 74 | Urithi wa maarifa | Heritage | التراث |
| 75 | Ushahidi wa kilimwengu | Universal evidence | البرهان الكوني |
| 76 | Ushoga | Homosexuality | شذوذ – مثلية جنسية |
| 77 | Utandawazi | Globalization | عولمة |
| 78 | Utapeli | Refutation | نقض |
| 79 | Uvumbuzi wa kisayansi | Scientific inventions | اختراعات علمية |
| 80 | Uwazi wa kiutamaduni | Cultural openness | الانفتاح الثقافي |
| 81 | Uyakinifu | Materialism | المادية |
| 82 | Uzalishaji upya wa roho | Reincarnation | تناسخ الأرواح |
| 83 | Uzemba | Negligence | إهمال |

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Utangulizi | 5 |
| Maana ya Ukanamungu | 19 |
| Historia Fupi ya Ukanamungu | 39 |
| Kwanza: Nadharia ya Maendeleo ya Mbele au ya Upandisho | 49 |
| Sababu za kuibuka kwa Ukanamungu | 95 |
| Hatari za Ukanamungu Juu ya Mtu, Familia, na Jamii | 119 |
| Misamiati na Istilahi Kiarabu – Kiingereza - Kiswahili | 227 |
| Misamiati na Istilahi Kiswahili – Kiingereza - Kiarabu | 235 |

Shirika Kuu la Vitabu la Misri.

**Msimamizi wa miradi ya kitamadani.**

**Marwan Hamad**

Mkaguzi

**Faryal Fuad**

Mtangenezaji wa jarada la kitabu

**Muhammad Baghadady**

Upande wa Ufundi

**Mirfat Antar An-Nuhas**

**Namba ya kuhifadhia kwenye kitengo cha vitabu 2022**

**ISBN**